# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

### Kikao cha Hamsini na Sita – Tarehe 29 Juni, 2017

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wa Saba, Kikao cha Hamsini na Sita.

Katibu!

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:**

Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa Mwaka 2015/2016 *(The Annual Report of Social Security Regulatory Authority for The Year 2015/2016).*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Hati ya Uhamishaji Fedha Na. 1 ya mwaka 2016/2017 *(Statement of Reallocation Warrant No. 1 of 2016/2017);* na

Hati ya Uhamishaji Fedha Na. 2 ya mwaka 2016/2017 *(Statement of Reallocation Warrant No. 2 of 2016/2017).*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha na Mipango.

Katibu!

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu; Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu. *(Makofi)*

Swali la kwanza litaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, ambaye ni Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba.

Mheshimiwa Mgumba!

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali la kwanza.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, wewe ndiye Kiongozi wa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ndani ya Bunge, lakini pia ndiye kiranja mkuu wa Serikali hii ya Awamu ya Tano. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama unavyofahamu kuna wazabuni wengi katika Halmashauri zetu tunakotoka ambao sisi ni wawakilishi wao pamoja na Serikali Kuu, walifanya kazi ya kutoa huduma katika taasisi za Serikali na Serikali yenyewe kwa muda mrefu, wengine wana miaka miwili, mitatu, wengine mpaka mitano, lakini mpaka sasa hawajalipwa stahiki zao.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ukizingatia mnamo tarehe 01 Juni ndani ya Bunge hili, ulilimbia Bunge hili kwamba malipo yanachelewa ni kwa sababu wanafanya uhakiki, ambalo ni jambo zuri, kuwagundua wale ambao wanastahili kulipwa...

**SPIKA:** Swali Mheshimiwa Mgumba, moja kwa moja!

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Spika, nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, watu hawa wamesubiri kwa muda mrefu na ukaguzi umeshafanyika zaidi ya mara tano, nini kauli ya Serikali, watawalipa lini wazabuni wote waliotoa huduma ndani ya Serikali?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgumba, Mbunge wa Morogoro Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upo ukweli kwamba, Serikali inadaiwa na wazabuni wetu waliokuwa wanatoa huduma kwenye maeneo mbalimbali. Wako ambao wametoa huduma kwenye Halmashauri za wilaya kwa maana ya huduma kwenye shule, kwenye magereza, lakini pia wako ambao wamefanya kazi za kutoa huduma kwenye Wizara mbalimbali. Na kwa mara ya mwisho nilikuwa hapa nilipata swali la aina hii linalowahusu wadai/wazabuni wa pembejeo, wote hawa ni watoa huduma ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumeweza kugundua kwamba baadhi ya madeni na baadhi ya wadai wachache miongoni mwao wametuletea taarifa za madai ambayo si sahihi sana. Na kweli, tulichokifanya tulitoa maagizo kwenye maeneo yote, ili kuhofu kupoteza fedha, kulipa fedha ambayo haikufanyiwa kazi kwa madai yale.

Kwa hiyo, tumeendesha zoezi la uhakiki chini ya Wizara ya Fedha na taasisi yetu kupitia *CAG,* hasa kule kwenye

madeni makubwa ili kujiridhisha viwango vinavyotakiwa kulipwa kwa wazabuni hawa.

Mheshimiwa Spika, tuliweka utaratibu kwamba angalao kufikia mwishoni mwa mwezi huu tuwe tumemaliza hilo zoezi la uhakiki halafu tuanze kulipa madeni haya. Kwa hiyo ni matarajio yangu kwamba Wizara ya Fedha watanipa taarifa, na Wizara zile zote ambazo zina madeni ya watoa huduma zitatoa taarifa ya viwango vya fedha, halafu sasa tusimamie Wizara ya Fedha kuweza kuwalipa hawa watoa huduma.

Mheshimiwa Spika, nataka nitumie nafasi hii, kwanza niwashukuru kwa uvumilivu wao wadeni wote wanaotudai, lakini pili tuwasihi waendelee kutuvumilia na taratibu hizi kwa lengo lilelile nililokuwa nimelieleza awali la kuokoa fedha ambazo zinalipwa kwa watu ambao hawakutoa huduma. Hata hivyo bado tutaendelea kuwatumia watoa huduma kutoa huduma ndani ya Serikali kwenye maeneo ambayo wameendelea kutoa huduma na tuwahakikishie tu kwamba tutawalipa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kama wako watoa huduma kwenye eneo lako endelea kuwahakikishia kwamba Serikali tutlipa madeni. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mgumba, kuna haja ya nyongeza? Hebu tujaribu eeh, maana ahadi umeshapata!

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kuna swali dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu mazuri ambayo kutoka Serikalini.

Swali dogo la tu la nyongeza, kwa kuwa kama ulivyosema kwenye majibu yako ya msingi, kwamba mmegundua kuna watu ambao wameleta madai ambayo

si sahihi, lakini naamini pia kuna watu ambao watakuwa madai yao ni sahihi. Sasa nini kauli ya Serikali kwa wale ambao madai yao ni sahihi ambao wamekaa muda mrefu kiasi kwamba imewaongezea gharama kwa maana ya riba sehemu walizokopa, nani atalipa gharama hizi kwa ajili ya usumbufu uliotokea na gharama zilizoongezeka kwenye madeni hayo? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mgumba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu la awali kwamba kwanza tunathamini sana kazi waliyoifanya katika kutoa huduma kwenye sekta zetu. Lakini mbili, tumewashukuru kwa uvumilivu kwa kipindi chote hiki ambacho sisi tunafanya uhakiki. Baadhi ya wadai nimepata nafasio ya kukutana nao hapa Dodoma wakati huu wa Bunge na kuzungumza nao na kuwaambia kwa nini tumechelewa kuwapa fedha zao, wale ambao kweli wana madai halali.

Mheshimiwa Spika, lakini bado nirudi tena kusema kwamba, hatuna namna nyingine ya kufanya zaidi ya uchelewaji huu wa kulipa kwa sababu tuko kwenye zoezi la kuhakiki, ili tujiridhishe. Kama ingekuwa tumechelewa tu, kwamba hatuna kazi yoyote, tumeacha tu hapo kungekuwa na swali ambalo naamini unacholenga kingeweza kupata maelezo. Lakini bado niwahakikishie kwamba taratibu zinakamilika na tulisema tunakamilisha tarehe 30 Juni, yaani kesho tu tarehe 30 Juni, tunatarajia Wizara ya Fedha itapewa taarifa kutoka kwenye Wizara mbalimbali, kwamba madai yetu halali ni haya kwa ajili ya watu hawa kwa huduma waliyoitoa, baada ya hapo tunalipa tu na tutaendelea kuwapa nafasi zaidi ya kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niwahakikishie kwamba wataendelea kutoa huduma, hasa wale ambao ni waaminifu kwenye awamu ijayo hii ya mwaka wa fedha mpya wa mwaka 2017/2018.

**SPIKA:** Swali la pili kwa siku ya leo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu linatoka kwa Mbunge wa Mbulu Mheshimiwa Flatei Gregory Massay. Mheshimiwa Massay tafadhali swali fupi.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni Serikali imefanya uhakiki wa vyeti *fake* na imeacha ma-*gap* na mapengo katika maeneo yetu hasa ya vijijini kwa upande wa afya.

Je, lini sasa Serikali mtatusaidia ili vituo vyetu au zahanati ziweze kuendelea kutokana na nafasi hizo ambazo sasa zimechwa wazi?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba arudie tena swali, maana kulikuwa na msikiko usio sahihi kwenye vipaza sauti vyetu.

**SPIKA:** Tafadhali, kwa kifupi!

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya uhakiki wa watumishi ambao wana vyeti *fake.* Sasa baada ya uhakiki huo wengine wameacha vituo vya afya na zahanati zetu kule.

Sasa swali langu, je, lini mtaajiri sasa, ili watu wetu kule wapate huduma, hasa kwenye maeneo ya afya ambako watumishi wameshaacha kazi kutokana na kwamba, walikuwa wana vyeti ambavyo havistahili kuendelea kuwepo? Ahsante.

**SPIKA:** Kuziba mapengo ya mapungufu ya watumishi waliopunguzwa kutokana na vyeti *fake.*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Massay, Mbunge wa Mbulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumepitisha zoezi hili la uhakiki wa vyeti kwa watumishi wetu na uhakiki huu baada ya kuwa tumekamilisha tulipata makundi matatu. Kundi la kwanza ni wale wenye vyeti *fake* moja kwa moja, kundi la pili ni wale wenye vyeti vinavyotumika na zaidi ya mtu mmoja, lakini kundi la tatu uko utata wa majina ambao umejitokeza kwenye vyeti hivi ambavyo wao wamepata nafasi ya kukata rufaa. Sasa wote hawa wameacha pengo kwa sasa, na ndilo ambalo Mheshimiwa Mbunge amelizungumzia, lini tunatoa ajira.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli ametoa nafasi za ajira zaidi ya 50,000 ili kuziba mapengo haya ambayo yamejitokeza kwa wenye vyeti *fake,* lakini vilevile ili kuongeza tu ajira kwenye sekta nyingine kwa lengo la kuboresha utoaji huduma kwenye sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tayari vibali vimeshatolewa na Wizara ya Utumishi, tumeanza na idara ya elimu, tumesha ajiri walimu wa masomo ya sayansi wamekwenda kwenye vituo, tumetoa pia nafasi kwenye sekta ya afya na vibali hivi vitaendelea kutolewa kadri ya nafasi ambazo Mheshimiwa Rais ameahidi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaamini Rais wetu mpendwa kwa ahadi yake nafasi hizi ataendelea kuzitoa ili tuzibe mapengo na kuboresha pale ambako kuna upungufu mkubwa. Na sasa ajira hizi zitaenda kitaaluma zaidi, ili kuweza kuleta ufanisi mkubwa kwenye sekta y ajira. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Munde Tambwe, Mbunge wa Tabora Viti Maalum. Mheshimiwa kuna swali la nyongeza tena kweli? Mheshimiwa Munde Tambwe kama hayupo tunaendelea. Mheshimiwa Martha Moses Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante; na mimi nashukuru kupata nafasi ili nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa, tarehe 15/05/2017 Serikali ilitangaza rasmi kuivunja Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma na majukumu yake kuhamishiwa Manispaa ya Dodoma, kwa hilo naipongeza Serikali. *(Makofi)*

Lakini kwa kuwa baadhi ya wananchi hata Waheshimiwa Wabunge pia walikuwa tayari wameshalipia viwanja na walikuwa hawajakabidhiwa. Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu jambo hili? Ahsante.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Rais alitoa agizo la kuvunja Mamlaka ya *CDA* na mamlaka hiyo na majukumu yake kuyahamishia Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kupitia Manispaa ya Dodoma. Kazi hiyo imeshafanywa na zoezi linaloendelea sasa kwanza wale watumishi wote wa *CDA* watahamishiwa Manispaa ya Dodoma, lakini tutafanya mchujo kidogo, wale ambao walikuwa na malalamiko, wanalalamikiwa na wananchi wale wote tutawaweka pembeni, kwa sababu tunataka tupate timu mpya ambayo inafanya kazi vizuri.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbili, tunaendelea sasa na uhakiki na ukaguzi wa kina kwenye masuala ya fedha na utumishi wenyewe ili tuweze kuanza vizuri, tujue *CDA* ilipoacha iliacha na fedha kiasi gani na shughuli zake zilifikia hatua gani halafu pia kuweza kuendelea, lakini majukumu yote yanabaki kama yalivyokuwa na *CDA* yataendelea kufanywa na Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma. Kinachobadilika pale ni maandishi, kama kwenye risiti zilikuwa zinasomeka *CDA,* sasa zitasomeka Manispaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha utaratibu huu mpango kazi wote utaendelea kama ulivyokuwa. Kama kuna mtu alilipa nusu anataka kumalizia, wataendela kukamilisha malipo yao, kama kuna mtu alishakamiliha hajapata kiwanja, ataenda kukabidhiwa kiwanja chake na namna yoyote ya utendaji wa kawaida utaendelea. Sasa hivi akaunti zote zimefungwa kwa hiyo, huwezi kulipa mpaka hapo tutakapofungua malipo.

Mheshimiwa Spika, tutamuagiza Mkurugenzi sasa wa Manispaa, atoe maelezo sahihi kwa Wana Dodoma na kwa Wananchi, Waheshimiwa Wabunge mkiwemo ili kila mmoja aweze kujua, lakini kwa kauli hii ndio usahihi wa taarifa ya *CDA* kwa namna ambavyo tumeivunja na tumehamishia Mamlaka pale Manispaa ya Dodoma na watumishi wote sasa watawajibika kwa Mkurugenzi wa Manispaa na hakutakuwa na chombo kingine pale.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ambayo tumewaelekeza sasa pale *CDA* kwenye Idara ya rdhi, kwenye lile jengo lisomeke Idara ya Ardhi - *CDA* na huko ndani tume-*plan* sasa Wizara ya Ardhi ipeleke mtu anayeandika Hati. Tunataka pale ndani iwe *One Stop Centre.* Ukienda kuomba ardhi, ukishapimiwa, ukishalipia, hati unapata humo humo kwenye hilo jengo. Kwa hiyo, tunataka turahisishe upatikanaji wa hati na viwanja kwenye jengo hilohilo moja, ukiingia ndani ukitoka unatoka na hati yako badala tena kwenda mahali pengine. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, Wana Dodoma, mambo *mswano* hayo.

Mheshimiwa Martha Mlata, bado kuna swali?

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana kwa majibu ambayo hakika yameponya nyoyo za watu ambao walikuwa wanaguswa sana na suala hili la *CDA.* Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa umesema mamlaka haya; na umeeleza vizuri Halmashauri ya Manispaa ya

Dodoma itakavyofanya kazi, naamini na Halmashauri nyingine nchi nzima zitafanya kazi kama ambavyo umetoa maelekezo.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo moja tu, kwamba wanapokwenda kuchukua ardhi kutoka kwa wamiliki au kwa watu ambao wanahodhi zile ardhi zao, wanalipa fidia kwa fedha ndogo sana, lakini wanapokuja kupima na kutaka kuviuza wanauza kwa bei ambayo ni tofauti na ile gharama ambayo walinunulia.

Je, Serikali hapa inaweza pia ikatoa maelekezo kwamba, angalau uwiano wake usipishane sana kwa ajili ya kuwanufaisha hata wale wahusika wa maeneo ambayo yanakuwa yamechukuliwa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Hilo swali ni la nchi nzima. Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mlata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ziko sheria ambazo zinaongoza fidia na ndizo ambazo tunazifuata. Fidia hizi kuna watu ambao wamepanda mazao kwenye ardhi, lakini wengine hawajapanda chochote. Kwa hiyo, mabadiliko ya bei ama tofauti ya bei inatokana na ambavyo mwenye ardhi alivyoweza kuwekeza kwenye eneo lile. Kama kuna mazao yoyote yanafanyiwa tathmini na tunalipa kwa mujibu wa bei na taratibu zilizopo kisheria.

Kwa hiyo, bado tutasisitiza mamlaka zote za halmashauri zote za Wilaya, Miji na Manispaa na Majiji kufuta sheria zile ambazo zimeelekezwa katika kufanya fidia. Na tumesemea ardhi ya mtu isichukuliwe bila fidia, kwa hiyo, bado hili litaende kuzingatiwa. Na agizo hili naomba wazingatie maeneo yote haya ambayo nachukua ardhi ya mtu, kwamba lazima alipwe kwanza ndipo uweze kuchukua, ili kuondoa migogoro ambayo siyo muhimu kwa sababu sheria ipo na inatuongoza kufanya hivyo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali la mwisho la Waziri Mkuu kwa siku ya leo. Linatoka kwa Mheshimiwa Ritta Esnepher Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu hivi karibuni Serikali imetoa tamko la kutosafirisha chakula nje ya nchi, lakini kuna baadhi ya mikoa ambayo imezalisha chakula cha kutosha cha ziada kinachoweza kusafirishwa hata nje ya nchi. Je, Serikali inatoa ufafanuzi gani kuhusiana na utekelezaji wa tamko hilo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Iringa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jambo hili nimelizungumza siku ya Idd Mosi nikiwa kwenye sherehe ya Idd kwenye Baraza la Idd kule Mjini Moshi, Mkoani Kilimanjaro. Nilizungumza kwa msisitizo kwamba tumedhibiti na tumezuia usafirishaji wa chakula na hasa mahindi nje ya nchi kwa sababu historia yetu sisi kuanzia mwaka wa jana mwezi Novemba, 2016 mpaka Februari, 2017 nchi yetu ilikosa mvua za msimu unaotakiwa na tutapata usumbufu mkubwa ndani ya nchi kwa maeneo mengi kukosa chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, na chakula kikuu sasa nchi Tanzania naona utamaduni umebadilika, nilikuwa nazungumza pia na Mheshimiwa Mbatia hapa kwamba utamaduni umebadilika, Wachaga, Wahaya sasa badala ya kula ndizi wanakula ugali. Wamasai waliokuwa wanakula nyama tu pekee sasa wanakula ugali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo utakuta mahindi yanatumika sana kuwa ni chakula kikuu nchini na kwa hiyo lazima tuweke udhibiti wa utokaji wa mahindi ili yaendelee kutusaidia kama chakula kikuu hapa nchini kwetu.

Kwa hiyo tumeweka zuio, na hasa baada ya kuwa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa Kilimanjaro ilitoa taarifa kwamba kuna utokaji wa mahindi mengi kwenda nchi za nje kwenye mipaka yetu. Na siku ile nilipokuwa Kilimanjaro malori kumi yalikamatwa yakiwa na mahindi yakivushwa kwenda nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo lazima tuweke utaratibu na ninyi wote ni mashahidi kwamba uzalishaji huu haukuwa wa uhakika sana kuanzia mwezi Machi mpaka mwezi Mei, kwa miezi mitatu. Maeneo machache yamezalisha sana kama ulivyosema Mheshimiwa Ritta Kabati lakini maeneo mengine hayana chakula. Juzi nilikuwa Mwanza nikiwa pale Usagara, *Kigongo Ferry* nilisimamishwa na wananchi, moja kati ya tatizo walilolieza ni upungufu wa chakula. Nimeona, hata Sengerema mahindi yote yamekauka, Geita mahindi yote yamelimwa yamekauka. Kwa hiyo, bado tuna tatizo la upungufu wa chakula. Pia bei za chakula chetu iko juu sana hatuna namna nyingine ni kudhibiti chakula chetu.

Mheshimiwa Spika, na nilieleza kwamba nchi nyingi za jirani hazina chakula. Sisi tuna barua hapa kutoka Congo, South Sudan tumepata kutoka Somalia na nchi za jirani wanaomba kupewa msaada wa chakula kutoka Tanzania wakati sisi wenyewe hatuna chakula cha kutosha. Kwa hiyo, ni muhimu sana kwa Serikali na wananchi mkatuunga mkono katika hili, kudhibiti utokaji wa chakula, na hasa mahindi yanayokwenda nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nimeeleza kwamba sisi tulichofanya ni kudhibiti kutoa mahindi nje bila kibali. Na kama kuna umuhimu wa kupeleka mahindi nje basi tunataka yasagwe ndani ili yapelekwe, kwa sababu ukisaga tunafaida zake, pumba tunazipata, tunazitumia kwa chakula cha mifugo lakini pia mashine zetu ambako tuna msizitizo wa viwanda vitafanya kazi ya kusaga, tutakuwa na ajira, lakini tunapotoa mahindi maana yake tunatoa kila kitu huku ndani tunakuacha tupu. Kwa hiyo, lazima tuwe na mpango ambao utasaidia sasa, sisi wenyewe Watanzania kunufaika kupitia zao hili.

Mheshimiwa Spika, bado msimamo ni ule ule kwamba tumezuia mahindi kutoka nje ya nchi na kama ni lazima basi aende Wizara ya Kilimo akaombe kibali kama ni lazima Wizara ikiona inafaa utapata kibali, lakini kibali hicho ni cha kutoa unga na si mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote ni mashahidi, jana tumepata taarifa malori zaidi ya 103 kwa siku nne kutoka siku ya Idd mpaka leo hii, malori 103. Je, kwa mwezi mzima tutakuta na mahindi hapa ndani?

Mheshimiwa Spika, tunazo taarifa kupita Kamati za Ulinzi na Usalama kwamba wengi wanaofanya biashara kuja kuchukua mahindi Simanjiro, Kibaya kwa maana ya hapa katikati maeneo ya Kongwa ni watu kutoka nje ya nchi ndio wanaokuja kuchukua. Kwa hiyo hatuna faida sana hao kuingia zaidi ya kwamba wanatuachia fedha. Hivyo tunaitengeneza shida ambayo tutakuja kuanza kuuliza tutapateje chakula ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Watanzania kwa jambo hili naomba mtuunge mkono kwa sababu tunachofanya ni kwa maslahi ya nchi, hatimaye bei zitapanda tutashindwa kununua mahindi na wote mnajua angalau sasa mahindi yamepungua kwenye masoko

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuendelee na hali hiyo ili chakula kiwe cha kutosha baada ya kuwa tumefanya tathimini tukijiridhisha kwamba chakula cha ndani cha kutosha kipo na tuna akiba kutoka kwenye maeneo yanayozalisha sana basi vibali hivyo vinavyotolewa kwa utaratibu vitaendelea kutoka, na wale ambao wanataka kufanya biashara nje ya nchi wataendelea kupata fursa ya kufanya biashara nje ya nchi. Lakini kwa sasa tumezuia; na ninataka nimpongeze sana Mkuu wa Mkoa ya Kilimanjaro mama Anna Mghwira na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama kwa kuendelea kusimamia.

Mheshimiwa Spika, tumeona malori yale agizo limebaki pale pale, mahindi yale ambayo yatakuwa

yamaekamatwa; na tumejihisi kwamba yalikuwa yamekwenda nje ya nchi, yote yataingizwa kwenye hifadhi ya taifa, na hayo malori yanyofanya biashara hiyo yote yatabaki kituo cha polisi. Lakini pia kwa namna ambavyo wanaendelea na waendelee kwa utaratibu wote na maagizo yetu yatabaki vilevile ili tuweze kuwahudumia Watanzania ndani ya nchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu ya maswali haya. Katibu tunaendelea na maswali.

**NDG. CHARLES J. MLOKA:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 462

**Ahadi ya Ujenzi wa Nyumba za Watumishi Wilaya ya Itilima**

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO (k.n.y MHE. NJALU D.SILANGA)** aliuliza:-

Wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu mwaka 2015, Mheshimiwa Rais aliahidi kujenga nyumba za watumishi katika Makao Makuu ya Wilaya ya Itilima katika Kijiji cha Langabidili.

Je, ni lini ahadi hiyo itaanza kutekelezwa?

**NABU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mbunge wa Itilima kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Itilima ni kati ya Wilaya tano zinazounda Mkoa wa Simiyu. Wilaya hii ilianzishwa

mwaka 2012 kwa *GN* Na. 73, na Halmashauri yake ilianzishwa mwezi Mei, 2013 kwa *GN* Na. 47. Wilaya ya Itilima imezaliwa kutoka katika Wilaya ya Bariadi na kuunda Mkoa wa Simiyu wenye Wilaya tano na Halmashauri sita. Watumishi wa Halmashauri wanalazika kuishi Bariadi Mjini na kusafiri umbali wa kilometa 33 kila siku kutoka Bariadi hadi Makao Makuu ya Wilaya kwa ajili ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na usumbufu na gharama za usafiri Serikali ilitoa shilingi milioni 500 kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi na kulipa fidia maeneo ya wananchi. Hadi sasa ujenzi wa nyumba nne unaendelea katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali ilitenga shilingi milioni 230 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba nne za wananchi. Aidha, Serikali imetoa shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji. Ujenzi unaendelea na unatekelezwa na Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA).*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/ 2018, Serikali imetenga shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba nyingine nne za watumishi. Serikali itaendelea kutenga fedha kidogo kidogo kwa kadri zitakavyopatikana ili kuweza kukamilisha nyumba za watumishi.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika**,** ahsante sana. Kwanza kabisa napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Nina maswali mawili tu madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ujenzi unaendelea, lakini unaendelea kwa kasi ndogo sana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wanatoa fedha kwa wakati na kuhakikisha ujenzi huo unaendelea kwa haraka ili ukamilike, kwa sababu watumishi wanapata shida sana kusafiri kutoka Bariadi hadi Ligangabilili?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali ina mpango gani juu ya kuikaribisha *National Housing* (Shirika la Nyumba la Taifa) kwenye Mkoa wa Simiyu kuweza kujenga nyumba za *National Housing* katika mkoa nzima yaani katika wilaya zake zote tano ili kuweza kuwasaidia wafanyakazi kupata makazi mazuri ya kuweza kuishi? Ahsante sana.

**NABU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa ajenda ya kasi ndogo ya utendaji wa kazi naomba nichukue *concern* hiyo, tutafanya *follow up* kuangalia ni kinachoendea. Nilifika pale Itilima, ni kweli changamoto kubwa ilikuwa ni tatizo la fedha. Tukaja kufanya uhangaikaji katika ofisi yetu ndiyo maana tukapata zile fedha nyingine zikaenda kule, ili kuweza kuongeza *speed* ya ufanyaji wa kazi pale. Vilevile tutawasiliana na wenzetu wa Itilima ili kuangalia kuna kitu gani ambacho kinakwaza. Nia ni kuongeza *speed* ya utendaji wa kazi ili hatimaye wananchi na hasa watumishi wa Itilima waweze waweze kukaa katika mazingira rafiki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la *National Housing* kuweza kukaribia katika Mkoa wa Simiyu kwa ajili ya kujenga nyumba; ni wazo nzuri, na niwashukuru sana wenzetu wa *National Housing* wamekuwa wakishiriki ujenzi wa nyumba katika maeneo mbalimbali. Hata hivyo ninaamini kwamba tutapata maelekezo vizuri juu ya nini cha kufanya kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambayo ni Wizara yenye dhamana katika eneo hilo, hasa katika Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi sana wanaambiwa kwamba watenge maeneo maalum kwa ajili ya kuwakaribisha *National Housing.* Hata hivyo kuna maeneo mengine *National Housing* walijenga nyumba lakini matumizi ya zile nyumba imekuwa ni changamoto kubwa na sana katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuchukue kama ni *challenge* nyingine katika upande wetu vilevile, kwamba endapo *National Housing* wanakuja kuwekeza basi lazima

nisiamasishe Halmashauri tuwe tayari kuhakikisha kwamba tunazitumia nyumba hizo, kwa sababu fedha hizi zisipotumika vizuri tutatengeneza gharama kubwa kwa Serikali yetu. Kwa hiyo, ni wazo zuri Mheshimiwa Nyongo na mimi kama TAMISEMI nitalichukua jambo hili, nitaongea na dada yangu Mheshimiwa Angelina, Naibu Waziri wa Ardhi tuangalie namna ya kufanya ili wananchi wa Simiyu waweze kufanya kazi kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa Simiyu.

**SPIKA**: Nimekuona Mheshimiwa Maryam Msabaha swali la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi kabla ya Maryam Msabaha.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI:** Mheshimiwa Spika, Ahsante sana. Napenda kujibu swali la nyongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri alivyojibu majibu yake mazuri kuhusiana na suala la *National Housing.*

Kwa Mkoa wa Simiyu tayari *National Housing* wana maeneo waliyopewa katika Wilaya mbili, Wilaya ya Busega pamoja na Wilaya ya Bariadi. Tatizo lililoko katika wilaya zingine ni kwamba bado hawajawa tayari kutenga maeneo.

Mheshimia Spika, kwa maelekezo ambayo pia Mheshimiwa Rais alitoa kwamba *National Housing* ili waweze kujenga na waweze kutoa nyumba zao kwa bei nzuri lazima Halmashauri husika iwe imeshatenga eneo ambalo halina changamoto kwa maana kwamba litahitaji fidia, litahitaji miundombinu. Kwa hiyo, wao wafanye maandalizi tayari viwanja waweke *National Housing* watakwenda kujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili pia, kuna Wilaya zaidi ya 30 ambazo *National Housing* wamejenga na nyumba zile zinaharibika, ikiwemo Mkoa wa Rukwa, nyumba zimejengwa lakini watu hawajaingia wala hawajapanga. Kwa hiyo, wakati mwingine ku-*pull up resources* katika maeneo mengine inakuwa ni ngumu; na katikati hapa walisimama kwa ajili ya kuendeleza eneo la Iyumbu. Kwa hiyo halmashauri yoyote itakayokuwa tayari *National Housing* wataweza kuja,

lakini tuwaombe pia mfanye maandalizi yale ya msingi ili *National Housing* waweze kushiriki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Msabaha.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nipate kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa watumishi wengi wa Serikali wamehamishiwa Mkoa wa Dodoma, je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha watumishi wote wa Serikali wanapata nyumba na waache kuhangaika hangaika mitaani kwa sababu nyumba za *National Housing* hazitoshi kwa watumishi wa Serikali waliohamishiwa Dodoma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI majibu ya swali hilo muhimu.

**NABU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la *mate* wangu wa Bulombora dada yangu Mheshimiwa Maryam Msabaha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli, ni nia njema Serikali. Tumesema kwamba Serikali ya Awamu ya tano si *mlimila dole,* kwamba inatekeleza kile ilichokiahidi; imesema tunaamia Dodoma na tumehamia sasa hivi Dodoma. Naomba niwahakikishie kwamba Serikali imeweka mipango vizuri kupitia nyumba za *TBA*, *National Housing* na *CDA.* Mkiangalia kule kama mnapita *Iringa Road* zimekarabatiwa, lengo lake kubwa ni kwamba kuweza kuwa-*accommodate* watumishi wote wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunashukuru sana kwa suala hili zuri, Serikali imeweka mpango vizuri. Niwaahakikishie watumishi wote kwamba msiwe na hofu mtakapokuja Dodoma, Serikali inapanga mipango mizuri, na ndiyo maana hata *National Housing* sasa wanajenga huu mji mpya pale. Hii yote ni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kwenye mchakato

huu wa Mji Mkuu wa Serikali kuhamia Dodoma, Dodoma iweze ku-*accommodate* watumishi hawa wanaokuja hapa.

**SPIKA:** Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Swali linaulizwa na Mbunge wa Ukerewe, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi.

Na. 463

**Serikali kutoa Posho kwa Watumishi wa Maeneo ya Pembezoni**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Watumishi walio maeneo ya pembezoni mwa nchi ikiwemo Wilaya ya Ukerewe wanafanya kazi katika mazingira magumu, mfano walimu wa watumishi wa afya.

Je, Serkali ina mpango gani wa kutoa posho ya mazingira magumu kwa watumishi wa maeneo ya pembezoni?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Jimbo la Ukerewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba watumishi walio katika Halmashauri zilizo katika maeneo ya pembezoni ikiwemo Wilaya ya Ukerewe hufanya kazi katika mazingira magumu na upungufu mkubwa wa watumishi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010 Serikali ilipitisha Sera ya Malipo ya Mishahara na Motisha katika utumishi wa umma ambayo miongoni mwa malengo yake mahsusi ni kuwavutia, kuwapa motisha na kuwabakiza watumishi katika utumishi wa umma. Lengo ni kupunguza tatizo la uhaba wa watumishi katika Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza sera hii mwaka 2012/2013 Halmashauri 33 za Wilaya, ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe ziliwezeshwa kuandaa miongozo ya kutoa motisha kwa watumishi wake. Kutokana na zoezi hilo Halmashauri 29 ziliandaa na kuwasilisha katika ofisi yangu miongozo iliyoabainisha aina za motisha zinazohitajika kwa ajili ya watumishi wake. Utekelezaji wa miongozo hiyo kwa Halmashauri zote 29 ulikadiriwa kugharimu jumla ya shilingi bilioni 331.087 kwa mwaka, ambapo kati ya hizo kiasi cha shilingi bilioni 314.372 kilihitajika kwa ajili ya miradi ya maendeleo na kiasi cha shilingi bilioni 16.761 kilihitajitaka kwa ajili ya matumizi ya kawaida na utekelezaji wa miongozo hii ulitarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2013/2014. Hata hivyo, utekelezaji wa miongozo hii haujaanza kutokana na ufinyu wa bajeti ya Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mkundi swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL J. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inakiri kwamba Ukerewe ni moja kati ya maeneo ambayo watumishi wake wanafanyakazi katika mazingira magumu na kwa kuwa huduma za elimu na afya visiwani Ukerewe hususan kwenye Visiwa vya Ilugwa, Ukara, Bwilo na kwingineko zinaadhirika sana na changamoto zinazowakabili watumishi kwenye maeneo haya.

Je, Serikali iko tayari kutoa fedha na kuwezesha sera hii ya malipo ya mishahara na motisha katika utumishi wa umma kuanza kutekelezwa ili kuokoa maisha na mazingira ya wakazi wa visiwa hivi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mwanzoni mwa mwaka huu Serikali ilisambaza walimu kwenye Halmashauri zetu hasa walimu wa sayansi lakini kumekuwa na malalamiko mengi sana kutoka kwa walimu hawa kuishi katika mazingira magumu sana kwa sababu ya kutolipwa

stahiki zao. Je, nini kauli ya Serikali juu ya tatizo hili? Nashukuru sana.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Kairuki.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NAUTWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli ukiangalia si tu kwamba wananchi wa Ukerewe wanaadhirika kutokana na ukosefu wa huduma za elimu na afya, lakini hata watumishi wenyewe walio katika mazingira magumu pia huduma ya elimu katika eneo lile na afya inapokuwa si nzuri inawafanya pia na wenyewe wasivutiwe kufanya kazi katika maeneo hayo. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeiona changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba kwa ujumla wake mwongozo huu haujaanza kutekelezwa lakini kupitia Bajeti ya Serikali na kupitia bajeti za Halmashauri ambazo zimepitishwa wameshaanza kutekeleza maeneo mbalimbali ikiwemo sekta ya elimu pamoja na afya.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba tutaendelea kulifanyia kazi kama Serikali kutoa msisitizo ili kuhakikisha kwamba maeneo haya yanayokabiliwa na changamoto hizi basi yanaweza kutengewa fedha za bajeti za kutosha ili kuweza kutekeleza sera hii.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili kuhusiana na walimu wa sayansi na hesabu walipangiwa vituo mwaka huu, kwamba hawajalipwa stahiki zao. Kwa kweli ni jambo ambalo limetusikitisha, na haswa ukizingatia katika Halmashauri moja unakuta mtu amepangiwa walimu 12 tu, inakuwaje Halmashauri inashindwa kuwahudumia kwa watumishi wake wapya waliopangiwa katika kituo kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, niseme kupitia hadhara hii natoa tamko au agizo kwa Halmashauri zote zilizopokea walimu

wapya wa sayansi na hesabu lakini pia zilizopokea wataalam wa maabara za sayansi zihakikishe ndani ya siku saba zimewalipa watumishi hao stahiki zao zote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Martha Umbulla swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hamasa kubwa kwa vijana waajiriwa katika shule zetu hasa za maeneo ya pembezoni pamoja na vituo vya afya na zahanati, ni kule kuwepo kwa mitandao ya simu na umeme wa uhakika, kwa kuwa vijana wetu kwa kweli wanapenda kutumia simu za mikononi katika mitandao hiyo kwa uhakika; na kwa kuwa maeneo yetu ya vijijini hasa katika Mkoa wetu wa Manyara na kwingineko maeneo ya pembezoni, huduma hiyo ya umeme na mitandao ya simu haipo.

Je, Serikali hasa Wizara ya Utumishi ina mikakati gani mahususi ya kuwa na mawasiliano ya karibu kuhakikisha kwamba katika maeneo ya pembezoni katika shule hasa za sekondari na vituo vya afya kunakuwepo na umeme ili kutia hamasa ya waajiriwa waendelee kuishi maeneo hayo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nipende tu kusema kwamba kwa utafiti uliofanywa na bodi yetu ya mishahara katika utumishi wa umma mwaka 2014/ 2015, moja ya changamoto ambazo zilibainika, kwanza katika mazingira haya magumu inategemeana na sekta kwa sekta maeneo mengine jiografia, hali ya miundombinu, huduma za kijamii zilizopo; lakini pia nafurahi kwamba ametaja suala zima la mitandao ya simu pamoja na umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipende kumuhakikishia tu kwamba kupitia ripoti ile ya utafiti tulitoa maelekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, lakini pia tumewasilisha katika Wizara husika ikiwemo Wizara ya Nishati na nyinginezo kuhakikisha kwamba wanapopanga mipango yao ya maendeleo basi wanatoa vipaumbele katika maeneo haya yenye mazingira magumu.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa, lakini wakati tunaendelea Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Jaffo, hawa walimu wa sayansi ambao walipangiwa kwenye Halmashauri mbalimbali wamekuwa wakipangiwa huko kwa kupangwa moja kwa moja kutoka TAMISEMI; nafikiri jambo hili mliangalie lina matatizo makubwa sana. Ni vizuri Halmashauri zenyewe zikaangalia maeneo ambayo wana uhaba mkubwa zaidi wa walimu wakaweza ku-*allocate.* Shule kadhaa hazina walimu kabisa, ukiuliza kwa nini unaambiwa wanakuja wameshakuwa *allocated* kwenda kwenye shule ambazo tayari zina walimu, kwa hiyo, tatizo linaendelea kuwa kubwa. *(Makofi)*

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed, Mbunge wa Bumbwini, kwa niaba yake Mheshimiwa Abdallah Mtolea.

Na. 464

**Tatizo la Kuvuja Kwa Mitihani Nchini**

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA (K.n.y MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED)** aliuliza:-

Kumekuwa na tatizo la kuvuja kwa mitihani ya Taifa hapa nchini hususani ile ya kidato cha nne *(CSEE)* hali inayoondoa ufanisi hasa ikizingatiwa matokeo yanayotoka yamejaa udanganyifu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti tatizo hili?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed, Mbunge wa Bumbwini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweza kudhibiti na kuondoa tatizo la kuvuja kwa mitihani ya kidato cha nne, ambapo kwa mara ya mwisho ilikuwa ni mwaka 2008 katika somo la hisabati pekee. Changamoto inayoendelea kujitokeza ni kwa baadhi ya watahiniwa kujihusisha na udanganyifu wakati mitihani inapofanyika kwa kuingia katika chumba cha mtihani na vitu visivyoruhusiwa kama vile *notes* na simu ya mkononi kwa ajili ya kufanya mawasiliano ndani ya chumba cha mtihani.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kujidhatiti na kuikabili changamoto ya udanganyifu katika mitihani kwa kuimarisha usimamizi na kutoa elimu kwa watahiniwa kuhusu madhara ya kufanya udanganyifu. Wizara imekuwa ikitoa adhabu ikiwa ni pamoja na kufutiwa matokeo ya mitihani pale inapothibitika kuwepo kwa udanganyifu huo. Mfano, watahiniwa waliofutiwa matokeo ya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2011 ni 3,303, mwaka 2012 ni 789, mwaka 2013 ni 272, mwaka 2014 ni 184, mwaka 2015 ni 87 na mwaka 2016 ni 126.

**SPIKA:** Mheshimiwa swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, umekuwa ni utaratibu wakati wa mtihani wa kidato cha nne Serikali inapeleka askari tena askari wenye silaha kwenda kuwasimamia watoto wakati wanafanya mtihani. Kitendo hiki kinawatia uoga wanafunzi kwa sababu hawajazoea kusimamiwa na askari wakati

wakifanya mitihani au wakati wanajisomea, hivyo wanapoteza *concentration* katika mitihani na hii inawapeleka wengine kufeli.

Je, Serikali haina njia mbadala ya kuhakikisha kunakuwa na ulinzi lakini usiotisha kama vile kuweka askari ambao hawana *uniform* na hawana silaha ili waweze kuwasimamia watoto hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tunaaminishwa kwamba mtihani wa mwisho sio pekee ndiyo unaomfanya mtoto afaulu katika mitihani yake ya kumaliza kidato cha nne, kwamba *continuous assessment* inachukua asilimia 50 na mitihani ya mwisho inachukua asilimia 50, kama hili ni kweli kuna sababu gani ya kuweka ulinzi mkubwa wakati wa mtihani wa mwisho wakati ule unachangia tu asilimia 50? Je, ulinzi huo pia unawekwa kwenye zile *continuous assessment* ili kufanya usawa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, anachouliza Mheshimiwa watoto wa Kibiti wapi kule wakiona bunduki zile mtihani watafanya kweli? Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kimsingi tunapoweka ulinzi lengo si kuwatisha watahiniwa bali kuhakikisha kwamba mazingira hayo yanakuwa salama kabisa. Kama ambavyo imeshuhudiwa katika siku za karibuni, hali ya uhatarishi imekuwa ikijitokeza katika aina tofauti tofauti. Kwa kweli siamini kama wanafunzi wa Kitanzania wanaweza wakamuogopa askari kwa sababu ni maisha yao ya siku zote, hawezi akawa hamuoni kabisa askari, karibu kila mahali nchi hii imeimarisha ulinzi na askari kama polisi tuko nao siku zote tena kuna ulinzi jumuishi na shirikishi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa misingi hiyo mimi nadhani kwamba lengo la muhimu lieleweke kwamba ni kuhakikisha kwamba tunaweka mazingira salama kabisa ambayo wanafunzi wale badala ya kuogopa askari kwao ni

suala la usalama ili wafanye mitihani yao bila kupata uhatarishi wa aina yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kupimwa kwa kufuata matokeo endelevu *(continuous assessment),* ni kweli tumekuwa tukifanya hivyo na hiyo haiwezi kuwa ndio sababu ya kusema kwamba kwa sababu *marks* tunazozitegemea mwishoni ni asilimia 50 tu, basi tusiwawekee mazingira ya usalama. Tutaendelea kufanya hivyo, na kwa sababu umetoa hoja hiyo, tutafanyia kazi kama tukiona kweli mwanafunzi anaogopa sana askari tutajua namna bora zaidi ya kufanya.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Waitara na Mheshimiwa James Mbatia.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naomba niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mitihani ya kidato cha nne tunajua inatumika kwa lugha gani lakini kuna mitihani ya darasa la saba ambapo mitihani hii inatungwa maswali ya kuchagua yote. Sasa nilikuwa naomba niiulize Serikali ni lini mtaanza kutunga mitihani ambayo si ya kuchagua, hasa katika masomo ya hesabu ili watoto wetu wapimwe uelewa badala ya kuchagua na wengine wanabahatisha kufaulu kwenda sekondari? Swali langu ni hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na mtazamo wa wadau tofauti tofauti katika maswali ya kuchagua hasa katika mitihani ya hisabati. Serikali nasi pia tumekuwa tunaliangalia hilo japo katika utafiti uliofanyika ilionesha kwamba kuchagua peke yake hakumwezeshi mtu kufaulu isipokuwa lazima kwanza awe ana msingi wa kujua swali analolifanyia uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa siku za nyuma hasa kipindi chetu sisi, ni kwamba hata kama unakuwa na mtihani wa kuchagua ilikuwa bado unakuwa na sehemu ya kufanyia kazi ambayo na yenyewe inakuwa ni sehemu ya kuiangalia. Kwa hiyo, tutaona namna gani tuweze kufanya hivyo ili yule anayekuwa amechagua tuweze pia kupata uthibitisho isiwe tu kwamba swali la mwisho ndio jibu la kuliangalia, lakini ni suala ambalo linafanyiwa kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa James Mbatia swali la mwisho kwa eneo hili.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, lengo la nne la maendeleo endelevu ya dunia ni elimu bora, sawa, shirikishi kwa wote. Suala la mitihani na udanganyifu ni mchakato mdogo *to end product.* Sasa Serikali ina weka lini au itaanzisha lini chombo cha kudumu cha kuangalia mchakato mzima wa elimu yaani ubora wa elimu, kuwekeza kwenye miundombinu ya elimu kwa walimu, ukaguzi, vyote yaani *quality assurance* itaanzishwa lini chombo hiki ili elimu yetu, mitihani iwe ni sehemu ndogo tu kama ilivyo nchi ya Finland ambapo asilimia kumi tu ndiyo ile mitihani lakini mchakato mwingine wote wa kumuandaa mtoto unakuwa umeandaliwa na umesiamamiwa na chombo chenye mamlaka na kinachojitegemea? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, wizara imeliona hilo. Ni kwamba kwa sasa hivi kwanza tunaiangalia upya Sheria yetu ya Elimu kwa sababu ni ya muda mrefu na kuna mambo mengi yamejitokeza na hiyo tungependa iendane na uhalisia. Vilevile tunataka kuangalia mfumo mzima wa namna ya ukaguzi. Kwa mfano mwanzo tulikuwa na ukaguzi katika sehemu za kanda na kwenye Halmashauri/kwenye Wilaya zetu lakini sasa hivi baada ya kuongeza shule nyingi, inaonesha kwamba sasa kanda peke yake si sehemu sahihi

badala yake tungeweza kuangalia mfumo mzima na tukauboresha zaidi. Hii ni kwa sababu sasa shule za Serikali kwa mfano za sekondari zimeshaongezeka sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunaona kwamba haitoshi tu kuangalia shule ina walimu wangapi, madarasa mangapi na vyoo vingapi, tunataka tuangalie mfumo mzima, na hivyo wizara sasa hivi inaandaa Mfumo wa Uthibiti na Tathmini kwa ujumla *(National Schools Assurance Framework)* ambayo itawezesha sasa hata kama unafanyika ukaguzi unakuwa tayari una mwongozo unaokwambia ni nini unatakiwa ufuatilie. Vilevile hata kushirikisha kamati za shule pamoja na walimu na wananchi wenyewe kwa ujumla katika kudhibiti ubora wa elimu Tanzania. *(Makofi)*

Na. 465

**Mkakati wa Kubadilisha Maji ya Bahari kwa Matumizi ya Kawaida**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Kumekuwa na upungufu mkubwa wa maji safi na salama kutokana na kuongezeka kwa idadi kubwa ya watu nchini na mpaka sasa nchi yetu bado inategemea maji kutoka vyanzo vichache kama mabwawa, mito, maji ya mvua na kadhalika.

Je, Serikali ina mkakati gani maalum wa kubadilisha matumizi ya maji ya bahari kwa ajili ya matumizi ya kawaida ili kupunguza au kuondoa kabisa tatizo la upatikanaji wa maji nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kwa sasa kulingana na takwimu zilizopo ina maji juu ya ardhi na chini ya ardhi yanayofaa kwa matumizi mbalimbali kiasi cha kilomita za ujazo elfu 96.27, ambapo kila mwananchi ana uwezo wa kupata maji wastani wa mita za ujazo 1,800 kila mwaka hadi mwaka 2035 iwapo hatua madhubuti zitachukuliwa za kusimamia rasilimali za maji. Kiwango hicho cha maji kwa kila mtu kwa mwaka ni kikubwa ukilinganisha na kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa kila mtu kinachokubalika kimataifa cha mita za ujazo 1,700 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kukabiliana na changamoto ya kupungua kwa rasilimali za maji ikiwa ni pamoja na uhamasishaji wa uvunaji maji ya mvua ili nchi yetu isifike kiwango kikubwa cha uhaba wa maji na kusababisha athari kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maji yaliyopo yanatosha, na gharama za uwekezaji katika maji ya bahari kwa matumizi ya kawaida ni kubwa Serikali itaendelea kutumia vyanzo vingine vilivyopo, na endapo itabainika vyanzo hivyo vimepungua maji Serikali itajielekeza kuwekeza katika maji ya bahari kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**SPIKA:** Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar swali la nyongeza.

**MHE. FAIDA MOHAMED. BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza maswali yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu hapa kwamba maji yanatosheleza kulingana na ujazo uliopo, lakini cha kushangaza ni kwamba maji hayo hasa vijijini hayapatikani kwa ukamilifu.

Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kuyasambaza hayo maji anayosema yapo, maana kuwepo tu ardhini na juu ya ardhi si sababu ya kuyasambaza maji

hayo ili yawafikie wananchi na kuwapunguzia matatizo hususani wanawake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maji ya baharini tunayaona, hasa mvua ikinyesha maji ya mvua yanaelekea baharini, mwisho wake ni baharini. Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga mabwawa yaliyo mengi katika nchi yetu kila eneo ili kuyahifadhi maji hayo kwa matumizi ya wananchi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawaili Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji Mheshimiwa *Engineer* Isack Kamwelwe.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza ni kwamba kweli kuna kiwango kikubwa cha maji hapa nchini, lakini yapo maeneo hapa nchini ambayo hayana maji. Hilo ni kweli kabisa kwamba yapo maeneo na ndiyo maana Serikali kuanzia bajeti ya mwaka 2006/2007 ilianzisha Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Malengo yake ni kuhakikisha kwamba tumeyachukua haya maji na kuyafikisha maeneo ambayo yana ukame. Programu hiyo imeenda mpaka Juni mwaka 2015, na sasa hivi tumeingia kwenye awamu ya pili.

Mheshimiwa Spika, lakini matokeo ya programu hiyo ni nini? Tayari tumesaini mikataba ya kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka Shinyanga na sasa hivi tumesaini mkataba mwingine tunatoa Shinyanga kupeleka Nzega, Tabora hadi Igunga. Hiyo ndiyo tunaendelea utekelezaji wa kuichukua sasa hiyo hazina ya maji iliyopo ili tuweze kuyasambaza kwa wananchi, na tunapoyapeleka tunapita kwenye vijiji mbalimbali vingi kuhakikisha wananchi wanapata maji.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kweli mvua zinanyesha ni nyingi katika nchi yetu na maji haya yanapotea yanakwenda baharini, tunafanyeje? Tayari tumeshatengeneza utaratibu, tumeagiza kila Halmashauri kila mwaka kwenye bajeti zao watenge fedha ili kuhakikisha wanavuna maji. Si hilo tu, ni kwamba kwenye maeneo

ambayo Halmashauri wanahitaji hayo maji kwa ajili ya wananchi kupata maji safi na salama, Wizara ya Maji na Umwagiliaji pia tunatoa fedha kwa ajili ya kujenga hayo mabwawa madogo na ya kati. Pia tunaendelea sasa kujenga mabwawa makubwa ya kimkakati ambayo yatazalisha umeme wakati huo huo tutapata maji kwa ajili ya umwagiliaji na tutapata maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Rhoda Kunchele na Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mkoa wa Katavi bado una changamoto ya kupata maji safi na salama, lakini kibaya zaidi katika Jimbo la Katavi ambalo ni Jimbo la Mheshimiwa Waziri, katika maeneo ya Songambele, Kamsisi na Ilunde hakuna maji kabisa. Sasa Mheshimiwa Waziri ni lini utapeleka maji kwa sababu wananchi hawa umewatelekeza kwa muda mrefu? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Hilo si swali, ni tuhuma. Hata hivyo Mheshimiwa Waziri kwa kuwa upo ni vizuri ukasema kidogo jinsi gani unawapenda wananchi wako.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, nijibu tu swali kwa ufupi kwa Mheshimiwa Rhoda Kunchela kwa sababu amechokoza jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, Kamsisi wana visima vitatu tayari na wanapata maji. Songambele wana visima vinne na tayari wanapata maji, Ilunde tayari wana visima vitano na tayari wanapata maji, ndiyo tunaongeza vingine, kwa hiyo tayari jimbo langu linatendewa haki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Safi sana, Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Wanaulanga kwanza naomba niishukuru Serikali kwa ukamilishaji wa Daraja la Mto Kilombero, haya ndiyo matunda ya Serikali ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo yanazunguka Mto Kilombero yana shida kubwa sana ya maji...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mlinga, Daraja la Kilombero lipi?

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, Daraja la Mto Kilombero la kwenda Ulanga, limelamilika.

**SPIKA:** Lile kubwa kabisa?

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, lile limekamilika, lile kubwa kubwa.

**SPIKA:** Limekamilika?

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, kabisa na tunapita pale. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, swali langu ni hili, maeneo ambayo yanazunguka huu Mto Kilombero yana shida kubwa sana ya maji kwa upande Wilaya ya Kilombero, kwa maana ya Ifakara Mjini, pamoja na Tarafa ya Lupilo. Je, sasa Wizara ina mpango gani wa kubadilisha matumizi ya Mto Kilombero ili uwe unatumika kwa matumizi ya binadamu, kwa maana ya maji ya kunywa na kupikia?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri nimetembelea Morogoro kwenye Majimbo yote na Halmashauri zote, nimefika mpaka Mto Kilombero. Kwanza baada ya kuvuka Kilombero, Lupilo pale tayari tulishaweka mfumo wa maji na wananchi wanapata maji safi na salama. Maeneo mengi tunaendelea kuhudumia kwa kutumia Bonde la Mto Kilombero, lakini mawazo yako pia pale itakapofika sasa inahitajika tutajenga

bwawa kulingana na uwekezaji uliopo na idadi ya watu waliopo. Tutajenga bwawa kubwa Mto Kilombero ili tuweze kuwahudumia wananchi. Lakini kwa sasa bado tunaendelea kutumia Bonde la Mto Kilombero, wananchi wote wanapata maji safi na salama.

Na. 466

**Mlundikano wa Viwanda vya Simenti Ukanda wa Pwani**

**MHE. ZAYNABU M. VULU (K.n.y. MHE. MARIAM N. KISANGI)** aliuliza:-

Kumekuwa na mlundikano wa viwanda vingi vya aina moja katika kanda moja, kwa mfano kumekuwa na viwanda vingi vya saruji *(cement)* katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi na Mtwara.

Je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na tatizo hilo ili kuondoa changamoto za madhara ya athari kwa binadamu wanaoishi maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa wapi kiwanda kijengwe kwa kiasi kikubwa hutegemea uwepo wa soko la bidhaa itakayozalishwa na/au upatikanaji wa malighafi na/au teknolojia.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Ukanda wa Pwani kuanzia Tanga mpaka Mtwara wanayo faida ya kuwa na malighafi nyingi na yenye ubora wa hali ya juu wa utengenezaji wa saruji. Lakini pia inapotokea malighafi hiyo inaagizwa kutoka nje ya nchi, viwanda vilivyoko Pwani

vinakuwa na faida katika unafuu wa gharama za usafirishaji. Vile vile kihistoria soko kubwa la saruji na hata bidhaa nyingine ni Ukanda wa Pwani na hasa Dar es Salaam, si kwa nia mbaya viwanda kulundikana katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuondoa changamoto za madhara ya shughuli za viwanda kuwa ndani ya makazi ya watu wanaoishi maeneo ya karibu kupitia Sera ya Mazingira, ambapo kwanza kabla ya kiwanda kujengwa katika eneo husika, Tathmini ya Athari za Mazingira *(Environmental Impact Assessment)* hufanywa. Zoezi hili hufanywa na Baraza la Taifa la Mazingira *(NEMC)* kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wizara inayosimamia.

Mheshimiwa Spika, pili, baada ya kiwanda kuanza kufanya kazi Ukaguzi wa Athari za Mazingira *(Environmental Auditing)* hufanyika kila baada ya mwaka mmoja. Tatu, Serikali huhamasisha matumizi ya teknolojia rafiki kwa mazingira. Kwa mfano matumizi ya *Electrostatic precipitator, west scraper* ili kuzuia vumbi kusambaa hewani na kwenye makazi ya watu. Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira inaendelea kutoa mafunzo na kusimamia Sheria ya Mazingira ili kuepusha madhara yatokanayo na shughuli za viwanda nchini.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa juhudi zake za kuhakikisha viwanda vinakuwa vingi nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika majibu yake ya swali la msingi amegusia upatikanaji wa faida kwa kuhusisha kwa kuwa na miundombinu rahisi kwa kufikisha malighafi kwenye viwanda.

Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba hadi sasa baadhi ya maeneo miundombinu ya barabara si rafiki kwa magari yanayobeba bidhaa, hali kadhalika miundombinu hiyo haileti tija kwa wafanyabiashara wa viwanda na wanaokwenda viwandani kununua na kupelekea walaji kwa maana ya wananchi kuwauzia?

Je nini mpango wa Serikali wa kuhakikisha miundombinu hiyo itaboreshwa na kuimarishwa ili kuwapa nafuu wale wanaozalisha na wanunuzi wa hizo bidhaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kujua, viwanda vinapoanza kunakuwa na utaratibu wa kuangalia hali ya mazingira rafiki kwa wananchi. Viwanda vile vinapoongezwa kwa maana ya wanavyopanua au kuongeza idadi ya miundombinu ya uzalishaji mali.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuangalia usalama wa raia wanaozunguka kiwanda, hali kadhalika na wale wanaofanya kazi katika viwanda vile? Tumeshuhudia wengi wakiathirika, naomba majibu ya maswali hayo.

**SPIKA:** Majibu ya maswali haya Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineer* Isack Kamwelwe.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI):** Mheshimiwa Spika, ninaamini kwamba Mheshimiwa Mbunge yupo Tanzania. Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika suala la miundombinu yeye mwenyewe ni shahidi, kila kona zinajengwa barabara za lami ili kuunganisha Mikoa na Wilaya kwa barabara imara zinazopitika mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upande wa umeme, maana mali ikishazalishwa inahitaji kusafirishwa kwenda kwa wananchi inatumia barabara, lakini pia kuna miundombinu imara na Wizara ya Nishati na Madini inaendelea kuweka

umeme wa msongo mkubwa ili viwanda visipate shida kwa ajili ya kupata *power,* pia pamoja na matumizi ya gesi. Kwa hiyo, suala la miundombinu, Mheshimiwa Mbunge linakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ni mwaka huu tu kupitia TAMISEMI tayari na ninyi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, tumeunda *Rural Road Agency* ili kuhakikisha sasa utekelezaji wa barabara zile ndogo *(feeder roads)* zinafika kila kona ili mali zinazozalishwa viwandani ziweze kwenda kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la usalama viwandani; kuna usalama kupitia kwenye mazingira, lakini kuna usalama wa watumishi wanaofanya kazi ndani ya viwanda. Suala hili linashughulikiwa vizuri sana na idara husika ya mazingira kuhakikisha kwamba matatizo yanayojitokeza ndani ya viwanda hayaathiri wananchi wanaoishi katika mazingira ya pembezoni mwa kiwanda kama tulivyojibu katika swali la msingi, lakini pia yapo masuala ya usalama yanayokuwa-*addressed* ndani ya watumishi kwenye viwanda.

**SPIKA:** Majibu ya nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi uliyonipa, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na Mheshimiwa Vulu kwa maswali yake mazuri sana ya mazingira hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ameuliza swali linalohusu miundombinu. *Actually,* kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyoeleza, kwamba tunafanya tathmini ya mazingira kabla kiwanda hakijaanza ili kuona kwamba kiwanda hicho mahali kinapowekwa kama hakitakuwa na madhara yoyote katika mazingira au kwa wananchi wanaoishi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, sasa pale inapojitokeza kiwanda kinataka kupanua miundombinu yake katika eneo husika,

tunafanya tena tathmini ya athari kwa mazingira ili kujiridhisha, je, upanuzi na miundombinu inayoongezwa haitakuwa na athari yoyote ile kwa mazingira? Kwa hiyo, Mheshimiwa Vulu wala asiwe na wasiwasi, kila kiwanda kinapopanua miundombinu huwa tunashiriki na kujiridhisha kwamba hakuna athari yoyote ile kwa mazingira.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Magereli nilikuona swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kigamboni, Kata ya Kimbiji, tuna Kiwada cha Saruji cha Nyati. Nimesikia majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba kuna *Environmental Impact Assessment* ambayo hufanyika lakini tuna changamoto kubwa sana ya vumbi linalotimka kutoka kiwandani katika kata ile. Bahati mbaya kabisa kile kiwanda kiko katikati ya makazi ya watu. Sasa hivi minazi yetu Kimbiji haizai, miembe haizai, michungwa haizai, mazao ya mahindi tukilima kuvuna tunashindwa kwenda kulima kwa sababu panakuwa na vumbi kali sana ndani ya mazao ambayo tunayalima.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba utusaidie kwenye hili, ni kweli *Environmental Impact Assessment* ilifanyika, na je ilitoa majibu sahihi? Mbona tunapata adha hii kubwa namna hii? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Nyati, nilipokea malalamiko ya kiwanda hiki na baada ya kuletwa, yalikuwa malalamiko mengi sana dhidi ya uchafuzi wa mazingira ya kiwanda hiki. Kwanza, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba *Environmental Impact Assessment* ilifanyika katika kiwanda hicho na kiwanda

kikajengwa, japokuwa katika utekelezaji wake zilijitokeza changamoto.

Mheshimiwa Spika, nilipokwenda kwenye ziara hiyo kulikuwa na changamoto ya hilo suala la vumbi, lakini suala la vumbi *NEMC* walikwenda kushughulika pamoja na kiwanda na kuhakikisha kwamba changamoto hiyo imetatuliwa. Kulikuwa na changamoto ya kulipa fidia wananchi waliokuwa wanaishi karibu sana na kiwanda, wananchi hao wote wamekwisha kulipwa fidia mpaka sasa hivi tunavyozungumza.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na tatizo la yale makaa ya mawe kwamba yalikuwa yako nje na yalikuwa mvua zikinyesha yanatiririka mpaka kwenye vyanzo vya maji na kuchafua vyanzo hivyo. Tatizo hilo lilishughulikiwa na sasa makaa hayo hayaendi tena kwenye vyanzo vya maji. Kama bado kuna tatizo hilo analolizungumza sasa hivi Mheshimiwa Mbunge, tutakwenda kujiridhisha kuona kama kiwanda hicho bado kina tatizo hilo na kuchukua hatua stahiki.

Na. 467

**Umeme wa Gridi ya Taifa – Mkoa wa Katavi**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza:-

Mkoa wa Katavi hauna umeme wa Gridi ya Taifa.

Je, ni lini Mkoa huo utapatiwa umeme wa Gridi ya Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Katavi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Mikoa ya Kusini Magharibi ikiwemo Katavi, Kigoma na Rukwa kuunganishwa na umeme wa Gridi ya Taifa. Serikali kupitia *TANESCO* imeanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa Gridi Msongo wa kilowati 400 yenye urefu wa kilometa 1,080 kutoka Mbeya – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma hadi Nyakanazi.

Mheshimiwa Spika, mtaalam mshauri amekamilisha kazi ya kudurusu taarifa ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuhuisha mradi kutoka kilovoti 220 hadi kilovoti 400. Utekelezaji wa ujenzi wa mradi huu utaanza mwezi Desemba, 2017 na kukamilika mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo Mkoa wa Katavi utaanza kupata umeme wa Gridi ya Taifa. Gharama za mradi ni dola za Marekani milioni 664.

**SPIKA:** Mheshimiwa Taska swali la nyongeza.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umeme wa gridi mpaka kufika Mkoa wa Katavi utachukua muda mrefu; na kwa kuwa umeme hautoshi Mkoani Katavi, lakini pia napenda kuishukuru Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Uholanzi kwa ujenzi wa jenereta mbili na jenereta hizo zimeanza kufanya kazi kutoka tarehe 27 Mei, 2017 , lakini jenereta hizo hazitoshi.

Mheshimiwa Spika, umeme unaotakiwa Mkoa wa Katavi ni megawati tano, jenereta zinazalisha megawati 2.2. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza jenereta nyingine mbili kwa Mkoa wa Katavi? Kwa sababu mahali pa kuzifunga jenereta hizo tayaripameshajengwa, maana eneo la hizo jenereta limejengwa sehemu za kufunga jenereta nne, lakini Serikali pamoja na Serikali ya Uholanzi imefunga jenereta mbili, eneo hilo lipo. *(Makofi)*

Meshimiwa Spika, je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza jenereta mbili?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa jenereta hizi zinatumia mafuta ya dizeli na ni gharama zaidi, je, Serikali haioni kwamba matumizi ya jenereta kwa Mkoa wa Katavi ni gharama zaidi kuliko kufunga umeme wa gridi? Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, maswali yake ni mazuri na kwa faida ya Mkoa wa Katavi ambao na mimi mwenyewe natoka kule siwezi kuahidi lakini niseme kwamba nitalifikisha hili ili waweze kuongeza jenereta nyingine mpya kuongeza umeme. Lakini pia haya masuala ni ya kiuchumi. Ipo historia kwamba matumizi ya umeme katika mkoa wetu, hasa katika masuala ya viwanda bado hatujawa na viwanda vingi, kwa hiyo umeme sehemu kubwa unatumika majumbani tu na taarifa iliyopo ni kwamba *TANESCO* imekuwa inatoa gharama kubwa zaidi kuliko makusanyo yanayofanywa kutokana na matumizi ya umeme, lakini suala hili tutalifikisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili linalozungumzia dizeli. Ni kweli kabisa kwamba kutumia dizeli ni gharama kubwa kabisa na ndiyo maana sasa hivi Serikali nzima inataka kwenda kwa kutumia umeme ama wa gesi au wa maji, na ndiyo maana sasa Serikali imeshalitambua hili, inaleta umeme wa msongo mkubwa ambao sehemu kubwa utatumia uzalishaji kwa kutumia maji badala ya kutumia dizeli. Kwa hiyo, mawazo yako Mheshimiwa Mbunge ni mazuri na tayari Serikali imeshaanza kuyatekeleza.

**SPIKA:** Mheshimiwa John Mnyika nilikuona.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, tatizo la umeme wa Gridi ya Taifa kutokufika kwa wananchi haliko tu Mkoa wa Katavi, bali

pia liko katika Jimbo la Kibamba, Jijini Dar es Salaam ambapo kwenye Kata ya Mbezi maeneo kama ya Msumi kwa Londa hayana kabisa miundombinu ya umeme. Kata ya Goba kuna mitaa ambayo haina umeme, Kata ya Msigani kuna mitaa ambayo haina umeme, Kata ya Kwembe kuna mitaa haina umeme, Kata ya Saranga kuna mitaa haina umeme na Kata ya Kibamba kuna mitaa haina umeme.

Sasa kwa kuwa *TANESCO* iko jirani kabisa na Jimbo la Kibamba, je, Serikali iko tayari baada ya Mkutano huu wa Bunge kufanya ziara maalum kwenye kata hizi zote sita kwenda kuwaeleza wananchi ni lini hasa maeneo haya yatapata umeme?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, niseme kwanza Serikali iko tayari ndiyo maana imeanzisha *REA III,* na tayari maeneo mengi miradi imezinduliwa kuhakikisha kwamba vijiji vyote tulivyonavyo katika Tanzania vinapata umeme. Kwa hiyo, tayari imeshaanza, lakini niseme Mheshimiwa Mbunge mimi na wewe ni Madiwani tuna uwakilishi ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, ni kazi yetu sasa kwamba wewe kwasababu ni Mbunge uko ndani ya Bunge na matamshi haya ya Serikali umeyasikia, urudi kwenye Jimbo lako ukawaambie kuwa "jamani sasa Awamu ya Tatu ya *REA* inafika na kwetu tunapatiwa vijiji moja, mbili, tatu" na vijiji vyako vimeainishwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, kwa hiyo uende ukatoe taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa mtaona kwamba muda hauko upande wetu, naomba sasa tusikilizane.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusiana na wageni walioko katika jukaa la Spika. Ninao wageni 23 wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni washiriki na waandaaji

wa shindano la *Miss Tanzania* kutoka Mkoani Dodoma. Naomba msimame pale mlipokaa, ahsanteni sana na karibuni sana ma-*miss.* Rafiki zangu Wasukuma hawa ni ma-*miss* kutoka Dodoma, kama na ninyi mnao hebu tuone siku moja mlete ma-*miss* wa Mwanza, Shinyanga, Tabora. *(Makofi/ Kicheko)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 35 wa Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na Mheshimiwa Juma Nkamia ambao ni wachezaji wa timu ya *Area C United*-Dodoma na bingwa wa Mkoa wa Dodoma waliopanda ligi daraja la pili. *Area C United* naomba msimame hapo mlipo, karibuni sana na hongereni sana kwa kutubeba Mkoa wa Dodoma kuweza kuingia katika ligi daraja la pili. Naamini katika muda mfupi ujao mtakuwa katika ligi daraja la kwanza. Hongereni sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni tisa wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke ambao ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Wilaya ya Kasulu Mkoani Kigoma, Waheshimiwa Madiwani, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa James Mbatia ambao ni wazee wa kutoka Jimbo la Arumeru Mashariki, Kata ya Ngarenanyuki, Kitongoji cha Momela wakiongozwa na Mzee Senyael Nnko. Wazee kutoka Momela karibuni sana wazee wetu. *(Makofi)*

Wageni 30 wa Mheshimiwa Seif Gulamali ambao ni wanafunzi 28 na walimu wawili kutoka Shule ya Sekondari ya Ulaya iliyoko Ikungi, Wilaya ya Igunga, Mkoani Tabora, karibuni sana! Mmependeza kweli Wanyamwezi ninyi, karibuni sana! *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 81 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Sadiki Nuru, UDOM!! Karibuni sana

wanafunzi wa UDOM, tunawatakia kila la heri muongeze bidii katika mafunzo. *(Makofi)*

Wanafunzi 89 kutoka Chama cha Wanafunzi wanaosomea taaluma ya Manunuzi na Ugavi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 30 na walimu kutoka Chuo ca Ualimu *Capital* cha Mkoa wa Dodoma; karibuni sana wanafunzi wa ualimu kutoka *Capital. (Makofi)*

Lakini pia tuna wanafunzi 80 kutoka Chuo cha Kumbukumbu ya Hurbet Kairuki Jijini Dare es Salaam. *(Makofi)*

Karibuni sana wanafunzi wote ambao mmetutembelea siku ya leo, na baadaye maofisa wangu wa Bunge watawapatia maelezo mbalimbali kuhusu Bunge na namna ambavyo linafanya kazi na mnaweza mkawa pamoja nasi kufuatilia ni shughuli gani zinazoendelea. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa ibada *chapel* ya Bunge, Anna Lupembe anawataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba baada ya shughuli zetu saa 7:00 mchana anawaomba wanamaombi mkutane *basement* leo ambapo patakuwa na maombi ya kuliombea Taifa na kumuombea Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na yataongozwa na Mtumishi wa Mungu Mheshimiwa Dkt. Getrude Rwakatare; saa 7:00 baada ya shughuli zetu hapa, wanamaombi wote *basement. (Makofi)*

Katibu wa Bunge ameomba niwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba saa 7:00 tukimaliza hapa kutakuwa na semina ya *Red Cross,* kwa hiyo tutaombwa tubaki, wale ambao tutaona inafaa kufanya hivyo ili tuweze kusikiliza masuala yanayohusiana na *Red Cross.*

Naomba baada ya hapa tufanye shughuli moja inayofuata halafu kama kuna wanaotaka miongozo

nitawapa nafasi mbele kidogo tu lakini tufanye shughuli moja kwanza ili na mimi niweke meza yangu vizuri hapa mezani.

Katibu!

**NDG. CHARLES J. MLOKA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA ZA SERIKALI**

Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi wa Mwaka 2017 *[The Natural Wealth and Resources Contrats (Review and Re-Negotiations of Unconscieonable Terms)] Bill, 2017.*

Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa Mwaka 2017 *[The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Bill, 2017].*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 *[The Written Ammendment Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017].*

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Palikuwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao sijui ilikuwaje, lakini majina sikuwa nimeyapata hapa mezani kwenye orodha yangu, lakini nitambue uwepo wa wageni wa Mheshimiwa Taska Mbogo wakiongozwa na mume wake Ndugu John Kilowoko na watoto wake pale mlipo karibuni sana na watoto wa Mheshimiwa Taska wapo pale, karibuni sana. Mume wake Mheshimiwa Taska anafanya kazi kule *UNHCR* Ethiopia sasa sijui Rukwa na Ethiopia mnafanyaje kazi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Cecilia Paresso ana wageni wake wanafunzi 15 kutoka UDOM, wale pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Lema ana wageni wake pia sikuwanao kwenye orodha kama wapo popote walipo wageni wa Mheshimiwa Lema. Ahsante sana, karibuni sana, sikuambiwa ni akina nani, kwa hiyo, nimeshindwa kuwatambua vizuri zaidi.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Ni watoto wangu.

**SPIKA:** Ni watoto? Oooh, basi karibuni sana watoto wetu.

Waheshimiwa Wabunge, mtaona mmegawiwa karatasi ya ratiba na mtaona kwamba ratiba hii ni ratiba ambayo ina mabadiliko tofauti na ratiba mliyokuwanayo mwanzo. Kwa hiyo, nitaomba kila Mheshimiwa Mbunge aiangalie ratiba hii na naomba sana tusikilizane Waheshimiwa Wabunge mnaoongeaongea ili twende pamoja katika baadhi ya mambo haya, mtaongea baadaye tena.

Kamati ya Uongozi ilikaa jana na kupitia na kupendekeza kwamba tulete ratiba hii ambayo kila mmoja wenu nina uhakika ameshagawiwa, ambapo leo tunaendelea na Maazimio baada ya shughuli zetu. Kesho kutakuwa na maswali baada ya maswali tutatawanyika kwenda kwenye Kamati mbalimbali kama nitakavyoeleza na shughuli hiyo itaendelea hadi siku ya Jumatano ambapo kutakutakuwa na Hoja ya Kuahirisha Bunge tarehe 5 Julai.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo la kazi za Kamati ya Uongozi sasa nieleze maelezo ya Spika kama ifuatavyo na naomba mnisikilize.

## MAELEZO YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyosikia muda mfupi uliopita Makatibu wangu hapa wamesoma kwa mara ya kwanza kuna Miswada mitatu ya Sheria ya Serikali. Kwa mujibu wa Kanuni zetu, Miswada hiyo sasa nitaipeleka kwenye Kamati za Kudumu za Bunge ili ikafanyiwe kazi kama ipasavyo kwa utaratibu ufuatao:-

Kwanza, ule Muswada mmojawapo ambao unasomeka kama Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa mwaka 2017 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments, Bill 2017)* utafanyiwa kazi na Kamati ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa. Huo ni ule Muswada mmoja.

Pili, kwa mujibu wa Kanuni ya 7(3) ya Nyongeza ya Nane, nimeunda Kamati ya Pamoja ambayo itafanya kazi ya kuchambua Miswada miwili ya sheria ifuatayo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi wa Mwaka 2017 *(The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiations of Unconscionable Terms) Bill, 2017.*

(ii) Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa Mwaka 2017 *(The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty), Bill 2017.*

Waheshimiwa Wabunge, Kamati hii ya pamoja ambayo nimeiunda itaongozwa na Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko na itajumuisha Kamati nne ambazo ni Kamati ya Nishati na Madini; Kamati ya Katiba na Sheria; Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na Kamati ya Sheria Ndogo.

Narudia tena, Kamati ya Nishati na Madini; Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira; Kamati ya Sheria Ndogo na Kamati ya Katiba na Sheria. Hawa kwa pamoja watapitia ile Miswada miwili na Mwenyekiti wao atakuwa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Pamoja itafanya kazi kuanzia leo Alhamisi tarehe 29 Juni, 2017 baada ya shughuli zetu kwisha saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa mpaka siku ya Jumatatu tarehe 3 Julai, 2017. Hadidu za Rejea itakuwa ni kuchambua Miswada hiyo miwili na kuandaa taarifa ambayo itawasilishwa hapa Bungeni siku ya Jumanne tarehe 4 Julai, 2017. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kufuatia Miswada hiyo, ratiba ya Bunge kama nilivyosema imebadilika kwa kuongeza siku tatu za kazi kutoka tarehe 30 Juni, 2017 hadi tarehe 5 Julai, 2017 ambapo tutaahirisha Mkutano huu wa Saba wa Bunge. Ratiba mpya inayoonesha mabadiliko hayo tayari imeshasambazwa na iko mikononi mwenu.

Waheshimiwa Wabunge, aidha, napenda kutoa taarifa kwenu Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla kwamba, Miswada hii mipya mitatu tutakayoifanyia kazi imeshawekwa kwenye tovuti ya Bunge ambayo ni *www.parliament.go.tz.* Kwa maana hiyo, baada ya Miswada hii kwenda kwenye Kamati kama nilivyosema *immediately* baada ya saa 7.00 Kamati zitaanza kukutana, zinazohusika na Miswada hii; wao ndiyo watapanga utaratibu wa kuwaalika wadau na ratiba yao ya kukutana na wadau itakuwaje na jambo hilo litafanyika kama taratibu zetu zilivyo na shughuli zitaendelea kwa utaratibu huo.

Waheshimiwa Wabunge, haya maelezo niliyokuwa nayatoa ni maelezo yanayotokana na maamuzi ya Kamati ya Uongozi iliyokutana jana saa 1.00 jioni katika Ukumbi wa Spika. Sasa kwa hatua hii kama kuna watu walitaka miongozo na nini, haya, Katibu nipatie majina.

Mheshimiwa Flatei Massay ana wageni wake watano popote pale walipo pia wasimame!! Karibuni sana Wageni, karibuni sana. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**SPIKA:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi, naomba mwongozo wako kuhusu jambo ambalo limejitokeza mapema hapa Bungeni wakati wa maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kuna swali ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Ritta Kabati juu ya zao la mahindi na Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema kwamba katazo hilo lipo na maana yake Wakulima wetu wa mahindi hawatauza zao hilo nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba nipate mwongozo wako; kama ndio msimamo wa Serikali ni kwanini sasa Serikali isituambie wazi kupitia Waziri wa Kilimo au Mheshimiwa Waziri Mkuu au kauli ya Serikali kwamba wamejipanga kwa kiasi gani kwa *NFRA* kununua mahindi hayo ya wakulima. Kwa sababu wananchi wetu wanategemea zao la mahindi kama zao la biashara na zao la chakula pia na wengine pia wana *excess.* Naomba nipate mwongozo wako kwa nini Serikali isitufafanulie kwa kina badala ya kusema tu wametoa katazo, watuambie wamejipanga kwa kiasi gani ili wananchi wetu ambao wanategemea zao hilo la mahindi wasipate hasara.

**SPIKA:** Nachukulia kama ni ushauri kwa Serikali kwamba unaiomba Serikali ingejipanga ije itoe kwa wakati wake unaofaa ufafanuzi wa kina zaidi kuhusu suala la ununuzi wa mahindi kutoka kwa wakulima wetu. Ni jambo jema, linapokelewa na ninaamini Serikali imelisikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, mwongozo wangu ulikuwa unafanana na Mheshimiwa Pauline Gekul, kwa hiyo naomba ni-w*ithdraw.*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba muongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) jambo ambalo limetokea mapema.

Hivi karibuni kuna mchezaji wa Tottenham anaitwa Victor Wanyama aliingia Nchini kwetu na kwa bahati nzuri sana akawa amepokelewa na Meya wa Ubungo Ndugu Boniface Jacob, wakati huo huo huyu mchezaji akawa ameahidi kutengeneza ile barabara ya mtaa, akawa amepewa jina la mtaa lakini akasema kwamba atatengeneza barabara ya mtaa vizuri kwa kiwango cha lami, atainua soka la nchini kwetu. Kwa bahati mbaya sana Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ambaye tumekuwa tukimlalamikia akaagiza kwamba...

**SPIKA:** Samahani Mheshimiwa Haonga. Hilo jambo limetokea hapa Bungeni lini? *(Kicheko)*

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, limetokea mapema siku za hivi karibuni. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Tunaendelea Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kutoa mwongozo wangu.

**MBUNGE FULANI:** Kuomba!

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Kuomba Mwongozo wako. Ninaamini kabisa kwamba wajibu wa Serikali ni kuhamasisha wa Tanzania wengi na wananchi wengi wa Tanzania, kuhakikisha wanaingia kwenye mpango wa kilimo na kuhakikisha wanazalisha chakula kwa wingi. Lakini Serikali inawajibu wa kuhakikisha masoko yanapatikana ya chakula ambacho wanazalisha Watanzania hawa.

Mheshimiwa Spika, Watanzania hawa wanaofanya kilimo kama biashara ni wafanyabiashara kama wafanyabiashara wengine. Lakini wakulima hawa sasa hivi imetokea imekuwa ni tatizo na imekuwa ni kawaida ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kila wakati inapofika kipindi cha mavuno, Serikali inatoa makatazo wananchi wasitafute masoko...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka samahani, si ndio hili la Mheshimiwa Gekuli kwamba Serikali ije na maelezo mapana zaidi.?

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, inatofautiana kidogo, huyu ameomba mimi siombi najaribu kueleza hali halisi wakulima ni watu wa namna gani Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Kama huombi mwongozo basi kaa chini, ahsante sana. Mheshimiwa Heche. *(Kicheko)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, mwongozo wangu kwa sababu nipo kwenye *boarder* ya Sirari, nilikuwa nataka kuongea suala la mahindi hilo hilo, sasa na *withdraw.*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, muda mfupi uliopita tumekabidhiwa hii ratiba ya Bunge na maelezo ambayo umeyatoa ya kwamba Mosi Serikali inaleta miswada mitatu kwa hati ya dharura. Lakini pili, katika hiyo Miswada mitatu kuna siku moja ambayo Miswada miwili yote inajadiliwa kwa siku moja.

Mheshimiwa Spika, Bunge hili lina historia, mwaka 1997 ilileta miswada ya madini na miswada ya kodi ikapitishwa haraka haraka hatimaye nchi imeingia kwenye matatizo makubwa ya madini ikiwemo hayo ya makinikia na madini kwa ujumla. Mwaka 2005, Bunge hili tena lilitewa miswada mitatu kwa siku moja kwa Hati ya Dharura, miswada iliyohusiana na masuala ya gesi, mapato na tasnia ya uziduaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi ya Bunge kwa Ibara ya 63 ni kuishauri na kuisimamia Serikali, na Bunge ndio lenye mamlaka ya kutunga sheria na sisi Wabunge tulioko humu ndani, sisi ni wawakilishi wa wananchi. Kwa sababu sisi Wabunge ni wawakilishi wa wananchi, na hii Miswada mitatu inayoletwa, Miswada kuhusu Mapitio ya Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi, Muswada wa Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili na Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali. Miswada hii kwa umuhimu wake na kwa maslahi yake kwa nchi ni vizuri sisi wananchi tukapata wasaa wa kukutana na tunaowawakilisha ili tukapata maoni na mapendekezo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vema hii miswada ikasomwa leo kwa mara ya kwanza tu, Hati ya Dharura ikaondolewa, tukapata muda wa kurejea kwenda kukutana na wananchi wetu ili Miswada hii ikaletwa kwenye Bunge lijalo, Mkutano ujao wa Bunge tukaijadili na kuipitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiondoa wananchi, Bunge hili vilevile linawategemea wadau. Kwa maelezo uliyoyatoa ni kwamba wadau hawa sasa wanatakiwa kuitwa Dodoma kwa *short notice* wafike Dodoma kuja kutoa maoni kwa Kamati hapo Msekwa, kitu ambacho kitafanya wadau wengi kukosa muda, sio tu wakuchambua haya maoni, bali kukosa muda wa kuja kutoa maoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge vilevile, ni binadamu, Miswada mitatu inaletwa, tunatakiwa kwa muda mfupi tuichambue kifungu kwa kifungu, kipengele kwa kipengele tuweze kufanya marekebisho. Huu ni mtego, ni mtego wa kutufanya tushindwe kutekeleza haki yetu ya Kibunge ya kuishauri ya kuisimamia Serikali na haki yetu ya kibunge ya kutunga sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwahiyo, naomba mwongozo wako kwamba, mapendekezo hayo ya kamati ya uongozi, kwa sababu Kamati ya Uongozi si Bunge ni sehemu tu ya Bunge, sisi ndio Bunge. Mapendekezo haya ya Kamati ya Uongozi yaweze kujadiliwa na Bunge hili, mapendekezo haya yaweze kutenguliwa, badala yake ratiba iondolewe hivi ilivyo, tupewe ratiba ambayo Muswada utasomwa kwa siku moja, tutakwenda kujadiliana. Naomba kutoa hoja kwamba jambo hili lijadiliwe kama sehemu ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 51. Naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi nimekuona!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, kila jambo katika Bunge letu tukufu, linaongozwa na kanuni ambazo tunazo. Masharti ya kutunga sheria na masharti ya

jumla yanayoongoza mjadala unaohusu utungaji wa sheria ndani ya Bunge letu Tukufu, yamewekwa katika Sehemu ya Nane ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Na masharti hayo, yanaongozwa na Kanuni ya 80 na vifungu vyake vidogo na ukiendelea na Kanuni nyingine zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Miswada ambayo tumeleta mbele ya Bunge lako Tukufu, imekuja kwa Hati ya Dharura. Na ili Bunge lako Tukufu lijiridhishe kama Miswada hii inastahili kujadiliwa na Bunge ama haistahili kujadiliwa na Bunge, kanuni ambazo zinatuongoza ni hizi zifuatazo na ninaomba kwanza nizisome. Kanuni ya 80(4) inasema; Muswada wowote wa Sheria wa Serikali wa dharura hautaingizwa kwenye shughuli za Bunge bila ya kuwa na hati iliyowekwa saini na Rais inayoeleza kuwa Muswada uliotajwa katika hati hiyo ni Muswada ambao unachukua sura hiyo kwamba unatakiwa uingie Bungeni Hati ya Dharura.

Mheshimiwa Spika, lakini Kanuni ya 80 (6) inaendelea kusema; iwapo kama Kamati ya Uongozi, itaona kuwa Muswada wa Sheria wa Serikali, iliowasilishwa kwa Hati ya Dharura, haustahili kuwasilishwa kwa dharura, Kamati hiyo itaishauri Serikali ipasavyo. Lakini bado Kanuni hizo zinaendelea kutupa maelezo; Muswada wowote ule ambao umeletwa ndani ya Bunge lako na umekabidhiwa kwako na mamlaka uliyonayo Mheshimiwa Spika, ili uweze kuonekana unastahili kuingia ndani ya Bunge ama haustahili kuingia ndani ya Bunge, utakwenda kutoa picha na muelekeo huo, baada ya kufika kwenye Kamati ya Bunge iliyopewa kazi ya kujadili Muswada huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, naomba niseme mambo machache yafuatayo:-

La kwanza, sisi kama Serikali tumeshatimiza masharti yote ya Miswada hii kuingizwa ndani ya Bunge lako Tukufu. Sababu za Miswada hii kuingizwa kwa Hati ya Dharura tumeshazikamilisha zote, Kamati ya Uongozi kwa mujibu wa kanuni ilikuwa pia na wawakilishi wanaowakilisha Kambi ya

Upinzani na tulijadiliana kwa pamoja umuhimu wa Miswada hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo ambalo litakaloendelea kutoka hapa, wanaoweza kulishauri Bunge lako baada ya kuona uzito wa kazi iliyoletwa na Serikali, ukubwa wa Miswada, yaliyomo kwenye Miswada ni Kamati husika zitakazopewa kazi ya kujadili Miswada hiyo. *(Makofi)*

La nne ambalo ni la mwisho nililolitaka kulisema hapa, haitakuwa ni busara na wala siamini kama ni utaratibu mzuri, sisi Wabunge kabla hatujaona maslahi mazito yaliyomo katika Miswada hiyo, tukajenga hoja ndani ya Bunge ya kukataa maslahi mapana ya Taifa letu bila kuangalia kile kilichomo ndani ya Miswada hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwahiyo, nilikuwa naomba sana, tunapoendelea na jambo hili, tujue kwamba hata Wabunge sisi tuliopo katika upande mwingine wa Bunge hili na sisi tunawawakilisha wananchi na sio wenzetu tu peke yao wanawakilisha wananchi. Niliomba niyaseme hayo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyoelezwa mwanzoni, kwa niaba yetu nilipokea Hati ya Mheshimiwa Rais, Hati ya dharula. Na kama ilivyo ada na wajibu, niwakumbushe Wabunge zamani kabla ya mwaka 2007 kwa wale waliokuwepo wachache, ilikuwa Hati ya Dharura zinasemwa tu pale na Spika kwamba kuna Hati ya Dharura, Kamati ya Uongozi inaridhia na kadhalika. *(Makofi)*

Lakini tulipofanya mabadiliko ya Kanuni mwaka 2007, moja ya kitu tulichokiweka ni kwamba Hati ya Dharura ya Mheshimiwa Rais itakuja hati yenyewe yenye sahihi yake ndani ya Kamati ya Uongozi. Kwa hiyo, baada ya kuipokea jana, Wajumbe wa Kamati ya Uongozi waliiona na pale ndani tukapewa na maelezo na sababu za kwa nini kuna haja ya kufanyia jambo hili kazi katika udharura huo. Na nikisema Kamati ya Uongozi ni uwakilishi wa pande zote. Tulijadiliana wote kwa pamoja, tukakubaliana kwamba tusonge mbele. *(Makofi)*

Pia kama ambavyo *Chief Whip* ameeleza, kwa hatua hii tuliyofikia kwa taratibu zilivyo kwamba jambo hili liende kwenye Kamati na nimesema Kamati mbili zitahusika. Kamati moja ni yale mambo ya kawaida *(Miscellaneous Amendment)* ambazo kwa taratibu zetu huwa inaenda kwenye Kamati ya Katiba na Sheria ambayo Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Mchengerwa.

Kwa vile hiyo ndiyo kawaida, tukasema hiyo itaendelea na huo Muswada mmoja ambao kwa vyovyote vile huwa ni *traditional* tunapeleka kwenye Kamati hiyo. Lakini hii miswada miwili mingine ambayo ni midogo sana nitakapoiangalia kwa maana vifungu vyake ni vichache vichache, lakini ni muhimu kwa Taifa letu. Tukasema kwamba hii tupeleke Kamati nyingi zaidi kitu ambacho sio *tradition* yetu, lakini kwa ajili tu ya kuongeza uwazi, kuongeza uelewa, tukasema tupeleke kwenye Kamati nyingi zaidi, Kamati nne kwa mpigo, ambazo zenyewe zitafanya kazi kule Msekwa Ukumbi wa Msekwa kuanzia leo mchana. Kulikuwa kuna shida ya taa lakini sasa hivi wanafunga taa, kutakuwa na mwanga wa kutosha. *(Makofi)*

Lakini pia Wabunge wengine wote kuanzia leo mchana kuelekea huko jioni, kesho baada ya maswali, Jumamosi, Jumapili na kadhalika wote mnakaribishwa kwenye kazi za Kamati hizo kushiriki kikamilifu. Kule ndiko ambako tutajifunza na kuona kila kitu kwa nini kina umuhimu gani na kwa sababu gani na kadhalika hatua kwa hatua ya kila jambo. *(Makofi)*

Wakati Mheshimiwa Rais anapokea taarifa ya Kamati ya pili ya masuala yanayohusu madini kule Ikulu, Dar es Salaam, nilikuwa mmoja wa waliokuwepo pale na nilipewa nafasi ya kuzungumza na kwa niaba yenu nilitoa ahadi pale, kwamba sisi Bunge hili kama kuna mambo mazito yenye maslahi kwa nchi tutakuwa tayari kuyafanyia kazi kwa uharaka wa kipekee. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naziomba Kamati hizo zikaangalie, kwa kawaida Spika hatawe za kupanga shughuli hapa isipokuwa

Mwenyekiti wa Kamati amenitaarifu kwamba jambo hili limekamilika, ndio utaratibu wetu wa Kikanuni. Kwa hiyo, hatuwezi tena sisi Bunge tukawa Kamati maalum tena kujadili, inatakiwa sasa mambo haya yaende kwenye Kamati husika, Kamati zitajadili zitapitia kila kitu, halafu wao watanishauri mimi Spika, na mimi nitawaambia Kamati ya Uongozi. Sasa kama linaingia Bungeni au haliingii itatokea kwenye Kamati sio hapa, ndio utaratibu wetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa hatua hii, tukubaliane tu kwamba linaenda huko na nyie mnakaribishwa kwenye kamati hizo mbili kwenda kushiriki kujadili. Lakini kwa ujumla wake ni fursa ambayo sio ya kuipoteza kirahisi. Nilisema neno moja tu jana kwenye Kamati ya Uongozi labda ningerudia na hapa, sisi Wabunge tumekuwa kwa muda mrefu tukipigania Bunge hili liwe na nafasi fulani katika mchakato wa mikataba mikubwa inayohusiana na masuala ya madini na gesi. Liwe na nafasi fulani ili Taifa lisije likatumbukia tena katika mikataba mikubwa ambayo inaweza ikatia hasara Taifa. *(Makofi)*

Moja ya mambo ambayo tunaenda kuyapata katika mikataba hii, ni kuliweka Bunge mahali ambapo litakuwa na mkono fulani. Fursa kama hizo ni nadra, tumepigania kwa miaka mingi hatujawahi kupata fursa kama hiyo na mambo haya huwenda na upepo, tunaweza tukasitasita leo baada ya mwezi mmoja mawazo yamebadilika jambo hili tusipate tena.

Kwa hiyo, ndio maana nasema ipo haja ya kwenda kule na kuona maudhui na nini kilichopo, na hakika wengi hata hamjasoma, labda hata hamjaiona Miswada kwa sababu ili muipate lazima isomwe mara ya kwanza. *(Makofi)*

Sasa baada ya kusomwa mara ya kwanza nina hakika kwenye *pegionhole* huko mtakapoanza kupitia mtapata nakala zake, na baada ya kusoma mara ya kwanza ndio imekuwa sasa *public,* kwa hiyo hata wadau sasa wanaweza waka *acess* kupitia *internet* Miswada hii kama tulivyokwisha sema. Kwahiyo Mtanzania yoyote mwenye internet hivi sasa, ataipata miswada hii kupitia mitandao na ninyi Wabunge

mtaipata mara moja na kwa hiyo tunaweza tukaendelea nakushauriana kadri tunavyoenda.

Baada ya maelezo haya naomba itoshe kusema kwamba, tukubali kwa hatua hii tuende hivyo, halafu tutaona kadri tunavyoenda tutazidi kushauriana vizuri. Baada ya maelezo haya sasa naomba nimkabidhi Mheshimiwa Mwenyekiti wa Bunge Mheshimiwa Zungu.

**MBUNGE FULANI:** Jambo la dharura.

*Hapa Mwenyekiti (Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu!

**NDG.CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAAZIMIO**

**Azimio la Bunge kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Nairobi wa Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi *(Amended Convention for the Protection, Management and Development of Marine and Coastal Environment of the Western Indian Ocean)***

**Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari Hindi kutokana na vyanzo na shughuli zinazofanyika Nchi Kavu *(Protocol for the Protection of the Marine and Coastal Environment of the Western Indian Ocean from Land-Based Sources and Activities)***

**Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Nagoya ya Kusimamia Upatikanaji na Mgawanyo Sahihi wa Faida zitokanazo na Matumizi ya Rasilimali za ki-genetic (Nagoya *Protocol on Access to Genetic Resources and the Fair and Equitable***

***Sharing of Benefits Arising from their Utilization to the Convention on Biological Diversity)***

**MWENYEKITI:** Ahsante mtoa hoja upande wa Serikali.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi mwanachama wa Mkataba wa Kuhifadhi Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Afrika Mashariki uliopitishwa tarehe 21 Juni, 1985 ukihusisha nchi tisa ambazo ni Comoro, Kenya, Somalia, Madagascar, Mauritians, Msumbiji, Ushelisheli, Reunion pamoja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania iliridhia mkataba huu tarehe 1 Machi, 1996 ikiwa ni nchi ya sita kuridhia. Mkataba huu ulikuwa na lengo la kuhidhi mazingira ya bahari na Ukanda wa Pwani kwa nchi wanachama tisa kwa kushirikiana katika kuandaa mikakati na mipango ya pamoja katika kuhifadhi, kusimamia na kuendeleza mazingira katika Ukanda wa Pwani wa Mashariki ya Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mkataba huu kuanza kutekelezwa na nchi wanachama mwaka 1996 kulijitokeza changamoto kati ya nchi wanachama. Kati ya changamoto hizo ni pamoja na ufumbuzi wa mazingira ya bahari na Ukanda wa Pwani kutokana na shughuli za kibinadamu zinazofanyika katika nchi kavu.

Pili, ni utupwaji wa takataka zenye kemikali na sumu baharini na tatu ni athari za mabadilikio ya tabia nchi ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa kina cha bahari, kuongezeka kwa joto la bahari na kuongezeka kwa asidini baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hizo nchi wanachama kupitia Mkutano wa Pili uliofanyika *Port Louis Mauritius* mwaka 1999, ziliamia kufanya marekebisho kwenye baadhi ya vipengele vya mkataba wa Nairobi kwa lengo la kuwezesha na kuhifandi na kusimamia na kuendeleza mazingira ya Bahari na ukanda wa Pwani ya magharibi ya Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kufikia Azimio la kufanya marekebisho ya mkataba huu nchi wanachama wa Nairobi ziliazimia kupitia mkataba huu kwa kuviboresha baadhi ya vipengele na kuongeza vipengele vipya. Vipengele vilivyoboreshwa na kuongezwa vinahusu:-

(i) Kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi;

(ii) Kudhibiti utupwaji wa takataka zenye kemikali za sumu Baharini;

(iii) Ufuatiliaji na uzingatiaji wa utekelezaji wa mikataba;

(iv) Kuongezeka kwa nchi ya Afrika ya Kusini kama mwanachama mpya na kusababisha mabadiliko katika jina la mkataba na kuwa mkataba wa Nairobi kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya mkataba huu yalitiwa saini na nchi wanachama 10 badala ya tisa za awali hii ilitokana nan chi ya Afrika Kusini kujiunga katika mkataba tarehe 1 Aprili, 2010 huko Nairobi nchini Kenya. Nchi wanachama kwa muundo pia ni Comoro, Reunion, Kenya, Madagascar, Mauritius, Msumbiji, Ushelisheli, Somalia, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nchi ya Afrika Kusini, sekretarieti ya mkataba huu iko *UNEP* nchini Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maelezo ya hapo juu kuna umuhimu wa nchi yetu kuridhia marekebisho ya mkataba huu ili iendelee kunufaika na ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika kukabiliana na changamoto mpya za usimamizi na uhifadhi wa mazingira zinazokabili maeneo ya Bahari na ukanda wa Pwani wa Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba huu uliorekebishwa pia umezingatia mikataba mingine baadhi ya mikataba hiyo ni pamoja na mkataba wa mwaka 1982 kuhusu Sheria ya Bahari, Mkataba wa mwaka 1992 Mabadiliko

ya Tabianchi, Mkataba wa Basel Unaodhibiti Usafirishaji Baina ya Nchi na Utupwaji wa Takataka za Sumu, Mkataba wa Bamako unaopiga marufuku uingizaji na usafirishaji na utupaji wa takataka zenye sumu baharini na vilevile mkataba unaoendelea kuzitambua itifaki zilizokuwa zimeridhiwa katika mkataba wa awali ili pamoja na itifaki kuhusu maeneo yaliyoundwa yenye viumbe pori pamoja na mimea wa mwaka 1985 na itifaki kuhusu mashirikiano ya kuthibiti uchafuzi wa bahari unaotokana na matukio ya umwagiaji wa mafuta ama kemikali zenye madhara ya mwaka 1985.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba huu unavipengele 34 ambavyo vimefafanua maeneo mbalimbali ya mkataba ambayo nchi wanachama zinatakiwa kuyazingatia katika utekelezaji wake. Kimsingi maeneo hayo yamehusiana na mawanda ya mkataba, ufafanuzi, wajibu wa nchi wanachama na ufafanuzi unaotokana na uchafunzi utokanao na meli, utupaji taka hovyo, kazi zifanyikazo nchi kavu toka taka hatarishi kutoka nchi moja kwenda nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo hayo vipengele muhimu ambavyo vinafanyiwa marekebisho kwenye mkataba huu wa awali ni:-

(i) Utangulizi, nia ya nchi wanachama kuridhia marekebisho; nchi wanachama zinatakiwa utekelezaji wa mkataba kutekeleza mkataba kwa kutambua changamoto inayokabili mazingira ya Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi na marekebisho yaliyofanywa kwenye aya ya tatu ya utangulizi yametambua changamoto mpya zinazohusu masuala ya mabadiliko ya tabia ya nchi. Kwa kuwa baadhi ya changamoto zinazokabili maeneo ya ukanda wa Pwani wa Bahari zinasimamiwa na mikataba mingine ya kimataifa aya ya tisa ya utangulizi imetambua mikataba hiyo;

(ii) Ibara ya 7 ambayo ni uchafuzi wa kutoka vyanzo vya nchi kavu Ibara hii inahusu udhibiti uchafuzi wa bahari na ukanda wa Pwani utokanao na vyanzo vya nchi kavu. Marekebisho yaliyofanyika kwenye Ibara hii ni kuongeza

masuala ya shughuli nyingine ambazo zinasababishia uchafu wa bahari;

(iii) Ibara ya 16 muundo wa kitaasisi, Ibara hii inahusu muundo wa kitasisi ambao shirika la kimataifa la mazingira lilipewa jumkumu la kusimamia masuala ya kitasisi pekee. Ibara hii kwa sasa inasomeka kama Ibara ya 17 na imempa Mkurugenzi Mtendaji wa *UNEP* pia jukumu la kusimamia masuala ya kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipengele vipya vinavyoongezeka katika mkataba huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Ibara ya 9 ambayo inaelezea uchafuzi unaotokana na usafirishwaji na umwagaji wa taka zenye kemikali za sumu. Ibara hii inahusu kuzuia uchafuzi wa bahari na Ukanda wa Pwani utokanao na usafirishwaji na umwagaji wa taka zenye kemikali na sumu zinazotoka nchi nyingine;

(ii) Ibara ya 11 bionuai ibara hii inahusu kuhifadhi na kulinda bionuai viumbe na mimea adimu vilivyo hatarini kutoweka na kuanzisha maeneo tengefu kama vile hifadhi za wanyama pori, misitu sanjali na kuzuia shughuli zinazoweza kusababisha uharibifu wa viumbe hao pamoja na maeneo yao;

(iii) Ibara ya 27 uzingatiaji na utekelezaji wa sheria. Ibara hii inahusu nchi wanachama kuchukua hatua kulingana na uwezo wa nchi husika kutekeleza majukumu yaliyo aninishwa katika mkataba na kuzingatia Sheria husika za kimataifa. Aidha, nchi wanachama kuanzisha taratibu za kutathimini utekelezaji ili kuhamasisha uzingatiaji wa mkataba ikiwa ni pamoja na kuwa na utaratibu wa wazi wa kubadilishana taarifa baina ya nchi na nchi;

(iv) Marekebisho ya mkataba yatasaidia kuimarisha hali ya uchumi wa nchi, kipato cha jamii za Ukanda wa Pwani na afya ya wananchi kwa ujumla.

(v) Matokeo mengine mahususi ni pamoja na kuongezeka kwa bionuai za Bahari na Ukanda wa Pwani na kudhibiti wa uchafuzi unaotokana na shughuli zinazofanyika nchi kavu;

(vi) Kuongezeka kwa ubora wa maji kwenye Bahari kwa kudhibiti utupaji wa taka zenye kemikali za sumu Baharini;

(vii) Kuongezeka kwa kipato cha jamii ukanda wa Pwani kutokana na kuongezeka kwa mazao ya Bahari, kuongezeka kwa uwezo wa jamii ukanda wa Pwani katika kuhimili athari za mabadiliko ya tabia nchi na kupunguza shughuli zinazosababisha mabadiliko ya tabia nchi;

(viii) Kuimarika kwa ushirikiano wa kikanda kutokana na mipango pamoja na programu za miradi ya kikanda inayolenga hifadhi ya mazingira Bahari pamoja na ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mkataba huu ili uweze kutekelezwa ni lazima nchi wanachama ziridhie. Aidha, utaratibu wa kuridhia mkataba huu unaoneshwa katika Ibara ya 30 ya mkataba wenyewe. Ibara hii inaeleza kuwa kila nchi mwanachama inatakiwa kuridhia marekebisho ya mkataba na kuwasilisha ridhaa hiyo Serikali ya Jamhuri ya Kenya ambayo ni jukumu la kupokea na kuhifadhi ridhaa hizo. Tangu mkataba huu usainiwe mwezi Aprili, 2010 nchi wanachama zipo katika hatua mbalimbali za kuridhia kulingana na Sheria na taratibu za nchi husika na utaanza kutekelezwa rasmi baada ya miezi sita baada ya kuridhia. Hadi kufikia Juni, 2017 nchi ya Msumbiji, Mauritius, Ushelisheli ndizo zimeridhia marekebisho ya mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya sasa naomba kuwasilisha Azimio lenyewe kwa Bunge lako Tukufu ili liweze kuridhia kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa mkataba wa Nairobi kuhusu hifadhi, usimamizi na uendelezaji wa mazingira ya bahari na Pwani

ya kanda ya Afrika Mashariki ulipitishwa tarehe 21 Juni mwaka 1985 ukihusisha nchi tisa ambazo ni Comoro, Kenya, Somalia, Madagasca, Mauritius, Msumbiji, Ushelisheli, Reunion na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Na kwa kuwa Tanzania iliridhia mkataba huu tarehe 1 Machi, 1996.

Na kwa kuwa mkataba huu unalenga katika kudhibiti uchafuzi kutokana na vyanzo vya shughuli zinazofanyika nchi kavu na nchi wanachama kushirikiana katika kuanda mipango na mikakati pamoja katika kuhifadhi na kusimamia na kuendeleza mazingira Ukanda wa Pwani na Bahari.

Na kwa kuwa tangu mkataba huu ulidhiwe na nchi wanachama na kuanza kutekelezwa mwaka 1996 kumejitokeza changamoto za mazingira ikiwa ni pamoja na uchafuzi wa mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani toka vyanzo na shughuli zinazofanyika nchi kavu, uharibifu wa maeneo ya Pwani, utupwaji wa takataka zenye kemikali za sumu Baharini na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Na kwa kuwa katika Mkutano wa Pili wa nchi wanachama uliofanyika *Port Louis Mauritius* mwaka 1999 nchi hizo ziliadhimia kufanya marekebisho kwenye baadhi ya vipengele katika mkataba wa awali na kuongeza vipengele vipya.

Na kwa kuwa marekebisho yanahusu kuongezeka kwa wigo wa vyanzo vya uchafuzi wa mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani kutoka nchi kavu na vipengele vilivyoongezeka vinahusu kakabiliana na athari za mabadilikoya tabia nchi, kudhibiti utupwaji wa takataka zenye kemikali za sumu baharini, ufuatiliaji na uzingatiaji wa utekelezaji wa mkataba na kuongezeka kwa nchi ya Afrika Kusini kama mwanachama mpya na hivyo kusababisha mabadiliko ya jina la mkataba na kuwa Mkataba wa Nairobi kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi.

Na kwa kuwa marekebisho ya mkataba ya litiwa saini na nchi wanachama ikiwepo Tanzania tarehe 1 Aprili, 2010 mjini Nairobi.

Na kwa kuwa marekebisho haya yatawezesha nchi wanachama kuchukua hatua zaidi katika utekelezaji wa mkataba ikiwa ni pamoja na uandaaji wa mikataba ya kikanda na katika kukabiliana na changamoto hizo.

Na kwa kuwa ni muhimu nchi yetu iridhia marekebisho ya mkataba huu ili iendelee kunufaika na ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika kukabiliana na changamoto mpya za usimamizi na uhifadhi wa mazingira zinazokabili maeneo ya Bahari na ukanda wa Pwani.

Na kwa kuwa hatua hii, itasaidia kuboredha hifadhi na usimamizi na uendelezaji wa mazingira ya Pwani ya Bahari ya Hindi.

Na kwa kuwa Tanzania kwa kutia saini mkataba huu na hatimaye kutelekeza itanufaika na mambo yafuatayo:-

(a) Kuimarisha hali ya uchumi wa nchi, kipato cha jamii za ukanda wa Pwani na afya ya wananchi kwa ujumla.

(b) Kuwa na mpango wa pamoja na utekelezaji wa mkataba ulioandaliwa.

(c) Kuimarisha mikakati na miongozo inayohusika na kuboresha na kuhifadhi na kusimamia mazingira ya Bahari na ukanda wa Pwani.

(d) Kuongezeka kwa bionuai za Bahari na Ukanda wa Pwani kwa kudhibiti uchafuzi kutokana na shughuli zinazofanyika nchi kavu.

(e) Kuongezeka kwa ubora wa maji kwenye bahari kwa kuthibiti utupaji wa taka zenye kemikali za sumu Baharini.

(f) Kuongezeka kwa kipato cha jamii za ukanda wa Pwani kutokana na kuongezeka kwa mazao ya bahari.

(g) Kuongezeka kwa uwezo wa jamii za Ukanda wa Pwani katika kuhimili athari za mabadiliko ya tabia nchi na kupunguza shughuli zinazosababisha mabadiliko ya tabia nchi.

(h) Kuimarika kwa ushirikiano wa kikanda kutokana na kuwa mipango ya pamoja na programu za miradi ya kikanda inayolenga kuhifadhi mazingira ya bahari na ukanda wa Pwani.

Hivyo basi kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya mkataba huu kwa Tanzania Bunge hili katika Mkutano wake wa Saba na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977 liliazimia kuridhia marekebisho ya mkataba wa Nairobi wa hifadhi, usimamizi na uendelezaji wa mazingira ya bahari na Ukanda wa Pwani ya magharibi ya Bahari ya Hindi yaani *Amended Convention for the Protection Management and Development of the Marine and Coastal Environment of the Western Indian Ocean.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante hoja imeungwa mkono, sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria awasilishea taarifa yake. *Sorry* awasilishe yote. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki ya Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani wa Magharibi ya Hindi kutokana

na vyanzo na shughuli zinazofanyika nchi kavu ni itifaki iliyoanzishwa chini ya Mkataba wa Nairobi kuhusu hifadhi, usimamizi na uendelezaji wa mazingira ya Bahari ukanda wa Pwani Magharibi ya Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali mkataba ulijulikana kama Mkataba wa Kimataifa wa Hifadhi, usimamizi na uendelezaji wa mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Afrika Mashariki. Mkataba huu ulibadilishwa jina na kupewa jina la sasa kwa kufanyiwa marekebisho mwaka 2010. Tanzania ilisaini itifaki hii sambamba na marekebisho ya mkatba huu wa Nairobi tarehe 1 Aprili, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya itifaki hii, ni kudhibiti uchafuzi na uharibifu wa mazingira ya Bahari na ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi unaotokana na vyanzo na shughuli za kibinadamu zinazofanyika nchi kavu. Nchi zinazohusika na itifaki hii, ni zile zinazohusika na mkataba wa wa Nairobi yaani Comoro, Kenya, Somalia, Madagascar, Mauritius, Msumbiji, Ushelisheli, Reunion, Jamhuri ya Afrika Kusini na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za kuwa na itifaki hii zinatokana na marekebisho yaliyofanywa katika mkataba wa Nairobi yaliyosababishwa na changamoto za mazingira zilizojitokeza wakati utekelezaji wa mkataba wa Nairobi wa awali. Kujitokeza kwa changamoto hizo mpya ndiko kuliko sababisha nchi wanachama kuazimia mkataba huo urekebishwe na kuzijumuisha changamoto hizo, changamoto hizo ni pamoja na:-

(i) Uchafuzi wa mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani toka vyanzo vya shughuli zinazofanyika nchi kavu;

(ii) Uharibifu wa maeneo ya Pwani; na

(iii) Utupwaji wa taka zenye kemikali za sumu baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza ususani suala la uchafuzi wa mazingira Bahari na Ukanda wa Pwani toka vyanzo na shughuli zinazofanyika nchi kavu na kwa kuzingatia Ibara ya 4(2) ya kataba wa Nairobi ambayo inazipa mamlaka nchi wanachama kuanzisha itifaki mbalimbali ili kutekeleza mkataba. Nchi wanachama zilikubaliana kuanzishwa kwa itifaki iliyopendekezwa ili Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liweze kuridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa mkataba wa Nairobi Tanzania imeendelea kushirikiana na nchi wanachama wengine katika kubadilishana uzoefu wa kitaalum wa masuala mbalimbali yanayohusu eneo la Magharibi ya Pwani ya Bahari ya Hindi, kuandaa na kutekeleza mikakati, programu na miradi mbalimbali kuhusu hifadhi za Ukanda wa Pwani na Bahari. Aidha, mwaka 2008 Serikali ilipitisha mkakati wa hatua za haraka za kuhifadhi mazingiria ya Bahari Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa kwa lengo la kuhifadhi mazingira na bionuai zilizopo maeneo hayo na kuongeza ubora wa maji ili kuhakikisha panakuwepo na utumiaji endelevu wa rasilimali za bahari ili kuboresha hali ya maisha jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuimarisha vikundi vya kijamii katika kusimamia rasilimali za bahari ikiwemo kufanya doria za mara kwa mara, kuongeza uelewa wa jamii kuhusu hifadhi ya mazingira ya Pwani na Bahari, kuimarisha utafiti, kuinua utalii endelevu na kuimarisha uvuvi endelevu. Pamoja na mafanikio hayo kumekuwepo na uelewa mdogo wa kutozingatia masuala ya uchafuzi kutokana na vyanzo na shughuli mbalimbali zinazofanyika nchi kavu zinavyoweza kuathiri mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imepelekea kutodhibiti kikamilifu shughuli zinazofanyika Nchi kavu ambazo zinaathiri mazingira ya bahari kupitia mito inayoingiza maji baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipengele muhimu vya Itifaki hii ni pamoja na:-

(i) Ibara 4 ambayo ni wajibu wa nchi wanachama, Ibara hii ni pamoja na mambo mengine inabainisha wajibu wa nchi wanachama kuchukua hatua madhubuti za kupambana na uhalibifu wa mazingira kulingana na Sheria za Kimataifa, Mkataba na Itifaki yenyewe;

(ii) Ibara ya 5 ambayo ni vyanzo vya uchafuzi Ibara hii inahusu udhibiti wa umwagaji au utiririshaji taka kwenye maji na uchafuzi wa hewa katika maeneo ya bahari na Ukanda wa Pwani toka kwenye makazi, viwanda, vyombo vya usafiri wa maji. Aidha, Ibara hii inazitaka nchi wanachama kuweka viwango vya kudhibiti uchafuzi na kuvisimamia;

(iii) Ibara ya 6 ambayo inaongelea udhibiti wa uchafuzi kutokana na shughuli za kilimo. Ibara hii inazitaka nchi wanachama kuchukua hatua za kudhibiti uchafuzi unaotokana na shughuli za kilimo zisizoendelevu ambazo zinaweza kuathiri mazingira ya bahari na Ukanda wa Pwani;

(iv) Ibara ya 7 shughuli nyingine zinazoleta madhara Ibara hii inazielekeza nchi wanachama kudhibiti shughuli zinazoweza kuleta madhara kwa viumbe hai wa baharini na mazingira yao. Sambamba na kuchukua hatua zitakazosaidia jamii za Pwani kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi;

(v) Ibara ya 8 uchafuzi unaovuka mipaka, Ibara hii inazitaka nchi wanachama kudhibiti umwagaji wa taka kwenye mito, inayopita nchi zaidi ya moja ambayo kwa njia moja ama nyingine huathiri viumbe na maeneo ya Ukanda wa Pwani na Bahari. Aidha, Ibara hii imeelezea umuhimu wa kushirikiana na nchi zisizo wanachama katika kudhibiti uchafuzi wa aina hii;

(vi) Ibara ya 13 ambayo ni tathimini ya athari kwa mazingira na ukaguzi wa mazingira, Ibara hii inataka kila Nchi mwanachama kuwa na kanuni na miongozo ya ukaguzi

na tathimini ya athari kwa mazingira kwa ajili ya programu miradi na shughuli ambazo utekelezaji wake unaweza kuwa kwa namna moja ama nyingine kuathiri mazingira ya bahari na Ukanda wa Pwani;

(vii) Ibara ya 14 ushirikiano katika masuala ya kitaalam na kujenga uwezo, Ibara hii inataka kila nchi mwanachama inapaswa kushirikiana na nchi nyingine katika masuala ya sayansi na teknolojia zinazohusu udhibiti wa uchafuzi unaotokana na shughuli zinazofanyika katika nchi kavu na kushirikiana katika kutekeleza program za kujenga uwezo wa nchi wanachama;

(viii) Ibara ya 15 ambayo ni utoaji wa elimu kwa umma na ushirikishwaji wa jamii, Ibara hii inataka Nchi wanachama kuhamasisha upatikanaji wa taarifa na nyaraka muhimu zinazohusu uchafuzi toka nchi kavu. Aidha, nchi hizo zinasisitizwa kukuza uelewa kwa jamii na kuhakikisha jamii inashirikishwa katika kutoa maamuzi yanayohusu utekelezaji wa Itifaki;

(ix) Ibara ya 20 yenyewe inaongelea utaratibu wa fedha kwa mujibu wa makubaliano. Kila nchi mwanachama kulingana na uwezo wake itatenga fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa programu na miradi inayolenga kudhibiti uchafuzi katika maeneo ya Ukanda wa Pwani ya bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo kwa upande wa Tanzania kuridhia Itifaki inayopendekezwa itakuwa katika nafasi nzuri kwa kushirikiana na nchi wanachama kukabiliana na changamoto zilizojitokeza chini ya mkataba huo na haitaathiri shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na uchimbaji wa gesi na mafuta. Aidha, itaweza kutekeleza mikakati na mbinu bora za kuhifadhi mazingira ya bahari tukizingatia kuwa uchafuzi katika maeneo hayo hauna mipaka. Mpaka sasa nchi ya Msumbiji, Ushelisheli, Mauritius zimeridhia Itifaki hii na nyingine zipo katika hatua za kuridhia kulingana na taratibu za nchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida za kuridhia itifaki hii ni pamoja na kuhifadhi na kuongezeka bionuai ya kuboresha mazingira ya bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi, kutekeleza mipango ya kudhibiti uchafuzi unaotokana na shughuli zinazofanyika nchi kavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongezeka kwa ubora wa maji kwenye mito, bahari na udhibiti wa uchafuzi, kuongezeka kwa kipato cha jamii za Ukanda wa Pwani na kuongezeka kwa mazao ya bahari na Ukanda wa Pwani, kuimarika kwa afya za wananchi kwa kuwa na mazingira bora, kuimarika kwa ushirikiano baina ya Tanzania na nchi wanachama kutokana na kuongezeka kwa hatua za kulinda mazingira ya Pwani na Bahari, kupatikana kwa fursa za utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali yenye ushirikiano na nchi nyingine inayolenga kudhibiti uchafuzi wa mazingira katika bahari na Ukanda wa Pwani wa Magharibi ya Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, sasa naomba kuwasilisha azimio lenyewe kwa Bunge lako Tukufu, kuridhia itifaki ya udhibiti wa uchafuzi wa mazingira ya bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi kutokana na vyanzo na shughuli zinazofanyika katika nchi kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa itifaki ya kudhibiti uchafuzi wa mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi, kutokana na vyanzo vya shughuli zinazofanyika Nchi kavu ilipitishwa na kusainiwa na nchi husika tarehe 01 Aprili, 2010 Nairobi nchini Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waambie wanaoongea Waziri wa Mambo ya Ndani anaongea hapo.

**MWENYEKITI:** Haya soma Azimio la tatu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Na kwa kuwa madhumuni ya itifaki hii ni kudhibiti uchafuzi na uharibifu wa mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani wa Magharibi ya

Bahari ya Hindi, unaotokana na vyanzo vya shughuli za kibinadamu ziinazofanyika nchi kavu;

Na kwa kuwa nchi wanachama zinazohusika na Itifaki hii ni zile zinazopatikana Bahari ya Hindi ambazo zinajumuisha Comoro, Kenya, Somalia, Madagascar, Mauritius, Msumbiji, Ushelisheli, Reunion Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Afrika ya Kusini;

Na kwa kuwa itifaki hii imeanzishwa chini ya Mkataba wa Nairobi uliofanyiwa marekebisho na nchi wanachama mwaka 2010 Mkataba wa Nairobi wa kuifadhi usimamizi na uendelezaji wa mazingira ya bahari ya Ukanda wa Pwani wa Magharibi ya Bahari ya Hindi;

Na kwa kuwa utekelezaji wa Mkataba wa Nairobi unaohusu hifadhi, usimamizi na uendelezaji wa mazingira ya Bahari na Pwani ya Kanda ya Mashariki ambayo Tanzania ililidhia tarehe 01 Machi, 1996 inaonyesha kuwa zipo changamoto za kimazingira zilizojitokeza ambazo zilisababisha nchi wanachama kuazimia Mkataba huo urekebishwe;

Na kwa kuwa makubaliano ya kufanya mapitio ya Mkataba wa Nairobi yalifikiwa katika Mkutano wa Pili wa nchi wanachama uliofanyika *Port Louis,* Mauritius mwaka 1999.

Na kwa kuwa mapitio ya mkataba huo yalibainisha changamoto mbalimbali zikiwemo uchafuzi wa mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani kutoka vyanzo vya shughuli zinazofanyika nchi kavu, uharibifu wa maeneo ya Pwani, utupwaji wa takataka zenye kemikali za sumu baharini na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi;

Na kwa kuwa katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza hususani uchafuzi wa mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani toka vyanzo na shughuli zinazofanyika Nchi kavu, marekebisho yamefanywa kwa kuzingatia Ibara ya 4(2) ya Mkataba wa Nairobi ambayo zinaipa nchi mamlaka

wanachama kuanzisha itifaki mbalimbali ili kutekeleza mkataba huo, na nchi wanachama zilikubaliana kuanzishwa kwa itifaki inayopendekezwa kuridhiwa.

Na kwa kuwa Tanzania kuweka saini ya Itifaki hii, hatimaye kuitekeleza itanufaika na mambo yafuatayo:-

(a) Kuhifadhi na kuongezeka kwa bionuai ya kuboresha mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi.

(b) Kutekeleza mipango ya kudhibiti uchafuzi unaotokana na shughuli zinazofanyika nchi kavu.

(c) Kuongezeka kwa ubora wa maji kwenye mito na bahari kutokana na udhibiti wa uchafuzi.

(d) Kuongezeka kwa kipato cha jamii Ukanda wa Pwani kutokana na kuongezeka mazao ya Bahari na Ukanda wa Pwani.

(e) Kuimarika kwa afya za wananchi kwa kuwa mazingira ni bora.

(f) Kuimarika kwa ushirikiano baina ya Tanzania na nchi wanachama, kutokana na kuongezeka kwa hatua za kulinda mazingira ya Pwani na Bahari.

(g) Kuimarisha ushirikiano katika masuala ya kitaalam na kujenga uwezo katika masuala ya sayansi na teknolojia zinazohusu udhibiti wa ufafanuzi unaotokana na shughuli zinazofanyika nchi kavu, na kushirikiana katika kutekeleza programu za kujenga uwezo kwa nchi wanachama.

(h) Kutoa elimu kwa umma na ushirikishwaji wa jamii kwa kuhamasisha upatikanaji wa taarifa na nyaraka muhimu zinazohusu uchafuzi wa Bahari kutoka nchi kavu.

(i) Kupatikana kwa fursa za utekelezaji kwa programu na miradi kwa ushirikiano na nchi nyingine inayolenga

kudhibiti Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Mazingira ya Bahari ya Hindi.

Hivyo basi kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya Itifaki hii kwa Tanzania, Bunge hili katika Mkutano wake wa Saba na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 liliazimia kuridhia Itifaki ya Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi, kutokana na vyanzo vya shughuli zinazofanyika nchi kavu yaani *the Protocol for Protection of the Marine and Coastal Environment of Western Indian Ocean from land based sources and activities.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa imeungwa mkono, maazimio matatu yote yamesomwa sasa namuita Mwenyekiti Kamati ya Katiba na Sheria na yeye aje kutoa taarifa yake. Bado Azimio moja? Haya limalizie hilo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi mwanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa mwaka 1992 *(The United Nations Conventional Biological Diversity)* uliopitishwa na Umoja wa Mataifa Mjini Rio De Janeiro nchini Brazil wakati wa Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu mazingira na maendeleo wa mwaka 1992. Mkataba huu una malengo makuu matatu, ambayo ni:-

(i) Hifadhi ya bionuai *(Conventional of Bio Diversity)*;

(ii) Matumizi endelevu ya bionuai; na

(iii) Usimamizi wa upatikanaji wa mgawanyiko wa haki na sahihi wa faida zinazotokana na matumizi ya raslimali za kijenetiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania iliridhia Mkataba huu tarehe 8 Machi, 1996 chini ya Mkataba huu kuna Itifaki tatu ambazo ni:-

(i) Itifaki ya Katagena ya mwaka 2000 inayohusu usimamizi wa mazingira dhidi ya athari zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya ki-bio teknolojia ya kisasa. Tanzania iliridhia Itifaki hii tarehe 16 Machi, 2003.

(ii) Itifaki ya kusimamia upatikanaji wa mgawanyo sahihi wa faida zinazotokana na matumizi ya rasilimali za asili, za kijenetiki Itifaki za ziada ya Nagoya, Kuala Lumpur kuhusu uwajibikaji wa kisheria na fidia katika kutekeleza Itifaki ya Cartagena.

(iii) Itifaki ya Nagoya ilipitishwa na nchi wanachama wa Mkataba wa *CBD* katika kikao chake cha kumi mwaka 2010 nchini Nagoya, Japan. Makubaliano haya yalifikiwa baada ya nchi wanachama wa *CBD* kujadiliana tangu mwaka 2004 juu ya kuanzishwa kwa Itifaki hii yenye nguvu ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu la Itifaki hii ni kuhakikisha kwamba kunakuwepo na mfumo wa kisheria, kiutawala na kitaasisi utakaosimamia upatikanaji wa rasilimali za kijenetiki kwa matumizi mbalimbali na pia kuweka utaratibu wa mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali katika nchi zinazotoa rasilimali hizi na zile zinazotumia rasilimali hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mukhtadha huu Itifaki hii itahamasisha utunzaji, uhifadhi, na matumizi endelevu ya raslimali za kijenetiki. Aidha, sehemu ya faida itokanayo na rasilimali hizi itazifaidisha jamii ambazo rasilimali hizi zinapatikana na hivyo kutoa motisha kwa jamii hizi kuzilinda na kuhifadhi rasilimali hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki ya Nagoya imeanza kufanya kazi mwezi Oktoba, 2014 katika Kikao cha Kumi na Mbili cha Mkataba, kilichofanyika mjini Pyeongchang, Korea

Kusini. Kwa mujibu wa utaratibu wa Mkataba huo Itifaki hii ilianza kutumika baada ya nchi 50 kuridhia. Katika Kikao cha Kumi na Mbili cha Mkataba wa nchi 50 zilikuwa zimekwisha ridhia Itifaki hii na kuwezesha nchi wanachama kuendesha kikao cha kwanza tarehe 13 hadi 17 Oktoba, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Juni, 2017 nchi 92 zimesaini ambapo nchi 100 duniani zimeridhia Itifaki hiyo ya Nagoya. Katika Ukanda wa nchi za Afrika Mashariki nchi ya Rwanda mwaka 2014, Kenya mwaka 2014, Uganda mwaka 2014 na Burundi mwaka 2014 tayari zimeridhia Itifaki hiyo. Katika ukanda huu ni nchi ya Tanzania na Sudan Kusini ambazo bado hazijaridhia Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo kwa Bunge lako kukubali kuridhia Itifaki hii Tanzania itakuwa imepiga hatua katika kuimarisha usimamizi wa raslimali za kijenetiki kwa kushirikiana na nchi za Ukanda huu na hatimaye kuchangia katika uchumi wa nchi yetu na hifadhi ya utajiri ambayo nchi yetu ndiyo imejariwa kuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura Namba 191 ya mwaka 2014 inatambua umuhimu wa rasilimali hizi katika uchumi wa nchi yetu na kuhifadhi bionuai. Sheria hii imetoa mamlaka kwa Waziri mwenye dhamana ya Mazingira kuandaa kanuni zitakazosimamia mfumo na usimamizi wa kisheria katika masuala ya upatikanaji wa raslimali za kijenetiki pamoja na kutoa muongozo wa mgawanyo sahihi wa faida zitakazotokana na matumizi ya rasilimali hizi. Ili kuweka mfumo huu wa kisheria tayari rasimu ya kanuni za kisheria zitakazosimamia masuala haya zimekwisha kuandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi kwa Bunge kuridhia Itifaki hii, itakuwa linasaidia pia utekelezaji wa Sheria ya usimamizi wa Mazingira katika Masuala haya kwa vile sheria hii ilikwishaelekeza hivyo, hii ni kwa sababu maudhui ya Itifaki hii tayari yamekwisha, kuwekwa kwenye Sheria ya usimamizi wa mazingira Sura Namba 191 ya mwaka 2004 kifungu 230(2)(d).

Mheshimiwa Mwenyekiti, msukumo mkubwa wa kuridhia Itifaki hii unatokana na ukweli kwamba kwa muda mrefu raslimali za kijenetiki zimekuwa zikichukuliwa na kusafirishwa nje kwa matumizi mbalimbali kama vile utafiti, mafunzo, ama kutengenezea bidhaa za viwandani na madawa. Faida inayotokana na matumizi ya rasilimali hizi imekuwa hairudi kuzinufaisha nchi ambazo ndizo zenye umiliki wa rasilimali hizi. Kwa hiyo, nchi hizi zinaonekana kama vile shamba la bibi na rasilimali hizi kugeuzwa kuwa ni rasilimali zinazoweza kuchukuliwa wakati wowote bila ya utaratibu uliowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi wanachama na hasa nchi za Afrika ambazo ndizo zenye utajiri wa raslimali za kijenetiki ziliona kuna umuhimu wa kudhibiti hali hii, ili nchi zenyewe ziweze kunufaika na rasilimali za kijenetiki pamoja na elimu ya asili ya rasilimali katika nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira za kuridhia Itifaki hii ni kwamba, endapo matumizi ya rasilimali za kijenetiki na elimu asili zinazohusisha matumizi ya rasilimali pamoja na kuimarisha fursa za mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali hizo, zitaimarishwa, nchi wanachama zinatarajia kwamba Itifaki hii itakuwa kichocheo katika kuhifadhi bionuai matumizi ya endelevu ya bionuai na bidhaa zinazotokana na bionuai na pia Itifaki itaimarisha mchango katika maendeleo endelevu ya maisha ya wananchi na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida za kuridhia Itifaki hii kwa nchi yetu ni pamoja na kuwezesha nchi kuweka utaratibu wa kusimamia upatikanaji wa rasilimali za kijenetiki na mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali za kijenetiki. Ofisi inayoratibu shughuli za mkataba huu wa kuhifadhi mazingira itaimarisha utekelezaji wa Mkataba huu, pamoja na Itifaki ya Nagoya kikamilifu kwa kuweka mfumo sahihi wa kusimamia rasilimali za kijenetiki na matumizi ya watumiaji wa ndani na nje kwa kuzingatia taratibu zitakazokuwa zimewekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kwamba mfumo wa sasa hauna utaratibu mzuri wa kudhibiti wageni wanaofanya utafiti kutoka nje, rasilimali zetu zinachukuliwa na kusafirishwa bila kujua. Aidha, matokeo ya tafiti hizo mbalimbali pamoja na faida zake zimekuwa hazijulikani na wala nchi au jamii ambako jenetiki hizo zinatoka ama zimechukuliwa hazifaidiki na tafiti hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na faida itakayotokana na tafiti kwa kuridhia itifaki hii itatusaidia mambo muhimu yafuatayo:-

(i) Kuweka misingi ya Kisheria na uwazi kwa utoaji na watumiaji wa ndani na nje wa rasilimali za kijenetiki;

(ii) Baada ya kuweka utaratibu sahihi wa watumiaji na watafiti wote watapaswa kuzingatia sheria za nchi zonazohusiana na rasilimali;

(iii) Ada ya kuweka utaratibu sahihi wa kusimamia upatikanaji wa rasilimali za kijenetiki jamii zenye elimu asili zinazohusiana na rasilimali za kijenetiki zitafaidika na mgawanyo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku nikiomba itifaki hii yote iingie kwenye kumbukumbu sahihi naomba sasa baada ya maelezo haya kuwasilisha azimio lenyewe kwa Bunge lako kuridhia kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Tanzania ni nchi mwanachama wa Mkataba wa Mwaka 1992 unaohusu Hifadhi ya bionuai, matumizi endelevu ya bionuai pamoja na mgawanyo wa faida zinazotokana na matumizi ya bionuai ambao uliridhiwa tarehe 8 Machi, 1996;

Na kwa kuwa chini ya mkataba huu kuna itifaki ya Cartagena ya mwaka 2000 inayohusu usimamizi salama wa mazingira dhidi ya athari zinazoweza kutokea kutokana na matumizi ya baionuai teknolojia ya kisasa ambayo Tanzania iiridhia tarehe 16 Machi, 2003;

Na kwa kuwa katika Mkutano wa Sita wa Mkataba uliofanyika Johannesburg, Afrika ya Kusini mwaka 2002 uliobaini kwa lengo la tatu la mkataba huo linahusu mgawanyo sahihi wa faida zinazotokana na matumizi ya rasilimali za kijenetiki halijafanikiwa kutokana na kukosekana kwa mfumo wa kusimamia utekelezaji wa mkataba huo;

Na kwa kuwa ili kuweka mfumo wa usimamizi wa mkataba mchakato wa kuanzisha itifaki ya kusimamia upatikanji wa mgawanyo sahihi wa faida zinazotoka na matumizi ya rasilimali za kijenetiki ulianzishwa na itifaki ilipitishwa katika Mkutano wa Kumi wa nchi wanachama uliofanyika Nagoya, Japan mwaka 2010;

Na kwa kuwa Tanzania iliridhia mkataba wa baionuai mwaka 1996 ambao umeanzisha itifaki ya kusimamia upatikanaji wa mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali ya kijenetiki;

Na kwa kuwa Tanzania kwa kuridhia itifaki hatimaye kuitekeleza itanufaika na mambo yafuatayo:-

(a) Kuwa na misingi ya kisheria uwazi wa utoaji wa watumiaji wa rasilimali za kijenetiki.

(b) Sheria ya nchi zinazohusiana na rasilimali za kijenetiki zitazingatiwa.

(c) Jamii itanufaika na elimu na ujuzi wa siri wa rasilimali za kijenetiki.

(d) Udhibiti wa uhamishaji holela wa rasilimali za kijenetiki bila faida kwa nchi ama umma kwa ujumla.

(e) Kuongezeka kwa motisha ya hifadhi na matumizi endelevu kwa ajili ya ustawi wa jamii.

(f) Kupatikana kwa fursa za fedha kwa ajili ya kutekeleza malengo ya itifaki,

Na kwa kuwa Sheria ya usimamizi wa Mazingira Sura Na. 191 ya mwaka 2004 iliyopitishwa na Bunge hili imeelekezwa kutungwa kwa kanuni na sheria zitakazoweka mfumo wa kisheria, kiutawala na kitaasisi katika usimamizi wa masuala ya mazingira;

Hivyo basi kwa kuzingatia umuhimu wa manufaa ya itifaki hii kwa Tanzania, Bunge hili katika Mkutano wake wa Saba kwa mujibu wa bara ya 63(3)(e) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 liliazimia kuridhia itifaki ya kusimamia upatikanaji wa mgawanyo sahihi wa faida zinazotokana na matumizi ya rasilimali za ki-genetic yaani *Nagoya Protocol on Access to Genetic Resources and Fair and Equitable Sharing of Benefits Arising from their Utilization of the Convention and Biological Diversity.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imeungwa mkono.

**AZIMIO LA BUNGE KURIDHIA ITIFAKI YA NAGOYA YA KUSIMAMIA UPATIKANAJI NA MGAWANYO SAHIHI WA FAIDA ZITOKANAZO NA MATUMIZI RASILIMALI ASILI ZA KIJENETIKI NAGOYA PROTOCOL ON ACCESS TO GENETIC RESOURCES AND THE FAIR AND EQUITABLE SHARING OF BENEFITS ARISING FROM THEIR UTILIZATION TO THE CONVENTION ON BIOLOGICAL DIVERSITY - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania ni nchi mwanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa Bioanuai wa mwaka 1992 (The United Nations Convention on Biological Diversity) ambao una malengo makuu (3) ambayo ni,Hifadhi ya bioanuai ( Conservation of Biodiversity); Matumizi endelevu ya bioanuai (Sustainable Utilization of Biological resources); na Usimamizi katika upatikanaji na mgawanyo wa haki na usawa wa

faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali asilia za kijenetiki ( fair and equitable sharing of benefits arizing from utilization of genetic resources).

***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania iliridhia Mkataba huu tarehe 8 Machi 1996. Chini ya Mkataba huu kuna Itifaki tatu ambazo ni: **Itifaki ya Cartagena ya mwaka 2000** inayohusu Usimamizi wa Mazingira Dhidi ya Athari zinaweza kutokea kutokana na Matumizi ya Biotekinolojia ya kisasa. Tanzania iliridhia Itifaki hii tarehe 16 Machi 2003; **Itifaki ya kusimamia upatikanaji na mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali asili za kiejenetiki;** na **Itifaki ya ziada ya Nagoya – Kuala Lumpur** kuhusu uwajibikaji kisheria na fidia katika kutekeleza Itifaki ya Cartagena.

***Mheshimiwa Spika,*** Itifaki ya Nagoya ilipitishwa (adopted) na nchi wanachama wa Mkataba wa CBD katika kikao chake cha kumi (10) mwaka 2010 nchini Nagoya, Japan. Makubaliano haya yalifikiwa baada ya nchi wanachama wa CBD kujadiliana tangu mwaka 2004 juu ya kuanzishwa kwa Itifaki hii yenye nguvu ya kisheria *(International Leagally binding instrument on Access and Benefit Shairing)*.

***Mheshimiwa Spika*,** Lengo kuu la Itifaki hii ni kuhakikisha kwamba panakuwepo na mfumo wa kisheria na kitaasisi utakaosimamia upatikanaji wa rasilimali za kijenetiki kwa matumizi mbalimbali na pia kuweka utaratibu wa mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali hizi kati ya nchi zinazotoa rasilimali hizi zinazotumia rasilimali hizi za kiejenetiki. Kwa muktadha huu, Itifaki hii itahamasisha utunzaji wa rasilimali hizi pamoja na matumizi endelevu ya rasilimali za kiejenetiki.

***Mheshimiwa Spika,*** Itifaki ya Nagoya imeanza kufanya kazi (entry into force) mwezi Oktoba, 2014 katika kikao cha kumi na mbili (12) cha Mkataba wa Bioanuai kilichofanyika mjini Pyeongchang, Korea Kusini*.* Kwa mujibu wa utaratibu wa Mkataba wa Bioanuai(CBD), Itifaki hii ilianza kutumika baada ya nchi 50 kuridhia. Katika kikao cha 12 cha Mkataba wa Bioanuai nchi 50 zilikuwa zimekwisha ridhia Itifaki hii na

kuwezesha nchi wanachama wa Itifaki kuendesha kikao cha kwanza (COP-MOP 1) tarehe 13-17 Oktoba, 2014.

***Mheshimiwa Spika,*** Hadi Januari, 2017 nchi 92 zimesaini ambapo **nchi 96 duniani zimeridhia Itifaki ya Nagoya**. Katika ukanda wa nchi za Afrika Mashariki nchi za Rwanda (2014), Kenya (2014), Uganda (2014 na Burundi (2014) tayari zimeridhia Itifaki ya Nagoya ni Tanzania ambayo ilikuwa bado haijaridhia Itifaki hii. Hivyo kwa Bunge lako kukubali kuridhia itifaki Tanzania itakuwa imepiga hatua katika kuimarisha usimamazi wa rasilimali za kijenetiki kwa kushirikiana na nchi wanachama.

***Mheshimiwa Spika,***Tanzania tayari imeandaa Kanuni za kisheria zitakazosimamia mfumo mzima wa upatikanaji wa rasilimali za kijenetiki, matumizi yake na kuhakikisha mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali za kijenetiki nchini.

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Msukumo mkubwa wa kuridhia itifaki hii unatokana na watafiti wengi wa kigeni kusafirisha nje ya nchi rasilimali za kijenetiki bila kuzingatia mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali hizi. Hivyo, nchi wanachama ziliona kwamba kuna umuhimu wa kudhibiti hali hii ili nchi hizi ziweze kunufaika na rasilimali za kijenetiki pamoja na elimu asili ya rasilimali hizi katika nchi zao. Vilevile utekelezaji wa Itifaki hii unawiana na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Cap 191 Kifungu cha 230 (2) (d) ambacho kinatoa fursa ya kuandaa kanuni ya kusimamia rasilimali za kijenetiki.

***Mheshimiwa Spika,*** Dhamira za kuridhia Itifaki ni kwamba, endapo matumizi ya rasilimali za kijenetiki na elimu asili zinazohusisha matumizi ya rasilimali pamoja na kuimarisha fursa za mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali hizo zitaimarishwa, nchi wanachama zinatarajia kwamba Itifaki hii itakuwa kichocheo katika hifadhi ya bioanuai, matumizi endelevu ya bioanuai na bidhaa zitokanazo na bioanuai na pia Itifaki itaimarisha mchango wa bioanuai katika maendeleo endelevu na maisha ya wananchi kwa ujumla.

***Mheshimiwa Spika,*** Faida za kuridhia Itifaki hii kwa nchi yetu ni kuwa itawezesha nchi kuweka utaratibu wa kusimamia upatikanaji wa rasilimali za kijenetiki na mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali asili za kijenetiki. Ofisi inayoratibu shughuli za Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuai itaimarisha utekelezaji wa Mkataba pamoja na Itifaki ya Nagoya kikamilifu kwa kuweka mfumo sahihi wa kusimamia rasilimali za kijenetiki kwa matumizi ya watumiaji wa ndani na nje kwa kuzingatia taratibu zitakazowekwa.

***Mheshimiwa Spika,*** Kwa kuzingatia kwamba mfumo wa sasa hauna taratibu nzuri za kudhibiti wageni na wanaofanya tafiti kutoka nje, rasilimali zetu muhimu zinachukuliwa na kusafirishwa bila kujua, na matokeo ya tafiti hizo mbalimbali pamoja na faida zake zimekuwa hazijulikani na wala nchi au jamii ambako jenetiki hizo za tafiti zimechukuliwa hazifaidiki na tafiti hizo pamoja na faida itokanayo na tafiti. Nimatarajio yetu kuwa Itifaki hii itatusaidia mambao muhimu yafuatayo:

i. Kuweka misingi ya sheria na uwazi kwa watoaji wa watumiaji wa ndani na nje wa rasilimali za kijenetiki;

ii. Baada ya kuweka utaratibu sahihi watumiaji na watafiti wote watapaswa kuzingatia sheria za nchi zinazohusiana na rasilimaliasili za kijenetiki;

iii. Baada ya kuweka utaratibu sahihi wa kusimamia upatikanaji wa rasilimali asili za kijenetiki jamii zenye elimu asili zinazohusiana na rasilimali za kijenetiki zitafaidika na mgawanyo sahihi wa faida utakaozingatiwa katika makubaliano ya kupata rasilimali husika;

iv. Kuwepo kwa sheria itayoweka utaratibu mzuri wa upatikanaji wa rasilimali za kijenetiki utaimarisha udhibiti wa watumiaji hususan wageni kuhamisha holela rasilimali asili za kijenetiki kupitia vibali visivyozingatia faida ya matokeo ya utafiti wa rasilimali za kijenetiki; na

v. Kutokana na utaratibu utakaowekwa wa kuhakikisha

kuwa sehemu ya faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali za kijenetiki itarejeshwa kuendeleza hifadhi ya bioanuai, utaratibu huu utatoa motisha ya hifadhi na matumizi endelevu ya bioanuai na utabaoresha ustawi wa jamii kwa ujumla.

***Mheshimiwa Spika,*** Kutokana na mfumo wa uendeshaji wa Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuai, nchi wanachama hupata fursa za kubadilishana mbinu na uzoefu wa kusimamia hifadhi ya bionuai na pia fursa za kupata fedha kupitia vyanzo mbalimbali ikiwemo Mfuko wa Mazingira wa Dunia kwa ajili ya kutekeleza malengo ya Itifaki na Mkataba wa Hifadhi ya bioanuai kwa ujumla. Hivyo, katika kuendeleza shughuli za hifadhi ya bioanuai na kuimarisha hali ya maisha kwa jamii kuna umuhimu wa kuridhia Itifaki hii.

***Mheshimiwa Spika,*** Kutokana na kutokuwepo kwa sheria zinazodhibiti kikamilifu watumiaji wa rasilimali za kijenetiki hususan wageni na watafiti mbalimbali kutoka nje, wageni na watafiti wengi wamesafirisha rasilimali asili za kijenetiki nje ya nchi na kuziendeleza na kunufaika wao binafsi na mataifa yao kwa ujumla. Mfano mmea ujulikanao kama *Usambara violate* unaopatikana Milima ya Usambara umesafirishwa nje ya nchi na sasa wauzaji wengi wanajipatia fedha kutokana na mauzo ya mmea huu bila ya Tanzania kufaidika. Hivyo, kutoridhia Itifaki hii kutatoa mwanya zaidi kwa wageni na watafiti wengine kuendelea kukusanya na kusafirisha nje ya nchi mimea, wanyama, na viumbe wengine kwa faida yao na nchi zao.

***Mheshimiwa Spika,*** Hasara za kuacha kuridhia Itifaki hii itakuwa ni kulikosesha Taifa na wananchi mbalimbali fursa ya kunufaika na rasilimali za kijenetiki pamoja elimu asili zao zinazohusiana na rasilimali asili za kijenetiki ambazo wageni na watafiti wengi wamekuwa wakizipata bila kutoa mchango wowote. Hivyo, hasara ya kutoridhia Itifaki hii ina sura mbili nazo ni:

i. Kukosa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali za kijenetiki na zile elimu asili zinazohusiana na rasilimali za kijenetiki; na

ii. Uhamishaji holela wa rasilimali za kijenetiki utaendelea na wageni na watafiti wataendelea kujinufaisha bila kusaidia hifadhi ya bioanuai.

**Mheshimiwa Spika**, Vipengele muhimu vya Itifaki hii ni pamoja na:

**Moja, Ibara ya 6: Utaratibu wa kupata idhini ya kuchukua rasilimali za kijenetiki.** Ibara hii inahusu nchi kuweka taratibu za kupata idhini au vibali vya kukusanya mimea, wadudu, na wanyama kwa shughuli za kiutafiti au biashara ambapo idhini ya kupata rasiliami hizo lazima ipatikane kwa wale wanaomiliki rasilimali husika kwanza.

**Mbili, Ibara ya 7: Upatikanaji wa elimu asili inayohusu Rasilimali za kijenetiki.** Ibara hii inahusu nchi kuweka taratibu zitakazohakikisha kuwa elimu asili za jamii zinazohusiana na rasilimali za kijenetiki zinazingatiwa na idhini ya kupata rasilimali inatolewa na jamii husika kabla ya kukusanya.

**Tatu, Ibara ya 9: Uchangiaji wa Hifadhi na matumizi endelevu ya Bioanuai.** Ibara hii inaelekeza nchi wanachama kuhimiza watumiaji na watoaji wa rasilimali za kijenetiki kuchangia faida zitokanazo na rasilimali za kijenetiki.

**Nne, Ibara ya 10: Mfumo wa kimataifa wa mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali za kijenetiki**. Ibara hii inaelekeza nchi wanachama kuzingatia umuhimu wa kuwa na mfuko wa dunia wa pamoja ambao utazingatia namna ya kupata idhini na faida kwa rasilimali za kijenetiki zilizoko mipakani ambazo zitahusisha jamii husika za z anchi mbili au zaidi.

**Tano, Ibara ya 13: Kuteua Mratibu wa kitaifa na mamlaka zenye dhamana ya kusimamia rasilimali za kijenetiki.** Ibara hii inaelekeza kila nchi wanachama kuteua Mratibu wa kitaifa na mamlaka zenye dhamana ya kusimamia rasilimali za kijenetiki kwa lengo la kufanya mawasilano na Sekretariati ya Mkataba ya bioanuai.

**Sita, Ibara ya 21: Kukuza uelewa wa wadau na jamii kwa ujumla kuhusu Itifaki.** Ibara hii inaelekeza nchi wanachama kukuza uelewa kuhusu umuhimu wa rasilimali za kijenetiki na elimu asili inayohusiana na rasilimali za kijenetiki na faida zitokanazo na upataikanaji wa rasilimali za kijenetiki.

**Saba, Ibara ya 22: Kujenga uwezo wa Taasisi na Rasilimali watu katika kusimamia na kutekeleza kikamilifu Itifaki.** Ibara hii inaelekeza nchi wanachama kujenga uwezo wa taasisi na rasilimali watu kwa ajili ya utekelezaji wa itifaki hii katika ngazi ya kitaifa na kimataifa. Hatua za kujenga uwezo ni pamoja na kujenga uwezo wa jamii asili na wananchi hususan wanawake kuhusiana na upatikanaji wa rasilimali za kijenetiki au elimu asili inayowiana na rasilimali za kijenetiki.

***Mheshimiwa Spika,*** Matokeo ya kuridhia Itifaki hii ni kuwezesha kuwepo kwa utaratibu wa upatinaji na mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali asili za kijenetiki ikiwa ni pamoja na:

i. Kuweka misingi ya Sheria na uwazi kwa watoaji na watumiaji wa rasilimali asili za kijenetiki;

ii. Kuwezesha uzingatiaji wa sheria za nchi zinazohusiana na rasilimali asili za kijenetiki;

iii. Kuwezesha jamii kufaidika na elimu au ujuzi asili wa rasilimali za kijenetiki;

iv. Kuimarisha udhibiti wa uhamishaji holela wa rasilimali asili za kijenetiki bila faida kwa nchi na jamii kwa ujumla;

v. Kutoa motisha ya hifadhi na matumizi endelevu ya bioanuai kwa ajili ya ustawi wa jamii kwa ujumla; na

vi. Kupata fursa za fedha kwa ajili ya kutekeleza malengo ya Itifaki.

**Mheshimiwa Spika;** baada ya maelezo haya, sasa naomba kuwasilisha Azimio la Bunge la kuridhia kama ifuatavyo;

**KWA KUWA,** Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Mkataba wa Bioanuai wa Mwaka 1992 unaohusu hifadhi ya bioanuai, matumizi endelevu ya bioanuai, na mgawanyo wa faida zitokanazo na matumizi ya bioanuai ambao uliridhiwa tarehe 8 Machi, 1996;

**NA KWA KUWA,** Chini ya Mkataba huu kuna Itifaki ya Cartagena ya Mwaka 2000, inayohusu Usimamizi Salama wa Mazingira Dhidi ya Athari Zinazoweza kutokea kutokana na Matumizi ya Biotekinolojia ya Kisasa ambayo Tanzania iliridhia tarehe 16 Machi, 2003;

**NA KWA KUWA,** katika Mkutano wa sita (**6**) wa Mkataba wa Bioanuai uliofanyika Johannesburg, Jamhuri ya Afrika Kusini Mwaka 2002, ulibaini kwamba lengo la tatu la Mkataba huo linalohusu mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali za kijenetiki halijafikiwa kutokana na kukosekana kwa mfumo wa kusimamia utekelezaji wa Mkataba huo;

**NA KWA KUWA,** ili kuweka mfumo wa usimamizi wa Mkataba, mchakato wa kuanzisha Itifaki ya Kusimamia Upatikanaji na Mgawanyo Sahihi wa Faida Zitokanazo na Matumizi ya Rasilimali za Kijenetiki ulianzishwa na Itifaki hii ilipitishwa katika Mkutano wa 10 wa Nchi Wanachama wa Mkataba uliofanyika Nagoya, Japan Mwaka 2010.

**NA KWA KUWA,** Tanzania iliridhia Mkataba wa Bioanuai Mwaka 1996 ambao umeanzisha Itifaki ya Kusimamia Upatikanaji na Mgawanyo Sahihi wa Faida Zitokanazo na Matumizi ya Rasilimali za Kijenetiki (*The Nagoya Protocol on Access to Genetic Resources and the Fair and Equitable Sharing of Benefits Arising From their Utilisation to the Convention on Biological Diversity*) ambapo Ibara ya 33 ya Itifaki hii, inaweka masharti ya kuridhiwa na Nchi Wanachama na kisha Hati ya kuridhia *(Instruments of Accession*) kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa;

**NA KWA KUWA** Tanzania kwa kuridhia Itifaki hii na hatimaye kuitekeleza itanufaika na mambo yafuatayo:

(a)kuwa na misingi ya Sheria na uwazi kwa watoaji na watumiaji wa rasilimali za kijenetiki kuwekwa;

(b)Sheria za Nchi zinazohusiana na rasilimali za kijenetiki kuzingatiwa;

(c) jamii itanufaika na elimu au ujuzi asili wa rasilimali za kijenetiki;

(d)kudhibiti uhamishaji holela wa rasilimali za kijenetiki bila faida kwa Nchi na Umma kwa ujumla;

(e)kuongezeka kwa motisha ya hifadhi na matumizi endelevu ya bioanuai kwa ajili ya ustawi wa jamii; na

(f) kupatikana kwa fursa za fedha kwa ajili ya kutekeleza malengo ya Itifaki.

**HIVYO BASI,** kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya Itifaki hii kwa Tanzania, Bunge hili katika Mkutano wa Saba (7) na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka, 1977, linaazimia kuridhia **ITIFAKI YA KUSIMAMIA UPATIKANAJI NA MGAWANYO SAHIHI WA FAIDA ZITOKANAZO NA MATUMIZI YA RASILIMALI ZA KIJENETIKI yaani** *Nagoya Protocol on Access to Genetic Resources and the Fair and Equitable Sharing of Benefits Arising from their Utilization to the Convention on Biological Diversity.*

**Mheshimiwa Spika;** naomba kuwasilisha na kutoa hoja**.**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Biashara, ajiandae Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO – KAIMU MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Bunge Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Marekebisho

wa Nairobi wa Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi mwa Bahari ya Hindi yaani *Amended Convention for the Protection, Management and Development of the Marine and Coastal Environment of the Western Indian Ocean.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6)(b) naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Marekebisho ya Nairobi wa Hifadi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani wa Magharibi ya Bahari ya Hindi Itifaki ya Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari yaani *Amended Convention for the Protection, Management and Development of the Marine and Coastal Environment of the Western Indian Ocean.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia masharti ya fasili ya 6(b), kifungu cha 53 ikisomwa pamoja na fasili ya 1(b) ya kifungu cha 7, Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira inalo jukumu la kushughulikia mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hoja ya Serikali kuhusu Bunge kuridhia marekebisho ya Mkataba wa Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi yaani *Amended Convention for the Protection, Management and Development of the Marine and Coastal Environment of the Western Indian Ocean* ililetwa kwenye Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa mujibu wa Kanuni ya 53 ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee chimbuko la mkataba wa marekebisho. Tanzania ni moja ya nchi ya Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi zina utajiri mkubwa wa rasilimali za bahari zikiwemo madini (ikiwemo gesi asilia na mafuta), samaki na mimea. Rasilimali

hizi zimekuwa na mchango wa pekee katika uchumi wa ukanda huu. Ili kutumia ipasavyo rasilimali zake ilionekana ni vyema nchi mbalimbali kushirikiana katika kutunza mazingira ya bahari. Kwa lengo hilo mkataba wa awali wa Nairobi wa Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari ya Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi uliridhiwa tarehe 21 Juni, 1985 huko Nairobi. Mkataba huo ulilenga kuzuia au kukabiliana na uchafuzi wa mazingira ya bahari unaotokana na:-

(i) Shughuli na vyombo vya usafirishaji baharini kama meli;

(ii) Utupaji wa taka;

(iii) Vyanzo na shughuli mbalimbali za kiuchumi zilizoko nchi kavu;

(iv) Utafutaji na uchimbaji maliasili mbalimbali zilizopo baharini; na

(v) Usafirishaji wa taka zenye sumu unaovuka mipaka ya nchi moja kwenda nchi nyingine na uchafuzi wa hewa/ anga unaotokana na shughuli mbalimbali kama usafiri wa ndege wa angani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekebisho ya Mkataba wa Nairobi wa Hifadhi, Usimamizi na Uendeshaji wa Mazingira ya Bahari ya Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi kwa kifupi Marekebisho ya Mkataba yaani (*Amended Convention for the Protection, Management and Development of the Marine and Coastal Environment of the Western India Ocean)* uliandikwa kwa kuzingatia changamoto mpya zilizojitokeza tangu kusainiwa kwa mkataba wa awali. Andiko la Mkataba wa Marekebisho lilikubaliwa na mkutano wa nchi za Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi tarehe 31 Machi, 2010 huko Nairobi. Moja ya nchi zilizokuwepo katika mkutano huo ni Nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika andiko la Mkataba wa Marekebisho, nchi za Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi zilidhamiria kuendelea kuzuia au kukabiliana na vyanzo vya uchafuzi vilivyoainishwa katika mkataba wa awali (namba 1 - 6 ambavyo nimevitaja hapo juu). Zaidi ya hayo, Mkataba wa Marekebisho umezingatia yafuatayo:-

(i) Haja ya kulinda na kudumisha bionuai ili kulinda shughuli za kiuchumi kama uvuvi ambao umekuwa ukidumaa kuanzia mwaka 2000;

(ii) Mabadiliko ya tabianchi na athari zake kwa viumbe hai kama vile, ongezeko la halijoto na kina cha bahari, kupungua kwa alkali au ongezeko la tindikali kwenye maji ya bahari, mabadiliko ya miongo na kadhalika;

(iii) Utambuzi wa haja ya kuwa na usimammizi wa pamoja wa maendeleo ya sekta mbalimbali za uchumi katika Ukanda wa Pwani yaani *intergrated coastal zone management* ya bahari ya Magharibi ya Bahari ya Hindi;

(iv) Makubaliano ya Mkutano wa Umoja wa Mataifa juu ya Mazingira na Maendeleo yaani *outcomes and decisions of the 1992 United Nations Conference on Environment and Development;*

(v) Ilikuwa ni mazingira maalum na hatarishi yanayojitokeza kwa nchi na visiwa hasa kutokana na madhara ya mabadiliko ya tabianchi;

(vi) Haja ya kuhamasisha utekelezaji kitaifa na kimataifa kwa mikataba mbalimabli ya kimataifa;

(vii) Nafasi ya taasisi zisizo za kiserikali yaani *Non-Governmental Organizations – NGO's*, makundi ya kijamii na wanaharakati mbalimbali katika kuhamasisha utunzaji bora wa mazingira;

(viii) Uwepo wa mikataba mbalimbali ya kimataifa juu ya mazingira ya bahari ambayo ukizingatia inapaswa hali

halisi ya Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi na kadhalika; na

(ix) Ongezeko la ukubwa wa eneo la mkataba na kujumuisha pwani ya nchi ya Afrika Kusini iliyojikomboa kutokana na ubaguzi wa rangi mwaka 1992.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya kazi yake tarehe 14 Juni, 2017 na Kamati ilikutana na kupata maelezo ya Serikali kuhusu pendekezo la kuridhia Mkataba wa Marekebisho ya Nairobi. Aidha, tarehe 18 Juni, 2017 Ofisi ya Bunge kupitia Mradi wa *LSP* iliiwezesha Kamati kupata uelewa na stadi muhimu kuhusu utaratibu wa Bunge kuridhia mikataba ya kimataifa. Uelewa huu uliisaidia Kamati kuwa katika nafasi nzuri ya kuifanyia kazi hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipotekeleza jukumu lake kuhusiana na hoja hii, ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117(8) na 117(9) kuhusu utaratibu wa Kamati pamoja na kuwaalika wadau. Katika hatua hii, Kamati iliwaalika wataalam kutoka Asasi za Serikali, Asasi za Kiraia (AZISE) na wadau wengine kwa ajili ya kupata maoni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru wadau wote waliowasilisha maoni yao kwa Kamati. Kwa namna ya pekee Kamati inakishukuru Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia Taasisi ya Sayansi ya Bahari kwa maoni na ushauri wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijiridhisha kuhusu hali iliyofikiwa katika mkataba huu kwa kuangalia nguvu ya kisheria ya mkataba. Mkataba wa Marekebisho uliopita uliwapatia nguvu ya kisheria ya tarehe 1 Aprili, 2010 kwa mujibu wa Ibara ya 29 kwa kuuweka wazi tayari kusainiwa na nchi wanachama. Nchi wanachama na ambazo sio wanachama zilizoalikwa na kuridhia kusaini kuanzia tarehe 1 Aprili, 2010 hadi tarehe 1 Aprili, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Marekebisho ya Mkataba huu utaanza siku 19 yaani mara baada ya nchi

mwanachama wa sita kuwasilisha hati ya kuridhia, ni kwa mujibu wa Ibara ya 32(2) ya Marekebisho ya Mkataba. Mpaka sasa ni nchi mbili tu ndio zimekwisha wasilisha Hati ya kuridhia na nchi nyingine zipo katika hatua za kuridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba radhi kwa sababu ya muda, baadhi ya mambo mengine yaingie kwenye kumbukumbu. Naomba sasa niende moja kwa moja kwenye maoni na ushauri wa Kamati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wako ni mdogo na una maazimio matatu. Ungeyapitisha yote ili mengine yaingie kwenye *Hansard.* Umebakiwa na dakika tano tu.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO – KAIMU MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa nashukuru. Nakwenda kwenye maoni na ushauri moja kwa moja wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza yote haya naomba sasa kutoa maoni ya mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Marekebisho ni muhimu kwa Tanzania na nchi nyingine za Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi kutokana na changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza makubaliano ya awali yaliyofanyika takribani miongo mitatu iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Marekebisho utaiwezesha Tanzania kama nchi na kwa kushirikiana na nchi majirani zake katika Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi kukabiliana na changamoto za uchafuzi na mabadiliko mengine yanayoathiri mazingira ya bahari kwa ukamilifu zaidi. Kama ilivyo kwa mkataba wa awali, mkataba wa Marekebisho pia umezingatia haja ya nchi za Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi kuwa na mtandao wa taasisi zake za utafiti ili kuimarisha mashirikiano katika tafiti, ufuatiliaji na ubadilishanaji wa taarifa. Kujumuika kwa

Afrika Kusini katika Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi kunatoa fursa kubwa na ya pekee kwa maendeleo ya sayansi na teknolojia ya mambo ya bahari. Kutokana na umuhimu huu Kamati inalishauri Bunge lako kuridhia Marekebisho ya Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wa kuridhia, yapo baadhi ya maeneo ambayo ni vyema tukachukua tahadhari katika utekelezaji wa mkataba huu. Ibara ya 26 ya Mkataba wa Marekebisho unaitaka nchi iliyokubaliana na mkataba iwe imesaini angalau moja ya itifaki zake kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 4, na pia nchi haiwezi kuwa mjumbe wa Itifaki bila kuwa mjumbe wa Mkataba wa Marekebisho.

Aidha, Ibara ya 33 inayoelezea kujitoa katika Mkataba, yaani nchi haiwezi kujitoa kwenye Mkataba wa Marekebisho ikabaki kwenye Itifaki au kinyume chake. Kamati inashauri Serikali kuzingatia mambo haya kwa ajili ya madhara ya kiuchumi yanayoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa suala la mazingira na mabadiliko ya tabianchi, Kamati inakubaliana na maelezo ya Serikali kuhusu faida zitakazopatikana na kuridhia Azimio hili, pamoja na ukweli kwamba Azimio hili halikuletwa kwa wakati. Kamati inaishauri Serikali kuleta Bungeni kwa wakati mikataba yote ya Kimataifa ili iweze kuridhiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuwa makini na mikataba inayohusu mazingira ya bahari kwa kuwa inaweza kuwa kikwazo katika uvunaji wa rasilimali za baharini ikiwemo ugunduzi wa gesi asilia, uvuvi, kilimo, makazi na viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe mwenzangu ambaye anakwenda sasa kutoa maoni ya Kamati kuhusiana na Itifaki ya Mazingira na baada ya hapo atakuja mwingine atatoa maoni ya Itifaki ya Nagoya. Ahsante sana.

# MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI KUHUSU AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA MKATABA WA MAREKEBISHO WA NAIROBI WA HIFADHI, USIMAMIZI NA UENDELEZAJI WA MAZINGIRA YA BAHARI NA UKANDA WA PWANI YA MAGHARIBI MWA BAHARI YA HINDI - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

**(***Amended Convention for the Protection, Management and Development of the Marine and Coastal Environment of the Western Indian Ocean***)**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b), naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Marekebisho wa Nairobi wa Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi (Amended *Convention for the Protection, Management and Development of the Marine and Coastal Environment of the Western Indian Ocean).*

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya fasili ya 6(b), Kifungu cha 53 ikisomwa pamoja na fasili ya 1(b) ya Kifungu cha 7, Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira inalo jukumu la kushughulikia Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Hoja ya Serikali kuhusu Bunge kuridhia Mkataba wa Marekebisho wa Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahariya Hindi (Amended *Convention for the Protection, Management and Development of the Marine and Coastal Environment of the Western Indian Ocean),* ililetwa kwenye Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (3) ya Kanuni za Bunge.

## 2.0 CHIMBUKO LA MKATABA WA MAREKEBISHO

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni moja ya nchi za Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi zina utajiri mkubwa wa rasilimali za bahari zikiwemo, madini (ikiwemo gesi asilia na mafuta), samaki na mimea. Rasilimali hizi zimekuwa na mchango wa pekee katika uchumi wa ukanda huu. Ili kutumia ipasavyo rasilimali zake ilionekana ni vyema nchi mbalimbali kushirikiana katika kutunza mazingira ya bahari. Kwa lengo hilo Mkataba wa awali wa Nairobi wa Hifadhi, Usimamizi na Uendeshaji wa Mazingira ya Bahari ya Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi uliridhiwa tarehe 21 June 1985 huko Nairobi. Mkataba huo ulilenga kuzuia na/au kukabiliana na uchafuzi wa mazingira ya bahari unaotokana na:

i) Shughuli na vyombo vya usafirishaji baharini k.m. meli;
ii) Utupaji wa taka;
iii) Vyanzo na shughuli mbalimbali za kiuchumi zilizoko nchi kavu;
iv) Utafutaji na uchimbaji maliasili mbalimbali zilizopo baharini;
v) Usafirishaji wa taka zenye sumu unaovuka mipaka ya nchi moja kwenda nchi nyingine; na
vi) Uchafuzi wa hewa/anga unaotokana na shughuli mbalimbali k.m. usafiri wa ndege angani.

**Mheshimiwa Spika**, Marehebisho ya Mkataba wa Mkataba wa Nairobi wa Hifadhi, Usimamizi na Uendeshaji wa Mazingira ya Bahari ya Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi (kwa kifupi – Marekebisho ya Mkataba) – (*Amended Convention for the Protection, Management and Development of the Marine and Coastal Environment of the Western India Ocean*) uliandikwa kwa kuzingatia changamoto mpya zilizojitokeza tangu kusainiwa kwa mkataba wa awali. Andiko la Mkataba wa Marekebisho lilikubaliwa na mkutano wa nchi za Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi tarehe 31 March 2010 huko Nairobi. Moja ya nchi zilizokuwepo katika mkutano huo na kuridhia andiko hilo ni Tanzani.

**Mheshimiwa Spika,** katika andiko la Mkataba wa Marekebisho, nchi za Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi zilidhamiria kuendelea kuzuia na/au kukabiliana na vyanzo vya uchafuzi vilivyoainishwa katika mkataba wa awali (nambari 1-6 hapo juu). Zaidi ya hayo, Mkataba wa Marekebisho umezingatia yafuatayo:

i) Haja ya kulinda na kudumisha bayoanuai ili kulinda shughuli za kiuchumi kama uvuvi ambao umekuwa ukidumaa kuanzia miaka ya 2000;

ii) Mabadiliko ya tabianchi na athari zake kwa viumbehai, kama vile, ongezeko la halijoto na kina cha bahari, kupungua kwa alkali au ongezeko la tindikali kwenye maji ya bahari, mabadiliko ya miongo n.k.;

iii) Utambuzi wa haja ya kuwa na usimammizi wa pamoja wa maendeleo ya sekta mbalimbali za uchumi katika ukanda wa pwani *(intergrated coastal zone management)* ya bahari ya Magharibi ya Bahari ya Hindi;

iv) Makubaliano ya Mkutano wa Umoja wa Mataifa juu ya Mazingira na Maendeleo (*Outcomes and decisions of the 1992 United Nations Conference on Environment and Development*);

v) Mazingira maalum na hatarishi yanayojitokeza kwa nchi za visiwa hasa kutokana na madhara ya mabadiliko ya tabianchi;

vi) Haja ya kuhamasisha utekelezaji kitaifa na kimataifa wa mikataba mbalimabli ya kimataifa;

vii) Nafasi ya taasisi zisizo za kiserikali (*non-governmental organisations – NGO*), makundi ya kijamii na wanaharakati mbalimbali katika kuhamasisha utunzaji bora wa mazingira;

viii) Uwepo wa Mikataba mbalimbali ya kimataifa juu ya mazingira ya bahari ambayo haikuzingatia ipasavyo hali halisi ya Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi; n.k.

ix) Ongezeko la ukubwa wa eneo la mkataba na kujumuisha pwani ya nchi ya Afrika Kusini iliyojikomboa kutokana na ubaguzi wa rangi mwaka 1992.

## 3.0 NAMNA KAMATI ILIVYOSHUGHULIKIA HOJA HII

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 14 Juni, 2017 Kamati ilikutana na kupata maelezo ya Serikali kuhusu pendekezo la kuridhia Mkataba wa Marekebisho wa Nairobi. Aidha, tarehe 18 Juni, 2017 Ofisi ya Bunge kupitia Mradi wa LSP iliiwezesha Kamati kupata uelewa na stadi muhimu kuhusu Utaratibu wa Bunge kuridhia Miakataba ya Kimataifa. Uelewa huu uliisaidia Kamati kuwa katika nafasi nzuri ya kuifanyia kazi hoja hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipotekeleza jukumu lake kuhusiana na hoja hii, ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117 (8) na 117 (9) kuhusu utaratibu wa Kamati pamoja na kuwaalika wadau. Katika hatua hii, Kamati iliwaalika wataalamu kutoka asasi za Serikali, asasi za kiraia (AZISE) na wadau wengine kwa ajili ya kupata maoni yao. Tunawashukuru wadau wote waliowasilisha maoni yao kwa Kamati. Kwa namna ya pekee Kamati inakishukuru Chuo Kikuu cha Dar es Salaa kupitia taasisi ya Sayansi ya Bahari kwa maoni na ushauri wao.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (e), Kamati ilizingatia mambo mbalimbali yaliyo muhimu katika kuifanyia kazi hoja ya Serikali iliyo mezani leo. Mambo hayo ni pamoja na kuangalia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baadhi ya Sheria za nchi zinazohusiana moja kwa moja na maudhui ya Mkataba unaopendekezwa, Uzoefu wa nchi nyingine katika masuala muhimu ya Mkataba na kutafakari kuhusu hasara au faida na kiwango cha manufaa au madhara yanayoweza kupatikana kwa kuridhia au kutokuridhia Mkataba huu. Kamati ilijiridhisha pia iwapo kuna umuhimu wa kuridhia Mkataba huu kama ulivyo au kuridhia baadhi ya vifungu vya Mkataba (*Ratifying with reservation*).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijiridhisha kuhusu hali iliyofikiwa katika Mkataba huu kwa kuangalia nguvu ya kisheria ya Mkataba. Mkataba wa Marekebisho ulipata nguvu ya kisheria tarehe 1 Aprili, 2010 kwa mujibu wa **Ibara 29** kwa kuuweka wazi tayari kusainiwa na nchi wanachama. Nchi wanachama na ambazo siyo wanachama zilizoalikwa na kuridhia kusaini kuanzia tarehe 1 Aprili, 2010 hadi 1 Aprili, 2011.

**Nanukuu***: **Article 29** "This convention shall be open for signature at the Nairobi, Kenya from the 1 April, 2010 to 1 April, 2011 by any Contracting party and non-contracting party that has been invited to the conference of Plenipotentiaries"* **Mwisho wa kunukuu***.*

Kwa kuzingatia takwa la Ibara hiyo Mkataba wa Marekebisho huu ulisajiliwa tarehe 1 Aprili, 2010 na kupewa Namba UNEP (DEPI)/EAF/CPP.6/11/Suppl na Nchi Wanachama zote kumi (10). Kwa sasa Nchi Wanachama zinaendelea na taratibu za kuridhia.

Utekelezaji wa Mkataba wa Marekebisho huu utaanza siku kumi na tisa (19) mara baada ya nchi mwanachama wa sita (6) kuwasilisha hati ya kuridhia hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 32 (2) ya Marekebisho ya Mkataba.

**Nanukuu***: **Article 32 (2) "**This convention shall enter into force on the ninetieth day following the date of the deposit of the sixth instrument of ratification, acceptance, approval or accession to this Convention by the states and organizations referred to in article 30"* **Mwisho wa kunukuu***.*

Mpaka sasa ni nchi mbili tu ndio zimekwisha wasilisha Hati ya kuridhia na nchi nyingine zipo katika hatua za kuridhia kulingana na taratibu za nchi husika.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, kwa mujibu wa **Ibara ya 33(1-5)** ya Mkataba wa Marekebisho huu unaruhusu Nchi Mwanachama kujitoa katika Mkataba, ambapo inaeleza kuwa, muda wowote baada ya miaka mitatu tangu

Mkataba kuanza kutekelezwa, nchi inaweza kujitoa kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa mtunza nyaraka.

**Nanukuu: Mfano, Article 33 (1)** "*At any time after three years from the date on which this Protocol has entered into force for a Party, that Party may withdraw from this protocol by giving written notification to the Depositary* " **Mwisho wa kunukuu**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Tanzania ni moja ya nchi wanachama wa Mikataba mbalimbali, Kamati ilizingatia umuhimu wa kulinganisha misimamo ya nchi hizi kwa mustakabali wa ushirikiano wetu. **Ibara ya 3 (1)** ya Mkataba wa Marekebisho wa Nairobi inairuhusu nchi mwanachama kuingia mikataba mingine ya uhifadhi na usimamizi wa Pwani ya Bahari lakini Mikataba hiyo isikinzane na utekelezaji wa Mkataba huu.

**Nanukuu: Mfano, Article 3(1)** "*The Contracting Parties may enter into a bilateral or multilateral agreements, including regional or sub regional agreements, for the protection and management of the marine and costal environment of the Convention area. Such agreement shall be considered with this Convention and Protocols made and in accordance with international law. Copies of such agreement should communicated to the organization and through the Organization to all Contracting Parties*" **Mwisho wa kunukuu**.

**Mheshimiwa Spika**, Mkataba wa Msingi kuhusu Mikataba ya Kimataifa ni Mkataba wa **Viena** ambao Tanzania iliuridhia mwaka 1976. Mkataba wa **Viena** umeweka kanuni za msingi kuhusu uridhiaji wa mikataba ya kimataifa. Kanuni hizo muhimu zilizngatiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, wakati wa kuifanyia kazi hoja iliyopo mbele ya Bunge hili kwa sasa.

**Mheshimiwa Spika,** Mkataba wa Marekebisho wa Nairobi ya Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi ni

Mkataba wa Nyongeza unaotokana Mkataba wa Nairobi (CBD..1996)

**Mheshimiwa Spika**, suala la Uhifadhi wa Mazingira ya Bahari na ukanda wa Pwani kwa Tanzania linafahamika, Serikali kwa kushiriana na wahisani imechkua hatua mbalimbali ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Hili linajidhihirisha katika miradi ya ujezi wa kingo za bahari Pangani, *Ocean road*, Kigomboni na Kisiwa Panza Zanzibar.

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kueleza yote hayo, naomba sasa kutoa maoni na mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

**Mheshimiwa Spika**, Mkataba wa Marekebisho ni muhimu kwa Tanzania na nchi nyingine za Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi kutokana na changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza makubaliano ya awali yaliyofanyika takriban miongo mitatu iliyopita. Mkataba wa Marekebisho utaiwezesha Tanzania kama nchi na kwa kushirikiana na nchi majirani zake katika Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi kukabiliana na changamoto za uchafuzi na mabadiliko mengine yanayoathiri mazingira ya bahari kwa ukamilifu zaidi. Kama ilivyo kwa mkataba wa awali, mkataba wa Marekebisho pia umezingatia haja ya nchi za Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi kuwa na mtandao wa Taasisi zake za utafiti ili kuimarisha mashirikiano katika tafiti, ufuatiliaji na kubadilishana taarifa. Kujumuika kwa Afrika Kusini katika Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi kunatoa fursa kubwa na ya pekee kwa maendeleo ya sayansi na teknolojia ya mambo ya bahari. Kutokana na umuhimu huuKamati inalishauri Bunge lako kuridhia Marekebisho ya Mkataba huu.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na umuhimu wa kuridhia, yapo baadhi ya maeneo ambayo ni vyema tukachukua tahadhari katika utekelezaji wa mkataba huu.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 26 ya Mkataba wa Marekebisho unaitaka nchi iliyokubaliana na mkataba pia iwe imesaini angalau moja ya itifaki zake kama ilivoainishwa katika ibara ya 4; na pia nchi haiwezi kuwa mjumbe wa Itifaki bila kuwa mjumbe wa Mkataba wa Marekebisho. Aidha, Ibara ya 33 inayoelezea kujitoa katika Mkataba, yaani nchi haiwezi kujitoa kwenye Mkataba wa Marekebisho ikabaki kwenye Itifaki au kinyume chake. Kamati inashauri Serikali kuzingatia mambo haya ajili ya madhara ya kiuchumi yanayoweza kujitokeza.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia umuhimu wa suala la mazingira na mabadiriko ya tabianchi, Kamati inakubaliana na maelezo ya Serikali kuhusu faida zitakazopatikana kwa kuridhia Azimio hili, pamoja na ukweli kwamba Azimio hili halikuletwa kwa wakati. Kamati inaishauri Serikali kuleta Bungeni kwa wakati mikataba yote ya Kimataifa ili iweze kuridhiwa kwa wakati;

**Mheshimi Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuwa makini na mikataba inayohusu mazingira ya bahari kwa kuwa inaweza kuwa kikwazo katika uvunaji wa rasilimali za baharini ikiwemo ugunduzi wa Gesi asilia, uvuvi, kilimo, makazi na Viwanda;

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nikushukuru sana wewe kwa uongozi wako mahiri na kwakunipa ruhusa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati. Niwashukuru pia Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia shughuli za Bunge kwa umakini na umahiri.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira Mhe. January Makamba(Mb), Naibu Waziri wake Mhe. Luhaga Joelson Mpina (Mb) Makatibu Wakuu, pamoja na wataalamu wote wa Ofisi hii muhimu kwa ushirikiani walioutoa wakati wa kujadili Azimio hili.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kupitia kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni yake juu ya Azimio hili mbele ya Bunge hili tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini na kwa ruhsa yako naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge.

| | |
|---|---|
| (i) Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo Mb | Mwenyekiti |
| (ii) Mhe. Vicky Passcal Kamata, Mb | Mjumbe |
| (iii) Mhe. Salim Hassan Turky, Mb | Mjumbe |
| (iv) Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb | Mjumbe |
| (v) Mhe Dkt. Dalaly Peter Kafumu | Mjumbe |
| (vi) Mhe. Khatib Said Haji, Mb | Mjumbe |
| (vii) Mhe. Tauhida Cassian Gallos, Mb | Mjumbe |
| (viii) Mhe. Munira Mustafa Khaibu, Mb | Mjumbe |
| (ix) Mhe. Anthony Calist Komu, Mb | Mjumbe |
| (x) Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb | Mjumbe |
| (xi) Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa,Mb | Mjumbe |
| (xii) Mhe. Lameck Okambo Airo, Mb | Mjumbe |
| (xiii) Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb | Mjumbe |
| (xiv) Mhe. Balozi Dkt Diodorus Kamala, Mb | Mjumbe |
| (xv) Mhe. Jesca David Kishoa, Mb | Mjumbe |
| (xvi) Mhe. Mbarouk Salim Ali, Mb | Mjumbe |
| (xvii) Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb | Mjumbe |
| (xviii) Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest, Mb | Mjumbe |
| (xix) Mhe. Faida Mohammed Bakar, Mb | Mjumbe |
| (xx) Mhe. Suleiman Ahmed Sadick, Mb | Mjumbe |
| (xxi) Mhe Ibrahim Hassanali Raza, Mb | Mjumbe |
| (xxii) Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb | Mjumbe |
| (xxiii) Mhe. Dkt. Raphael MMasunga Chegeni, Mb | Mjumbe |
| (xxiv) Mhe. Sylvestry Francis koka, Mb | Mjumbe |
| (xxv) Mhe. Gimbi Dotto Massaba, Mb | Mjumbe |
| (xxvi) Mhe. Martha Mosses Mlata, Mb | Mjumbe |
| (xxvii) Mhe. Joyce John Mukya, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Athumani Hussein; Mkurugenzi msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi Bw. Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati Bw. Wilfred Magova na Bi. Zainab Mkamba na Msaidizi wa Kamati Bi Paulina Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio.

Stanslaus Haroon Nyongo, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA**
29 Juni, 2017

**MWENYEKITI:** Aaah! Mimi nilifikiri unamaliza wewe yote kwa sababu yote ilikuwa haifiki dakika 20.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO – KAIMU MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako nadhani...

**MWENYEKITI:** Humalizi yote wewe?

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO – KAIMU MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana.

**MWENYEKITI:** Haya basi muite huyo. Muite.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO – KAIMU MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Dakika tano!

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA - K.N.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika tano au kumi?

**MWENYEKITI:** Mengine yataingia kwenye *Hansard!* Wewe toa kauli mengine yaingie kwenye *Hansard.*

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA - K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira Kuhusu Azimio la Bunge kuridhia Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi kutokana na vyanzo na shughuli zinazofanyika nchi kavu *(Protocal for the Protection of the Marine and Coastal Environment of the Western Indian Ocean from Land-based sources and activities).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kutokana na muda kuwa finyu sana naomba taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard* kama ilivyo na vilevile maeneo yote yaliyoandikwa protokali naomba yasomeke kama itifaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda ni mchache sana inabidi niruke maeneo mengine ndiyo maana nimesema yaingie kwenye *Hansard* kama ilivyo.

Naomba nisome maoni na ushauri wa Kamati; baada ya kueleza yote hayo naomba sasa kutoa maoni na mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, itifaki hii ina umuhimu mkubwa katika kulinda na kuhifadhi mazingira ya fukwe na yale ya bahari pamoja na rasilimali zake. Maeneo ya fukwe na bahari yana rasilimali nyingi ambazo ni muhimu kwa maisha ya binadamu lakini pia kwa uchumi wa nchi. Maeneo haya yamekuwa yakiathiriwa sana na uchafu pamoja na athari zingine zitokanazo na shughuli za kibinadamu zikiwepo makazi, kilimo, viwanda na shughuli nyingine zinazozalisha uchafu na vitu vingine vinavyoweza kuathiri mazingira ya

bahari. Kutokana na umuhimu huo, Kamati inalishauri Bunge lako kuridhia nyongeza ya Mkataba huu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA - K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ushauri huo wa kuridhia, yapo baadhi ya maeneo ambayo ni vyema tukachukua tahadhari katika utekelezaji wa mkataba huu.

**MHE. JOHN J. MYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Kamati inaishauri Serikali kwamba wakati wa utekelezaji wa sharti la Ibara hii izingatie mustakaali wa uchumi wa wananchi watakaoathiriwa na itifaki hii. Aidha ni vyema Serikali ikatoa...

**KUHUSU UTARATIBU**

**MWENYEKITI:** Subiri! Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumevumilia muda mrefu. Msomaji wa kwanza alikuwa anasoma hatuna Taarifa ya Kamati, msomaji wa pili anasoma hatuna Taarifa ya Kamati. Tungeweza kuvumilia na kusikiliza kama tu angekuwa anasoma ripoti yote sasa kwa bahati mbaya mambo yote wanasema yameingia kwenye *Hansard* kwa hiyo, maana yake hata kusikiliza napo hatuwezi kuyasikia. Sasa tutayasoma saa ngapi, tutachangia saa ngapi. Naomba utaratibu kabla hajaendelea mbele tupewe nakala...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, hebu kaa kwanza. Mheshimiwa Mnyika hebu kaa. Taarifa zote zinasambazwa sasa hivi. Mheshimiwa Mwanjelwa endelea.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.Vilevile ili kuweza kutekeleza kikamilifu masharti ya Ibara hii upo umuhimu wa kuainisha sheria, sera, programu na masuala mengine ya usimamizi ya nchi zote zitakazo saini makubaliano haya, suala hili ni changamoto kwa nchi zote wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho,naomba nikushukuru sana wewe kwa uongozi wako mahiri na kwa kunipa ruhusa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati, niwashukuru pia Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote Mheshimiwa Spika mwenyewe ambaye ni jemedari wetu wa Bunge lako Tukufu katika kuratibu na kusimamia shughuli za Bunge kwa umakini na umahiri. *(Makofi)*

Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na mazingira, Mheshimiwa January Makamba Mbunge, Makatibu wakuu pamoja na wataalamu wote wa Ofisi hii muhimu kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kujadili Azimio hili bila kumsahau Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Luhaga Mpina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa napenda kuwashukuru wajumbe wote wa kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kupitia na kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni yake juu ya azimio hili mbele ya Bunge hili Tukufu,orodha yao ipo hapo ni ndefu naomba nisiisome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi Bwana Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Bwana Alfred Magova na Bi. Zainabu Mkamba na Msaidizi wa Kamati Bi. Pauline Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati. Naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

# MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU AZIMIO LA BUNGE KURIDHIA ITIFAKI YA NAGOYA YA KUSIMAMIA UPATIKANAJI WA MGAWANYO SAHIHI WA FAIDA ZITOKANAZO NA MATUMIZI YA RASILIMALI ZA KIJENETIKI - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

(*Nagoya Protocol on Access to Genetic Resources and the Fair and Equitable Sharing of Benefits Arising from their Utilization to the Convention on Biological Diversity*)

---

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kabla sijasoma Taarifa hii naomba kufanya marekebisho katika nakala za hotuba yangu walizogawiwa Waheshimiwa Wabunge kwa kuondoa maneno "**Mkataba wa Nyongeza",** na badala yake kuweka neno **Itifaki**. Naomba Taarifa yangu yote pamoja na marekebisho yake, iingie kwenye kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b), naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Nagoya ya kusimamia Upatikanaji wa Mgawanyo sahihi wa faida zitokonazo na Matumizi ya Rasilimali za Kijenetiki (*Nagoya Protocal on Access to Genetic Resources and the Fair and Equitable Sharing of Benefits arising from their utilization to the Convention on Biological Diversity*).

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya fasili ya 6(b), Kifungu cha 53 ikisomwa pamoja na fasili ya 1(b) ya Kifungu cha 7, Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira inalo jukumu la kushughulikia Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyochini ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Hoja ya Serikali kuhusu Bunge kuridhia Itifaki ya Nagoya ya kusimamia Upatikanaji wa

Mgawanyo sahihi wa faida zitokonazo na Matumizi ya Rasilimali za Kijenetiki (*Nagoya Protocal on Access to Genetic Resouces and the Fair and Equitable Sharing of Benefits arising from their utilization to the Convention on Biological Diversity*) ililetwa kwenye Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (3) ya Kanuni za Bunge.

## 2.0 CHIMBUKO LA MKATABA WA NYONGEZA

**Mhesimiwa Spika,** chimbuko na asili la Itifaki hii ni miongoni mwa mambo muhimu katika kuridhia. Imeelezwa kuwa Mkataba wa Bioanuai wa Mwaka 1992, una Itifaki tatu ambazo ni **Itifaki ya Cartagena ya mwaka 2000** inayohusu Usimamizi wa Mazingira Dhidi ya Athari zinaweza kutokea kutokana na Matumizi ya Biotekinolojia ya kisasa; **Itifaki ya kusimamia upatikanaji na mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali asili za kiejenetiki;** na **Itifaki ya ziada ya Nagoya – Kuala Lumpur** kuhusu uwajibikaji kisheria na fidia katika kutekeleza Itifaki ya Cartagena.

**Mheshimiwa Spika**, mkutano wa sita (6) wa nchi wanachama wa Mkataba wa Bioanuai uliofanyika Johannesburg, Afrika ya Kusini mwaka 2002, ulibaini kusuasaua katika utekelezaji wa lengo la tatu la Mkataba huu. Lengo hili linahusu mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali za kijenetiki. Kutofikiwa kwa Lengo hili kunatokana na kutokuwepo mfumo rasmi wa usimamizi rasimali za kijenetiki.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mkutano huo ilikubaliwa kuanzisha Itifaki kwa ajilli ya kusimamia rasilimali hizi. Mchakato huo ulihusisha majadiliano yaliyofanyika katika mikutano tisa kuanzia 2002 hadi 2010. Itifaki inayopendekezwa ilipitishwa na nchi wanachama katika mkutano wa kumi uliofanyika Nagoya, Japani mwaka 2010.

## 3.0 NAMNA KAMATI ILIVYOSHUGHULIKIA HOJA HII

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 14 Juni, 2017 Kamati ilikutana katika  na kupata maelezo ya Serikali kuhusu pendekezo la

kuridhia Itifaki ya Nagoya ya kusimamia Upatikanaji wa Mgawanyo sahihi wa faida zitokonazo na Matumizi ya Rasilimali za Kijenetiki (*Nagoya Protocal on Access to Genetic Resouces and the Fair and Equitable Sharing of Benefits arising from their utilization to the Convention on Biological Diversity*). Aidha, tarehe 18 Juni, 2017 Ofisi ya Bunge kupitia Mradi wa LSP iliiwezesha Kamati kupata uelewa na stadi muhimu kuhusu Utaratibu wa Bunge kuridhia Mikataba na Itifaki mbalimbali za Kimataifa. Uelewa huu uliisaidia Kamati kuwa katika nafasi nzuri ya kuifanyia kazi hoja hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipotekeleza jukumu lake kuhusiana na hoja hii, ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117 (8) na 117 (9) kuhusu utaratibu wa Kamati pamoja na kuwaalika wadau. Katika hatua hii, Kamati iliwaalika wataalamu kutoka asasi za Serikali, asasi za kiraia (AZISE) na wadau wengine kwa ajili ya kupata maoni yao. Kamati inawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao kuhusu itifaki hii. Aidha, Kamati inawashukuru sana Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia Taasisi ya Sayansi za Bahari ambao wametoa maoni kadhaa yaliyosaidia kuboresha maoni ya Kamati kuhusu itifaki hii.

## 4.0 MAMBO YA MSINGI YALIYOZINGATIWA NA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (e), Kamati ilizingatia mambo mbalimbali muhimu katika kuifanyia kazi hoja ya Serikali iliyomezani leo. Mambo hayo ni pamoja na kuangalia Katiba ya Jamhuri ya Mungano, baadhi ya sheria za nchi zinazohusiana moja kwa moja na maudhui ya Itifaki inayopendekezwa, uzoefu wa nchi nyingine katika masuala muhimu ya Itifaki hii pamoja na kutafakari kuhusu hasara au faida na kiwango cha manufaa au madhara yanayoweza kupatikana kwa kuridhia au kutokuridhia Itifaki hii kama ulivyo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na maelezo ya Mtoa hoja, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu hali iliyofikiwa katika Mkataba huu kwa kuangalia kama una nguvu ya kisheria

na kubaini kuwa **Ibara ya 32** ya Itifaki, Ibara hii iliweka wazi Itifaki kwa ajili ya kusainiwa na Nchi Wanachama wa Mkataba kwenye Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa, New York kuanzia terehe 2 Februari, 2011 hadi 1 Februari, 2012.

**Nanukuu***: **Article 32** "This Protocal shall be open for signature by paties to the Convention at the United Nations Headquarters in New York, from 2 February 2011 to 1 February 2012* **Mwisho wa kunukuu***.*

Utekelezaji wa Itifaki hii ulianza terehe 29 Octoba, 2014 baada ya Nchi Wanacama 50 kuridhia. Hii ni kwa mujibu wa **Ibara ya 33 (1-3)** ya Itifaki ambayo inaeleza kuwa utekelezaji wa Itifaki utaanza siku ya kumi na tisa (19) mara baada ya nchi mwanachama ya hamsini (50) kuwasilisha hati ya kuridhia.

**Nanukuu***: **Article 33 (1) "**This convention shall enter into force on the ninetieth day following the date of the deposit of the fiftieth instrument of ratification, acceptance, approval or accession of the state or regional economic integration organizations that are Parties to the Convention".* **Mwisho wa kunukuu***.*

Aidha, hadi kufikia Mei, 2016 nchi Wanachama 72 zilikuwa zimekwisha ridhia Itifaki hii. Tanzania itaridhia Itifaki hii kwa kuzingatia Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1997.

Kwa mujibu wa **Ibara ya 35** ya Itifaki hii inaruhusu Nchi Mwanachama kujitoa katika Itifaki, ambapo imeeleza kuwa, muda wowote baada ya miaka miwili tangu Itifaki imeanza kutekelezwa, nchi hiyo inaweza kujitoa kwenye Itifaki kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa mtunza nyaraka zinazohusiana na uridhiaji Itifaki hii.

**Nanukuu: Mfano, *Article 35*** "At any time after two years from the date on which this Protocol has entered into force for a Party, that Party may withdraw from this protocol by giving written notification to the Depositary " **Mwisho wa kunukuu***.*

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Mikataba mbalimbali ya Kimataifa, Kamati ilizingatia kipengele cha Itifaki hii kuhusu ushikikiano wetu na mkiataba mingine. **Ibara ya 4** ya Itifaki inaeleza uhusiano kati ya Mkataba na Mikataba mingine ya kimataifa, kwamba masharti ya Itifaki hayatakinzana na haki na wajibu wa Nchi yoyote mwanachama anazozipata na kutokana na Mikataba mingine ya Kimataifa, isipokuwa pale ambapo utekelezaji wa haki na wajibu wa Mikataba hiyo mingine itasababisha hasara kubwa kwa Viumbe hai. Itifaki hii hailengi kuweka madaraja kati ya Mkataba huu na Mikataba mingine ya kimatafa.

**Nanukuu: Mfano, *Article 4*** "The provision of this Protocol shall not affect the right and obligation of any Party deriving from any existing international agreement, except where the exercise of those rights and obligations would cause a serious damage or threat to biological deversity" **Mwisho wa kunukuu**.

**Mheshimiwa Spika**, Mkataba wa Msingi kuhusu Mikataba ya Kimataifa ni Mkataba wa Viena ambao Tanzania iliuridhia Mkataba mwaka 1976. Mkataba wa **Viena** umeweka kanuni za msingi kuhusu uridhiaji wa mikataba ya kimataifa. Kanuni hizo muhimu zilizingatiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira wakati wa kuifanyia kazi hoja iliyopo mbele ya Bunge hili kwa sasa.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spiaka,** Lengo kuu la Itifaki hii ni kuimarisha ushirikiano wa haki na wa usawa juu ya faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali za kijenetiki, ikiwa ni pamoja na upatikanaji sahihi wa rasilimali hiyo, ikiwepo upatikanaji na uhamishaji wa teknolojia husika, na kwa ufadhili wa kifedha unaokubalika, hivyo basi kuchangia uhifadhi wa bioanuai na matumizi endelevu ya rasilimali zitokanazo kwayo. Lakini hili litafikiwa tu ikiwa utekelezaji wa kikamilifu na wa haki wa vipengele mbali mbali vilivyomo kwenye Itifaki hiyo utafanyika.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuipitia Itifaki hii imeonekana inahakikisha ulinzi na udhibiti wa kutosha wa rasilimali za kijenetiki zetu. Hata hivyo, ili Taifa linufaike ipasavyo na fursa zitokanazo na uanachama wa Itifaki hii ya Mkataba wa Bioanuai kwa ujumla wake mambo kadhaa yanapendekezwa kufanyika:

**Mheshimiwa Spika**, Itifaki inaopendekezwa inatoa fursa muhimu ya kuheshimiwa na kuzingatiwa masharti na matakwa ya sheria za ndani za nchi mwanachama husika, kwenye makubaliano yoyote ya utoaji/ubadilishanaji wa rasilimali za kijenetiki na mfumo wa ugawanaji wa faidi zitokanazo na matumizi ya rasilimali hiyo. Hivyo basi, Kamati inashauri kwamba Sheria za nchi ziimarishwe ili kutoa udhibiti wa kutosha wa rasilimali hiyo, ili kuhakikishwa kwamba Taifa linanufaika ipasavyo na rasilimali hiyo;

**Mheshimiwa Spika**, Itifaki inapendekeza kwamba upatikanaji na matumizi ya Ujuzi Jadi, an mgawanyo wa faida itokanayo na matumizi ya ujuzi huo, ufanyike kwa makubaliano kati jamii za jadi husika na mtumiaji (muhitaji). Kamati inashauri Serikali kuandaa mfumo madhubuti wa kisheria na kiutendaji kuhakikisha kwamba inajihusisha kikamilifu katika mazungumzo na makubaliano yoyote yakayofanyika kati ya pande hizo mbili ili kulinda maslahi ya nchi;

**Mheshimiwa Spika**, Itifaki haijatoa ukomo wa aina wala kiwango cha fidia anayotakiwa kupata mmiliki wa rasilimali hizi kwa matumizi (yakiwemo ya kibiashara) yatokanayo na rasilimali hiyo. Ni maoni ya Kamati kuwa mapendekezo haya yanaweza kutumiwa vibaya na watumiaji wa rasilimali hii, kwa kuamua kwa makusudi kulipa fidia isiyostahiki kwa mmiliki wa rasilimali. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu utakaoainisha aina na kiwango cha fidia kulinga na aina ya raslimali hiyo na matumizi yake;

**Mheshimiwa Spika,** Itifaki inapendekeza fursa ya ujenzi na uendelezaji wa uwezo wa rasilimali watu na wa kitaasisi kwenye Nyanja ya uhifadhi na usimamizi wa bioanuai na rasilimali kijenetiki. Kamati inaishauri Serikali kuweka mfumo

mzuri utakaohakikisha kuwa fursa hiyo inatumiwa ipasavyo kwa manufaa ya nchi, ikiwemo kuainisha vipaumbele vyetu kwenye nyanja mbalimbali;

**Mheshimiwa Spika,** Itifaki inapendekeza uwepo wa wataalamu na Taasisi/mamlaka maalum ya kitaifa (Competent National Authority) kwa kila nchi mwanachama itakayokuwa kitovu (focalpoint) cha utekelezaji wa shughuli za Itifaki. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inatumia umakini mkubwa kwenye uteuzi wa wataalamu na taasisi hiyo (hizo), ili kuhakikisha kwamba maslahi ya taifa yanalindwa kuhusiana na ubadilishanaji wa rasilimali za kijenetiki, ikikumbukwa kwamba taasisi hiyo itakuwa na mamlaka ya kuidhinisha ubadilishanaji wa rasilimali hiyo kwa niaba ya Serikali;

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na uporaji wa rasilimali za kijenetiki katika nchi hii kwa kisingizio cha utafiti, watafiti hawa huwashirikisha wazawa katika hatua za mwanzo kwa nia ya kujua baadhi ya rasilimali za kijenetihi hususani mizizi, majani, mbegu au magamba ya miti ambayo inatibu baadhi ya magonjwa. Wageni wamenufaika sana na rasilimali za kijenetiki kwa kujipatia ujuzi wa asili kutoka kwenye jamii zetu bila malipo huku wao wakijinufaisha na rasilimali zetu. Kamati inaishauri Serikali kubainisha maeneo yote yenye rasilimali hizi na kuyawekea utaratibu wa uvunaji. Jambo hili la kubaini maeneo liende sambamba na utoaji wa elimu kwa jamii juu ya matumkizi na faida zitakazopatikana kama rasilimali zetu zikitumika kwa kuzingatia utaratibu maalumu; na

**Mheshimwa Spika,** kumekuwepo na ucheleweshaji katika kuridhia Itifaki na Mikataba mbalimbali ya Kimataifa. Mfano ni Itifaki ya Nagoya iliyosainiwa tangu Oktoba, 2010, mpaka sasa Juni 2017, takribani miaka minane(8). Kamati inaishauri serikali kuwasilisha Bungeni kwa wakati Mikataba yote ya kimaifa pindi inaposainiwa.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nikushukuru sana wewe kwa uongozi wako mahiri na kwa kunipa ruhusa ya kuwasilisha

maoni haya ya Kamati. Niwashukuru pia Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia shughuli za Bunge kwa umakini na umahiri.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira Mhe. January Makamba(Mb), Naibu Waziri wake Mhe. Luhaga Joelson Mpina(Mb), Makatibu Wakuu, pamoja na wataalamu wote wa Ofisi hii muhimu kwa ushirikiani walioutoa wakati wa kujadili Azimio hili.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kupitia kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni yake juu ya Azimio hili mbele ya Bunge hili tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini na kwa ruhsa yako naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge.

| | |
|---|---|
| (i) Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo Mb | Mwenyekiti |
| (ii) Mhe. Vicky Passcal Kamata, Mb | Mjumbe |
| (iii) Mhe. Salim Hassan Turky, Mb | Mjumbe |
| (iv) Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb | Mjumbe |
| (v) Mhe Dkt. Dalaly Peter Kafumu | Mjumbe |
| (vi) Mhe. Khatib Said Haji, Mb | Mjumbe |
| (vii) Mhe. Tauhida Cassian Gallos, Mb | Mjumbe |
| (viii) Mhe. Munira Mustafa Khaibu, Mb | Mjumbe |
| (ix) Mhe. Anthony Calist Komu, Mb | Mjumbe |
| (x) Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb | Mjumbe |
| (xi) Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa,Mb | Mjumbe |
| (xii) Mhe. Lameck Okambo Airo, Mb | Mjumbe |
| (xiii) Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb | Mjumbe |
| (xiv) Mhe. Balozi Dkt Diodorus Kamala, Mb | Mjumbe |
| (xv) Mhe. Jesca David Kishoa, Mb | Mjumbe |
| (xvi) Mhe. Mbarouk Salim Ali, Mb | Mjumbe |
| (xvii) Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb | Mjumbe |
| (xviii) Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest, Mb | Mjumbe |
| (xix) Mhe. Faida Mohammed Bakar, Mb | Mjumbe |
| (xx) Mhe. Suleiman Ahmed Sadick, Mb | Mjumbe |

| | |
|---|---|
| (xxi) Mhe Ibrahim Hassanali Raza, Mb | Mjumbe |
| (xxii) Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb | Mjumbe |
| (xxiii) Mhe. Dkt. Raphael MMasunga Chegeni, Mb | Mjumbe |
| (xxiv) Mhe. Sylvestry Francis koka, Mb | Mjumbe |
| (xxv) Mhe. Gimbi Dotto Massaba, Mb | Mjumbe |
| (xxvi) Mhe. Martha Mosses Mlata, Mb | Mjumbe |
| (xxvii) Mhe. Joyce John Mukya, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Athumani Hussein; Mkurugenzi msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi Bw. Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati Bw. Wilfred Magova na Bi. Zainab Mkamba na Msaidizi wa Kamati Bi Paulina Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio.

Stanslaus Haroon Nyongo, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA**
29 Juni, 2017

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chegeni, Waheshimiwa kuna tangazo dogo kikao cha *caucus* cha Wabunge wote wa CCM, leo kutakuwa na kikao cha *caucus* Alhamisi tarehe 29 saa 12.00 jioni, *White House* Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi mnaombwa kuhudhuria na mahudhurio yatazingatiwa.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa kamati naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge kuridhia itifaki ya Nagoya ya kusimamia upatikanaji wa

mgawanyo sahihi ya faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali za kijenetiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda sitapenda kuwashukuru ila sitajikita kwenye maoni ya Kamati, maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu la itifaki hii ni kuimarisha ushirikiano wa haki na usawa juu ya faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali ya kijenetiki ikiwa ni pamoja na upatikanaji sahihi wa rasilimali hiyo, ikiwepo upatikanaji wa uhamasishaji na teknolojia husika na kwa ufadhili wa kifedha uliokubalika hivyo basi kuchangia hifadhi na bionuai na matumizi endelevu ya rasilimali zitokanazo na kwayo. Lakini hili litafikiwa ikiwa utekelezaji wa kikamilifu na uhakika wa vipengele mbalimbali vilivyomo kwenye itifaki hiyo utafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia itifaki hii imeonekana inahakikisha ulinzi na udhibiti wa kutosha wa rasilimali wa kijenetiki zetu, hata hivyo ili Taifa linufaike ipasavyo na fursa hizi zifuatazo na wanachama wa itifaki hii pamoja na mkataba wa bionuai kwa ujumla wake mambo kadhaa yanapendekezwa kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itifaki inayopendekezwa inatoa fursa muhimu ya kuheshimiwa na kuzingatiwa masharti na matakwa ya sheria ya ndani ya nchi mwanachama husika kwenye makubaliano yote ya utoaji, ubadilishaji wa rasilimali wa kijenetiki na mfumo wa ugawaji wa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali hiyo. Hivyo basi Kamati inashauri kwamba sheria za nchi ziimarishwe ili kutoa udhibiti wa kutosha wa rasilimali hiyo ili kuhakikisha kwamba Taifa linanufaika ipasavyo na rasilimali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itifaki inapendekeza kwamba upatikanaji wa matumizi ya ujuzi jadi na mgawanyo wa faida itokanayo na matumizi ya ujuzi huo ufanyike kwa makubaliano kati ya jamii za jadi husika na mtumiaji au muhitaji. Kamati inashauri Serikali kuandaa mfumo

madhubuti wa kisheria na kiutendaji kuhaikisha kwamba inajihusisha kikamilifu katika mazungumzo na makubaliano yote yatakayofanyika katika pande hizi mbili ili kulinda maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itifaki haijatoa ukomo wa aina wala kiwango cha fidia itayotakiwa kupata mmiliki wa rasilimali hizi kwa matumizi yakiwemo ya kibiashara yatokanayo na rasilimali hiyo. Ni maoni ya Kamati kuwa mapendekezo haya yanaweza kutumiwa vibaya na watumiaji wa rasilimali hii kwa kuamua kwa makusudi kulipa fidia isiyostahiki kwa mmiliki wa rasilimali. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu utakaoainisha aina na kiwango cha fidia kulingana na aina ya rasilimali hiyo na matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itifaki inapendekeza fursa ya ujenzi na utekelezaji wa uendelezaji wa uwezo wa rasilimali watu na wa kitaasisi kwenye nyanja ya uhifadhi na usimamizi wa manuai na rasilimali kijenetiki. Kamati inaishauri Serikali kuweka mfumo mzuri utaohakikisha kuwa fursa hiyo inatumiwa ipasavyo kwa manufaa ya nchi ikiwemo kuainisha vipaumbele vyetu kwenye nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itifaki inapendekeza uwepo wataalam na taasisi au mamlaka maalum ya kitaifa, *(Competent National Authority)* kwa kila nchi mwanachama itakayokuwa kitovu *(folk point)* cha utekelezaji shughuli za itifaki. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inatumia umakini mkubwa kwenye uteuzi wa wataalam na taasisi hiyo au hizo au kuhakikisha kwamba maslahi ya Taifa yanalindwa kuhusiana na ubadilishanaji wa rasilimali za kijenetiki ikikumbukwa kwamba taasisi hiyo itakuwa na mamlaka ya kuidhinisha ubadilishaji wa rasilimali hiyo kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na uporaji wa rasilimali za kijenetiki katika nchi hii kwa kisingizio cha utafiti, watafiti hawa hawashirikishi wazawa katika hatua za

mwanzo kwa nia ya kujua baadhi ya rasilimali za kijenetiki hususani mizizi, majani, mbegu au magamba ya miti ambayo inatibu baadhi ya magonjwa, wageni wamenufaika sana na rasilimali ya kijenetiki kwa kujipatia ujuzi wa asili kutoka kwenye jamii zetu bila malipo huku wao wakijinufaisha kwa rasilimali zetu. Kamati inaishauri Serikali kubainisha maeneo yote yenye rasilimali hizi na kuyawekea utaratibu wa uvunaji. Jambo hili la kubaini maeneo liende sambamba na utoaji wa elimu kwa jamii juu ya matumizi na faida zitakazopatikana kama rasilimali zetu zikitumika kuzingatia utaratibu maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo ucheleweshaji katika kuridhia itifaki na mikataba mbalimbali ya kimataifa, mfano ni itifaki ya Nagoya iliyosainiwa tangu Oktoba, 2010 mpaka sasa 2017 takribani miaka minane. Kamati inashauri Serikali kuwasilisha Bungeni kwa wakati mikataba yote ya kimataifa pindi inaposainiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nikushukuru wewe na uongozi wote mahiri wa Bunge, vilevile naomba niwashukuru sana Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Mheshimiwa January Makamba, Naibu wake Mheshimiwa Luhaga Mpina, Makatibu wakuu pamoja na wataalam wote wa ofisi hii muhimu kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa kamati kama ambavyo wameorodheshwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante.

# MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU AZIMIO LA BUNGE KURIDHIA ITIFAKI YA NAGOYA YA KUSIMAMIA UPATIKANAJI WA MGAWANYO SAHIHI WA FAIDA ZITOKANAZO NA MATUMIZI YA RASILIMALI ZA KIJENETIKI

*(Nagoya Protocol on Access to Genetic Resources and the Fair and Equitable Sharing of Benefits Arising from their Utilization to the Convention on Biological Diversity*)

---

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kabla sijasoma Taarifa hii naomba kufanya marekebisho katika nakala za hotuba yangu walizogawiwa Waheshimiwa Wabunge kwa kuondoa maneno "**Mkataba wa Nyongeza",** na badala yake kuweka neno **Itifaki**. Naomba Taarifa yangu yote pamoja na marekebisho yake, iingie kwenye kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b), naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Nagoya ya kusimamia Upatikanaji wa Mgawanyo sahihi wa faida zitokonazo na Matumizi ya Rasilimali za Kijenetiki (*Nagoya Protocal on Access to Genetic Resources and the Fair and Equitable Sharing of Benefits arising from their utilization to the Convention on Biological Diversity*).

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya fasili ya 6(b), Kifungu cha 53 ikisomwa pamoja na fasili ya 1(b) ya Kifungu cha 7, Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira inalo jukumu la kushughulikia Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyochini ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Hoja ya Serikali kuhusu Bunge kuridhia Itifaki ya Nagoya ya kusimamia Upatikanaji wa Mgawanyo sahihi wa faida zitokonazo na Matumizi ya

Rasilimali za Kijenetiki (*Nagoya Protocal on Access to Genetic Resouces and the Fair and Equitable Sharing of Benefits arising from their utilization to the Convention on Biological Diversity*) ililetwa kwenye Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (3) ya Kanuni za Bunge.

## 2.0 CHIMBUKO LA MKATABA WA NYONGEZA

**Mhesimiwa Spika,** chimbuko na asili la Itifaki hii ni miongoni mwa mambo muhimu katika kuridhia. Imeelezwa kuwa Mkataba wa Bioanuai wa Mwaka 1992, una Itifaki tatu ambazo ni **Itifaki ya Cartagena ya mwaka 2000** inayohusu Usimamizi wa Mazingira Dhidi ya Athari zinaweza kutokea kutokana na Matumizi ya Biotekinolojia ya kisasa; **Itifaki ya kusimamia upatikanaji na mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali asili za kiejenetiki;** na **Itifaki ya ziada ya Nagoya – Kuala Lumpur** kuhusu uwajibikaji kisheria na fidia katika kutekeleza Itifaki ya Cartagena.

**Mheshimiwa Spika**, mkutano wa sita (6) wa nchi wanachama wa Mkataba wa Bioanuai uliofanyika Johannesburg, Afrika ya Kusini mwaka 2002, ulibaini kusuasaua katika utekelezaji wa lengo la tatu la Mkataba huu. Lengo hili linahusu mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali za kijenetiki. Kutofikiwa kwa Lengo hili kunatokana na kutokuwepo mfumo rasmi wa usimamizi rasimali za kijenetiki.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mkutano huo ilikubaliwa kuanzisha Itifaki kwa ajilli ya kusimamia rasilimali hizi. Mchakato huo ulihusisha majadiliano yaliyofanyika katika mikutano tisa kuanzia 2002 hadi 2010. Itifaki inayopendekezwa ilipitishwa na nchi wanachama katika mkutano wa kumi uliofanyika Nagoya, Japani mwaka 2010.

## 3.0 NAMNA KAMATI ILIVYOSHUGHULIKIA HOJA HII

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 14 Juni, 2017 Kamati ilikutana katika na kupata maelezo ya Serikali kuhusu pendekezo la

kuridhia Itifaki ya Nagoya ya kusimamia Upatikanaji wa Mgawanyo sahihi wa faida zitokonazo na Matumizi ya Rasilimali za Kijenetiki (*Nagoya Protocal on Access to Genetic Resouces and the Fair and Equitable Sharing of Benefits arising from their utilization to the Convention on Biological Diversity*). Aidha, tarehe 18 Juni, 2017 Ofisi ya Bunge kupitia Mradi wa LSP iliiwezesha Kamati kupata uelewa na stadi muhimu kuhusu Utaratibu wa Bunge kuridhia Mikataba na Itifaki mbalimbali za Kimataifa. Uelewa huu uliisaidia Kamati kuwa katika nafasi nzuri ya kuifanyia kazi hoja hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipotekeleza jukumu lake kuhusiana na hoja hii, ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117 (8) na 117 (9) kuhusu utaratibu wa Kamati pamoja na kuwaalika wadau. Katika hatua hii, Kamati iliwaalika wataalamu kutoka asasi za Serikali, asasi za kiraia (AZISE) na wadau wengine kwa ajili ya kupata maoni yao. Kamati inawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao kuhusu itifaki hii. Aidha, Kamati inawashukuru sana Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia Taasisi ya Sayansi za Bahari ambao wametoa maoni kadhaa yaliyosaidia kuboresha maoni ya Kamati kuhusu itifaki hii.

## 4.0 MAMBO YA MSINGI YALIYOZINGATIWA NA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (e), Kamati ilizingatia mambo mbalimbali muhimu katika kuifanyia kazi hoja ya Serikali iliyomezani leo. Mambo hayo ni pamoja na kuangalia Katiba ya Jamhuri ya Mungano, baadhi ya sheria za nchi zinazohusiana moja kwa moja na maudhui ya Itifaki inayopendekezwa, uzoefu wa nchi nyingine katika masuala muhimu ya Itifaki hii pamoja na kutafakari kuhusu hasara au faida na kiwango cha manufaa au madhara yanayoweza kupatikana kwa kuridhia au kutokuridhia Itifaki hii kama ulivyo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na maelezo ya Mtoa hoja, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu hali iliyofikiwa katika Mkataba huu kwa kuangalia kama una nguvu ya kisheria

na kubaini kuwa **Ibara ya 32** ya Itifaki, Ibara hii iliweka wazi Itifaki kwa ajili ya kusainiwa na Nchi Wanachama wa Mkataba kwenye Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa, New York kuanzia terehe 2 Februari, 2011 hadi 1 Februari, 2012.

**Nanukuu***: **Article 32** "This Protocal shall be open for signature by paties to the Convention at the United Nations Headquarters in New York, from 2 February 2011 to 1 February 2012* **Mwisho wa kunukuu***.*

Utekelezaji wa Itifaki hii ulianza terehe 29 Octoba, 2014 baada ya Nchi Wanacama 50 kuridhia. Hii ni kwa mujibu wa **Ibara ya 33 (1-3)** ya Itifaki ambayo inaeleza kuwa utekelezaji wa Itifaki utaanza siku ya kumi na tisa (19) mara baada ya nchi mwanachama ya hamsini (50) kuwasilisha hati ya kuridhia.

**Nanukuu***: **Article 33 (1) "**This convention shall enter into force on the ninetieth day following the date of the deposit of the fiftieth instrument of ratification, acceptance, approval or accession of the state or regional economic integration organizations that are Parties to the Convention".* **Mwisho wa kunukuu***.*

Aidha, hadi kufikia Mei, 2016 nchi Wanachama 72 zilikuwa zimekwisha ridhia Itifaki hii. Tanzania itaridhia Itifaki hii kwa kuzingatia Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1997.

Kwa mujibu wa **Ibara ya 35** ya Itifaki hii inaruhusu Nchi Mwanachama kujitoa katika Itifaki, ambapo imeeleza kuwa, muda wowote baada ya miaka miwili tangu Itifaki imeanza kutekelezwa, nchi hiyo inaweza kujitoa kwenye Itifaki kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa mtunza nyaraka zinazohusiana na uridhiaji Itifaki hii.

**Nanukuu: Mfano, *Article 35*** "At any time after two years from the date on which this Protocol has entered into force for a Party, that Party may withdraw from this protocol by giving written notification to the Depositary " **Mwisho wa kunukuu***.*

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Mikataba mbalimbali ya Kimataifa, Kamati ilizingatia kipengele cha Itifaki hii kuhusu ushikikiano wetu na mkiataba mingine. **Ibara ya 4** ya Itifaki inaeleza uhusiano kati ya Mkataba na Mikataba mingine ya kimataifa, kwamba masharti ya Itifaki hayatakinzana na haki na wajibu wa Nchi yoyote mwanachama anazozipata na kutokana na Mikataba mingine ya Kimataifa, isipokuwa pale ambapo utekelezaji wa haki na wajibu wa Mikataba hiyo mingine itasababisha hasara kubwa kwa Viumbe hai. Itifaki hii hailengi kuweka madaraja kati ya Mkataba huu na Mikataba mingine ya kimatafa.

**Nanukuu: Mfano, *Article 4*** "The provision of this Protocol shall not affect the right and obligation of any Party deriving from any existing international agreement, except where the exercise of those rights and obligations would cause a serious damage or threat to biological deversity" **Mwisho wa kunukuu***.*

**Mheshimiwa Spika**, Mkataba wa Msingi kuhusu Mikataba ya Kimataifa ni Mkataba wa Viena ambao Tanzania iliuridhia Mkataba mwaka 1976. Mkataba wa **Viena** umeweka kanuni za msingi kuhusu uridhiaji wa mikataba ya kimataifa. Kanuni hizo muhimu zilizingatiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira wakati wa kuifanyia kazi hoja iliyopo mbele ya Bunge hili kwa sasa.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spiaka,** Lengo kuu la Itifaki hii ni kuimarisha ushirikiano wa haki na wa usawa juu ya faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali za kijenetiki, ikiwa ni pamoja na upatikanaji sahihi wa rasilimali hiyo, ikiwepo upatikanaji na uhamishaji wa teknolojia husika, na kwa ufadhili wa kifedha unaokubalika, hivyo basi kuchangia uhifadhi wa bioanuai na matumizi endelevu ya rasilimali zitokanazo kwayo. Lakini hili litafikiwa tu ikiwa utekelezaji wa kikamilifu na wa haki wa vipengele mbali mbali vilivyomo kwenye Itifaki hiyo utafanyika.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuipitia Itifaki hii imeonekana inahakikisha ulinzi na udhibiti wa kutosha wa rasilimali za kijenetiki zetu. Hata hivyo, ili Taifa linufaike ipasavyo na fursa zitokanazo na uanachama wa Itifaki hii ya Mkataba wa Bioanuai kwa ujumla wake mambo kadhaa yanapendekezwa kufanyika:

**Mheshimiwa Spika**, Itifaki inaopendekezwa inatoa fursa muhimu ya kuheshimiwa na kuzingatiwa masharti na matakwa ya sheria za ndani za nchi mwanachama husika, kwenye makubaliano yoyote ya utoaji/ubadilishanaji wa rasilimali za kijenetiki na mfumo wa ugawanaji wa faidi zitokanazo na matumizi ya rasilimali hiyo. Hivyo basi, Kamati inashauri kwamba Sheria za nchi ziimarishwe ili kutoa udhibiti wa kutosha wa rasilimali hiyo, ili kuhakikishwa kwamba Taifa linanufaika ipasavyo na rasilimali hiyo;

**Mheshimiwa Spika**, Itifaki inapendekeza kwamba upatikanaji na matumizi ya Ujuzi Jadi, an mgawanyo wa faida itokanayo na matumizi ya ujuzi huo, ufanyike kwa makubaliano kati jamii za jadi husika na mtumiaji (muhitaji). Kamati inashauri Serikali kuandaa mfumo madhubuti wa kisheria na kiutendaji kuhakikisha kwamba inajihusisha kikamilifu katika mazungumzo na makubaliano yoyote yakayofanyika kati ya pande hizo mbili ili kulinda maslahi ya nchi;

**Mheshimiwa Spika**, Itifaki haijatoa ukomo wa aina wala kiwango cha fidia anayotakiwa kupata mmiliki wa rasilimali hizi kwa matumizi (yakiwemo ya kibiashara) yatokanayo na rasilimali hiyo. Ni maoni ya Kamati kuwa mapendekezo haya yanaweza kutumiwa vibaya na watumiaji wa rasilimali hii, kwa kuamua kwa makusudi kulipa fidia isiyostahiki kwa mmiliki wa rasilimali. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu utakaoainisha aina na kiwango cha fidia kulinga na aina ya raslimali hiyo na matumizi yake;

**Mheshimiwa Spika,** Itifaki inapendekeza fursa ya ujenzi na uendelezaji wa uwezo wa rasilimali watu na wa kitaasisi kwenye Nyanja ya uhifadhi na usimamizi wa bioanuai na rasilimali kijenetiki.

Kamati inaishauri Serikali kuweka mfumo mzuri utakaohakikisha kuwa fursa hiyo inatumiwa ipasavyo kwa manufaa ya nchi, ikiwemo kuainisha vipaumbele vyetu kwenye nyanja mbalimbali;

**Mheshimiwa Spika,** Itifaki inapendekeza uwepo wa wataalamu na Taasisi/mamlaka maalum ya kitaifa (Competent National Authority) kwa kila nchi mwanachama itakayokuwa kitovu (focalpoint) cha utekelezaji wa shughuli za Itifaki. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inatumia umakini mkubwa kwenye uteuzi wa wataalamu na taasisi hiyo (hizo), ili kuhakikisha kwamba maslahi ya taifa yanalindwa kuhusiana na ubadilishanaji wa rasilimali za kijenetiki, ikikumbukwa kwamba taasisi hiyo itakuwa na mamlaka ya kuidhinisha ubadilishanaji wa rasilimali hiyo kwa niaba ya Serikali;

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na uporaji wa rasilimali za kijenetiki katika nchi hii kwa kisingizio cha utafiti, watafiti hawa huwashirikisha wazawa katika hatua za mwanzo kwa nia ya kujua baadhi ya rasilimali za kijenetihi hususani mizizi, majani, mbegu au magamba ya miti ambayo inatibu baadhi ya magonjwa. Wageni wamenufaika sana na rasilimali za kijenetiki kwa kujipatia ujuzi wa asili kutoka kwenye jamii zetu bila malipo huku wao wakijinufaisha na rasilimali zetu. Kamati inaishauri Serikali kubainisha maeneo yote yenye rasilimali hizi na kuyawekea utaratibu wa uvunaji. Jambo hili la kubaini maeneo liende sambamba na utoaji wa elimu kwa jamii juu ya matumkizi na faida zitakazopatikana kama rasilimali zetu zikitumika kwa kuzingatia utaratibu maalumu; na

**Mheshimwa Spika,** kumekuwepo na ucheleweshaji katika kuridhia Itifaki na Mikataba mbalimbali ya Kimataifa. Mfano ni Itifaki ya Nagoya iliyosainiwa tangu Oktoba, 2010, mpaka sasa Juni 2017, takribani miaka minane(8). Kamati inaishauri serikali kuwasilisha Bungeni kwa wakati Mikataba yote ya kimaifa pindi inaposainiwa.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nikushukuru sana wewe kwa uongozi wako mahiri na kwa kunipa ruhusa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati. Niwashukuru pia Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia shughuli za Bunge kwa umakini na umahiri.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira Mhe. January Makamba(Mb), Naibu Waziri wake Mhe. Luhaga Joelson Mpina(Mb), Makatibu Wakuu, pamoja na wataalamu wote wa Ofisi hii muhimu kwa ushirikiani walioutoa wakati wa kujadili Azimio hili.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kupitia kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni yake juu ya Azimio hili mbele ya Bunge hili tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini na kwa ruhsa yako naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge.

| | |
|---|---|
| (i) Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo Mb | Mwenyekiti |
| (ii) Mhe. Vicky Passcal Kamata, Mb | Mjumbe |
| (iii) Mhe. Salim Hassan Turky, Mb | Mjumbe |
| (iv) Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb | Mjumbe |
| (v) Mhe Dkt. Dalaly Peter Kafumu | Mjumbe |
| (vi) Mhe. Khatib Said Haji, Mb | Mjumbe |
| (vii) Mhe. Tauhida Cassian Gallos, Mb | Mjumbe |
| (viii) Mhe. Munira Mustafa Khaibu, Mb | Mjumbe |
| (ix) Mhe. Anthony Calist Komu, Mb | Mjumbe |
| (x) Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb | Mjumbe |
| (xi) Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa,Mb | Mjumbe |
| (xii) Mhe. Lameck Okambo Airo, Mb | Mjumbe |
| (xiii) Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb | Mjumbe |
| (xiv) Mhe. Balozi Dkt Diodorus Kamala, Mb | Mjumbe |
| (xv) Mhe. Jesca David Kishoa, Mb | Mjumbe |

| | |
|---|---|
| (xvi) Mhe. Mbarouk Salim Ali, Mb | Mjumbe |
| (xvii) Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb | Mjumbe |
| (xviii) Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest, Mb | Mjumbe |
| (xix) Mhe. Faida Mohammed Bakar, Mb | Mjumbe |
| (xx) Mhe. Suleiman Ahmed Sadick, Mb | Mjumbe |
| (xxi) Mhe Ibrahim Hassanali Raza, Mb | Mjumbe |
| (xxii) Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb | Mjumbe |
| (xxiii) Mhe. Dkt. Raphael MMasunga Chegeni, Mb | Mjumbe |
| (xxiv) Mhe. Sylvestry Francis koka, Mb | Mjumbe |
| (xxv) Mhe. Gimbi Dotto Massaba, Mb | Mjumbe |
| (xxvi) Mhe. Martha Mosses Mlata, Mb | Mjumbe |
| (xxvii) Mhe. Joyce John Mukya, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Athumani Hussein; Mkurugenzi msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi Bw. Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati Bw. Wilfred Magova na Bi. Zainab Mkamba na Msaidizi wa Kamati Bi Paulina Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio.

Stanslaus Haroon Nyongo, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA**
29 Juni, 2017

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msemaji Kambi ya Upinzani Dkt. Sware jiandae Mheshimiwa Gekul.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu kuridhia marekebisho ya mkataba wa Nairobi wa hifadhi, usimamizi na uendelezaji

wa mazingira ya bahari na ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Nairobi kuhusu Hifadhi Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Pwani ya Kanda ya Afrika Mashariki unalenga katika kusimamia mazingira ya Baharini na Ukanda wa Pwani. Tanzania ni nchi mwanachama kati ya nchi tisa zilizo katika Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Hindi kutoka mwaka 1996.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa moja ya majukumu ya mkataba huu kwa nchi mwanachama ni kutekeleza masharti ya mkataba huu *(the contracting parties shall cooperate in the formulation and adoption of protocols to facilitate the effective implementation of this convention).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali sasa ichukue hatua ya kutunga sheria mahususi ya kutekeleza hili ama kufanya marekebisho ya sheria ya mazingira *(Environmental Management Act)* ili kuendana sambamba na matakwa ya mkataba huu mfano, katika mkataba huu umeainisha Ibara ya 5, 6 na 9 kusimamia uchafuzi wa mazingira kutoka kwenye meli *(pollution from ships)* na utupaji taka baharini hovyo. Serikali inatakiwa kuchukua hatua mahususi ili kuhakikisha inadhibiti uchafuzi wa mazingira baharini kwa kuzingatia sheria za kimataifa. Hivyo basi, Serikali inatakiwa kukiwezesha Kitengo cha *Marine* chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ili kuweza kusimamia na kutekeleza sheria zake za utunzaji wa mazingira kama zipo.

(ii) Serikali itenge fedha mahususi kwa ajili ya udhibiti na usimamizi wa uharibifu wa mazingira kwa kuwezesha kifedha Baraza la Usimamizi wa Mazingira chini ya *NEMC* ili kuweza kusimamia na kudhibiti uharibifu wa mazingira katika sekta mbalimbali ili kuhakikisha madhara ya uharibifu wa

mazingira hayatokei katika bahari na Ukanda wa Pwani. Pia Serikali inabidi kuwezesha kifedha Mfuko wa Mazingira ulio chini ya Ofisi ya Makamu ya Rais, Muungano na Mazingira ili kuweza kusimamia utunzaji wa usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfano mwingine Katika Ibara ya 11 ya *convention* hii inataka kusimamia bionuai *(Biological Diversity).* Serikali inatakiwa kuhifadhi na kulinda bionuai viumbe adimu au vilivyo hatarini kutoweka, kuanzisha maeneo tengefu kama vile hifadhi za wanyamapori na misitu sanjari na kuzuia shughuli zinazoweza kusababisha uharibifu wa viumbe hao pamoja na maeneo hayo. Je, hili litatekelezwaje ili hali sekta muhimu za kusimamia eneo hili hazijawezeshwa kifedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kutilia mkazo juu ya umuhimu wa kusimamia na kudhibiti mazingira yake hususani ya baharini kwa kuziwezesha taasisi husika kifedha ili ziweze kuendana na matakwa ya mkataba ukizingatia kuwa tangu mkataba huu usainiwe nchi wanachama zipo katika hatua mbalimbali za kuridhia kulingana na sheria na taratibu za nchi husika na utaanza kutekelezwa rasmi baada ya nchi sita angalau kuridhia ambapo hadi sasa nchi za Msumbiji na Afrika Kusini ndizo zimeridhia marekebisho ya mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mkataba wa Afrika Mashariki na utunzaji wa mazingira ikiwemo bahari mkataba huu hauna tofauti kubwa na matakwa ya jumla ya Ibara ya 111 na 112 ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo kwa namna moja au nyingine unazitaka nchi wanachama kuwa na mpango wa pamoja wa usimamizi wa mazingira yakiwemo ya bahari. Kuingia kwenye mikataba ya kimataifa ni jambo moja na kutekeleza matakwa ya mikataba hiyo ni jambo jingine, izingatiwe kuwa mkataba wa sasa wa Afrika Mashariki imekuwa kwenye utekelezaji wa nchi wanachama kwa takribani miaka 16 sasa, na mkataba huu ambao unapitishwa kwa azimio la Bunge hili leo ni wa tarehe 01 Aprili, 2010 ambapo ni miaka sita toka kusainiwa kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa ni hatua gani ambazo zimechukuliwa kutekeleza matakwa ya Mkataba wa Afrika Mashariki kuhusu masuala ya Bahari ya Hindi huku ikizingatiwa kuwa nchi za Kenya na Tanzania ndio zinapakana na Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji haya kwa sababu tunaweza kuwa na mikataba mingi ya kimataifa, lakini kama nchi na Serikali kwa ujumla bado hakuna hatua mahususi ya utekelezaji wa mikataba hiyo. Tumeweka mkataba huo wa Afrika Mashariki ili tuangalie maudhui yake na siyo tu kuridhia mipya wakati tunashindwa kutekeleza mikataba ambayo ipo tayari lakini haifanyiwi kazi. Kambi Rasmi ya Upinzani haipingani kabisa na mkataba huu jambo la msingi ni kwa Serikali kuhakikisha inafuata ushauri ambao tumeutoa hapo awali. Baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako naomba nimuite Naibu Waziri Kivuli wa Maliasili na Utalii atoe maoni ya Kambi juu ya Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi pamoja na Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Nagoya ya Kusimamia Upatikanaji wa mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo matumizi ya rasilimali za kijenetiki.

**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU KURIDHIA MAREKEBISHO YA MKATABA WA NAIROBI WA HIFADHI, USIMAMIZI NA UENDELEZAJI WA MAZINGIRA YA BAHARI NA UKANDA WA PWANI YA MAGHARIBI YA BAHARI YA HINDI- *(AMENDED CONVENTION FOR THE PROTECTION, MANAGEMENT AND DEVELOPMENT OF THE MARINE AND COASTAL ENVIRONMENT OF THE WESTERN INDIAN OCEAN)* - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

Yanatolewa kwa mujibu wa kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la Januari, 2016"

**1. UTANGULIZI;**

**Mheshimiwa Spika,** Mkataba wa Nairobi kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Pwani ya Kanda ya Afrika Mashariki unalenga katika kusimamia mazingira ya Baharini na Ukanda wa Pwani

Tanzania ni nchi mwanachama kati ya Nchi tisa zilizo katika ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Hindi kutoka mwaka 1996.

**2. MAPITIO YA MKATABA**

**Mheshimiwa Spika,** Kwakuwa moja ya majukumu ya mkataba huu kwa nchi mwanachama ni kutekeleza mashari ya mkataba huu '*The Contracting Parties shall co-operate in the formulation and adoption of protocols to facilitate the effective implementation of this Convention*'

**Mheshimiwa Spika,** Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri yafuatayo:

i. Serikali sasa ichukue hatua kwa kutunga sheria mahsusi ya kutekeleza hili, ama kufanya marekebisho ya Sheria ya Mazingira (EMA-Environmental Management Act) ili kuendana sambamba na matakwa ya Mkataba huu
Mfano:

Ibara za 5, 6 na 9: Uchafuzi wa mazingira kutokana kwenye Meli 'Pollution from Ships, na utupaji taka baharini
Serikali inatakiwa kuchukua hatua mahsusi ili kuhakikisha inadhibiti uchafuzi wa mazingira baharini kwa kuzingatia sheria za kimataifa. Hivyo basi, Serikali inatakiwa kuiwezesha kitengo cha Marine chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ili kuweza kusimamia na kutekeleza Sheria zake za utunzaji wa Mazingira, kama zipo!

ii. Serikali itenge fedha mahususi kwa ajili ya udhibiti na usimamizi wa uharibifu wa Mazingira kwa;

- Kuwezesha kifedha baraza la Usimamizi wa Mazingiria (NEMC- National Environmental Management Council) ili kuweza kusimamia na kudhibiti uharibu wa mazingira katika

sekta mbalimbali ili kuhakikisha madhara ya uharibifu ya mazingira hayatokei katika bahari na ukanda wa pwani

- Kuwezesha kifedha Mfuko wa Mazingira, ulio chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Wizara ya Muungano na Mazingira ili kuweza kusimamia utunzaji na usimamizi wa Mazingira Mfano:

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 11: Bioanuai 'Biological Diversity', Serikali inatakiwa kuhifadhi na kulinda bioanuai, viumbe adimu au vilivyo hatarini kutoweka; kuanzisha maeneo tengefu kama vile hifadhi za wanyamapori na misitu sanjari na kuzuia shughuli zinazoweza kusabisha uharibifu wa viumbe hao pamoja na maeneo yao.

Je, hili litatekelezwaji ilhali Sekta muhimu za kusimamia eneo hili hazijawezeshwa kifedha?

**Mheshimiwa Spika,** Hivyo basi, Kambi rasmi ya Upinzani bungeni inaishauri Serikali kutilia mkazo juu ya umuhimu ya kusimamia na kudhibiti mazingira yake hususani ya Baharini kwa kuziwezesha Taasisi husika kifedha ili ziweze kuendana na matakwa ya Mkataba ukizingatia kuwa Tangu mkataba huu usainiwe, Nchi wanachama zipo katika hatua mbalimbali za kuridhia kulingana na sheria na taratibu za nchi husika na utaanza kutekelezwa rasmi baada ya nchi sita (6) kuridhia, ambapo hadi sasa ni nchi za Msumbiji na Afrika Kusini ndizo zimeridhia marekebisho ya Mkaba huu.

### 3. MKATABA WA AFRIKA MASHARIKI NA UTUNZAJI WA MAZINGIRA IKIWEMO BAHARI

**Mheshimiwa Spika**, Mkataba huu hauna tofauti kubwa na matakwa ya jumla ya ibara ya 111 na 112 ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo kwa namna moja ama nyingine unazitaka nchi wanachama kuwa na mpango wa pamoja wa usimamizi wa mazingira yakiwemo ya Bahari.

**Mheshimiwa Spika**, kuingia kwenye mikataba ya kimataifa ni jambo moja na kutekeleza matakwa ya mikataba hiyo ni jambo lingine. Izingatiwe kuwa Mkataba wa sasa wa Afrika

Mashariki umekuwa kwenye utekelezaji kwa nchi wanachama kwa takribani miaka 16 sasa. Na mkataba huu ambao unapitishwa kwa azimio la Bunge hili leo ni wa tarehe 01 Aprili, 2010 ambapo ni miaka sita toka kusainiwa kwake.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kulieleza Bunge lako tukufu kuwa ni hatua gani ambazo zimechukuliwa kutekeleza matakwa ya Mkataba wa Afrika Mashariki kuhusu masuala ya Bahari ya Hindi huku ikizingatiwa kuwa nchi za Kenya na Tanzania ndio zinapakana na Bahari ya Hindi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji haya kwa sababu tunaweza kuwa na mikataba mingi ya Kimataifa lakini kama nchi na serikali kwa ujumla bado hakuna hatua mahususi za utekelezaji wa mikataba hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** tumeweka Mkataba huo wa Afrika ya Mashariki ili tuangalie maudhui yake, na sio tu kuridhia mipya wakati tunashindwa kutekeleza mikataba ambayo ipo tayari lakini haifanyikazi.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani haipingani kabisa na Mkataba huu. Jambo la msingi ni kwa Serikali kuhakikisha inafuata ushauri ambao tumeutoa hapo awali.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

**Dr. Sware V. Semesi (Mb)**
**K.n.y Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira.**
**29.06.2017**

**MWENYEKITI**: Ahsante, huyo namuita mimi siyo wewe, Mheshimiwa Gekul.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI – OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Kuridhia Itifaki ya Udhibiti ya Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi kutokana na vyanzo na shughuli zinazofanyika nchi kavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itifaki hii ya udhibiti wa uchafuzi wa mazingira ya bahari ya Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi kutokana na vyanzo na shughuli zinazofanyika nchi kavu. Vyanzo na shughuli zinazofanyika nchi kavu maana yake ni kutokana na shughuli za kila siku zinazofanywa na jamii mbalimbali katika kujitafutia riziki za kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawanda ya Itifaki hii yameelezwa kwa undani katika Ibara ya 2 na vifungu vyake, vinne lakini mkataba hauhusishi mito ambayo inaishia kwenye maziwa yetu ya ndani. Kwa maana nyingine ni kwamba hauhusishi mito ambayo haimwagi maji yake kwenye bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 5 inahusu udhibiti wa umwagaji au utiririshaji taka kwenye maji au uchafuzi wa hewa katika maeneo ya bahari na Ukanda wa Pwani kutoka kwenye makazi, viwanda na vyombo vya usafiri wa majini. Aidha, Ibara hii inazitaka nchi wanachama kuweka viwango vya kudhibiti uchafuzi na kuvisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba miji mingi iliyopo Pwani mwa Bahari ya Hindi, mifumo ya maji taka imeunganishwa moja kwa moja kuingia baharini. Jambo hili ni chanzo kimojawapo cha uchafuzi wa mazingira ya bahari, ni mtazamo wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuondokana na tabia hiyo ya kuelekeza maji taka baharini, sambamba na hilo kuacha kabisa ile tabia iliyozoeleka ya wakazi wa mijini ya kutapisha vyoo vyao hovyo.Kambi Rasmi ya Upinzani katika mawasilisho yake, wakati wa kuchangia hoja ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira ilishauri kufanyika kwa

*recycling* ya taka maji hayo kwa matumizi mengine. Sambamba na hilo ni kwa viwanda vinavyotoa maji machafu vifunge mifumo ya kuyazungusha maji taka hayo kwa matumizi ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 6 inazitaka nchi wanachama kuchukua hatua za kudhibiti uchafuzi unaotokana na shughuli za kilimo zisizo endelevu ambazo zinaweza kuathiri mazingira ya bahari na Ukanda wa Pwani. Ibara hii ni pana mno kwani inagusa moja kwa moja na shughuli za kimaisha za jamii nyingi za kiasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kisichoendelevu kinachangiwa na aina ya kilimo kama vile matumizi ya mitambo mikubwa ya kilimo kama vile matrekta makubwa na hivyo kuifanya ardhi kuwa laini kuweza kuchukuliwa na mikondo ya maji. Pia matumizi yasiyo sahihi ya mbolea na madawa ya mimea na kuulia wadudu. Aidha, madawa na mbolea *fake* ni chanzo pia cha uchafuzi wa mazingira ya bahari. Tukumbuke kwamba pale mvua nyingi zinaponyesha mikondo hiyo ya maji yaliyoharibika tayari inaishia baharini na hivyo kuwa chanzo cha uchafuzi wa mazingira ya bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 15 inazitaka nchi wanachama kuhamasisha utapitakanaji wa taarifa na nyaraka muhimu zinazohusu uchafuzi toka nchi kavu. Aidha, nchi hizo zinasisitiza kukuza uelewa kwa jamii ma kuhakikisha jamii zinazoshirikishwa katika kutoa maamuzi yanayohusu utekelezaji wa itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli pia jamii nyingi zinazoishi kando kando mwa mito mikubwa, miaka yote wanatumia maji hayo kwa shughuli mbalimbali kama vile kufanya usafi binafsi wa mwili na nguo zao, makabila mengine yanatumia mito hiyo kwa uvuvi na wanatumia madawa ya mashambani au sumu kwa shughuli hizo. Aidha, wengine wanatumia mito hiyo kama vyoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, elimu ya kutosha kwa jamii zilizo kwenye mito mikubwa ni muhimu sana

kufanyika. Tukumbuke usemi usemao jasiri haachi asili, hivyo kuondokana na tabia ya jadi ni jambo gumu sana bila ya kutoa elimu ya kutosha kwa jamii husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Kambi Rasmi ya Upinzani haipingani na mahudhui ya Mkataba huu bali tunaitaka Serikali kuzingatia ushauri tulioutoa kwani kwa njia moja au nyingine mkataba unaathiri maisha ya kila siku ya jamii zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha kwa upande wa itifaki hii. *(Makofi)*

## MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU KURIDHIA ITIFAKI YA UDHIBITI WA UCHAFUZI WA MAZINGIRA YA BAHARI NA UKANDA WA PWANI YA MAGHARIBI YA BAHARI YA HINDI KUTOKANA NA VYANZO NA SHUGHULI ZINAZOFANYIKA NCHI KAVU- *(PROTOCOL FOR THE PROTECTION OF THE MARINE AND COASTAL ENVIRONMENT OF THE WESTERN INDIAN OCEAN FROM LAND-BASED SOURCE AND ACTIVITIES) - KAMA YALIVYYOWASILISHWA MEZANI*

Yanatolewa kwa mujibu wa kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la Januari, 2016"

### 1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Itifaki hii ya udhibiti wa uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi kutokana na vyanzo na shughuli zinazofanyika nchi kavu.

Vyanzo na shughuli zinazofanyika nchi kavu, maana yake ni kutokana na shughuli za kila siku zinazofanywa na jamii mbalimbali katika kujitafutia riziki za kila siku.

**Mheshimiwa Spika**, chimbuko la Itifaki hii ni Mkataba wa Nairobi uliofanyiwa marekebisho na ambao ulitiwa saini na wanachama wake tarehe 1 Aprili, 2010 Nairobi, Kenya.

## 2. MAPITIO YA ITIFAKI

**Mheshimiwa Spika,** mawanda ya Itifaki hii yameelezwa kwa undani katika Ibara ya 2 na vifungu vyake, vine lakini mkataba hauhusishi mito ambayo inaishia kwenye maziwa yetu ya ndani. Kwa maana nyingine ni kwamba hauhusishi mito ambayo haimwagi maji yake kwenye bahari ya Hindi.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 5 inahusu udhibiti wa umwagaji au utiririshaji taka kwenye maji au uchafuzi wa hewa katika maeneo ya bahari na ukanda wa Pwani kutoka kwenye makazi, viwanda na vyombo vya usafiri wa majini. Aidha, Ibara hii inazitaka nchi wanachama kuweka viwango vya kuthibiti uchafuzi na kuvisimamia.

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli kwamba miji mingi iliyopo Pwani mwa bahari ya Hindi,mifumo ya maji taka imeunganishwa moja kwa moja kuingia baharini. Jambo hili ni chanzo kimojawapo cha uchafuzi wa mazingira ya Bahari, ni mtazamo wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuondokana na tabia hiyo ya kuelekeza maji taka Baharini, sambamba na hilo kuacha kabisa ile tabia iliyozoeleka ya wakazi wa mijini ya kutapisha vyoo vyao.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani katika Wasilisho lake, wakati wa kuchangia hoja ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira ilishauri kufanyika kwa "recycling" ya taka maji hayo kwa matumizi mengine. Sambamba na hilo ni kwa viwanda vinavyotoa maji machafu vifunge mifumo ya kuyazungusha maji taka hayo kwa matumizi ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika**,Ibara ya 6 inazitaka nchi wanachama kuchukua hatua za kudhibiti uchafuzi unaotokana na shughuli za kilimo zisizo endelevu ambazo zinaweza kuathiri mazingira ya bahari na ukanda wa pwani. Ibara hii ni pana mno kwani inagusa moja kwa moja na shughuli za kimaisha za jamii nyingi za kiasili.

Mheshimiwa Spika, kilimo kisichoendelevu kinachangiwa na aina ya kilimo kama vile matumizi ya mitambo mikubwa ya

kilimo kama vile matrekta makubwa na hivyo kuifanya ardhi kuwa laini kuweza kuchukuliwa na mikondo ya maji. Pia matumizi yasiyo sahihi ya mbolea na madawa ya mimea na kuulia wadudu. Aidha, madawa na mbolea feki ni chanzo pia cha uchafuzi wa mazingira ya bahari. Tukumbuke kwamba pale mvua nyingi zinaponyesha mikondo hiyo ya maji yaliaharibika tayari inaishia baharini na hivyo kuwa chanzo cha uchafuzi wa mazingira ya bahari.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 15 inazitaka nchi wanachama kuhamasisha utapitakanaji wa taarifa na nyaraka muhimu zinazohusu uchafusi toka nchi kavu. Aidha nchi hizo zinasisitizwa kukuza uelewa kwa jamii ma kuhakikisha jamii zinashirikishwa katika kutoa maamuzi yanayohusu utekelezaji wa itifaki hii.

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli pia jamii nyingi zinazoishi kando mwa mito mikubwa, miaka yote wanatumia maji hayo kwa shughuli mbalimbali kama vile kufanya usafi binafsi wa mwili na ngua zao, makabila mengine yanatumia mito hiyo kwa uvuvi na wanatumia madawa ya mashambani au sumu kwa shughuli hizo. Aidha, wengine wanatumia mito hiyo kama vyoo. Hivyo basi, elimu ya kutosha kwa jamii zilizo kwenye mito mikubwa ni muhimu sana kufanyika. Tukumbuke usemi usemao "jasiri haachi asili", hivyo kuondokana na tabia ya jadi ni jambo gumu sana bila ya kutoa elimu ya kutosha kwa jamii husika.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kambi Rasmi ya Upinzani haipingani na mahudhui ya Mkataba huu bali tunaitaka Serikali kuzingatia ushauri tulioutoa kwani kwa njia moja au nyingine mkataba unaathiri maisha ya kila siku ya jamii zetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

**Pauline P. Gekul (Mb)**
**Msemaji Mkuu-Kambi Rasmi ya Upinzani-Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira.**
**29.06.2017**

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa tunaanza mjadala.

**MHE. PAULINE P. GEKUL - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI – OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MAZINGIRA:** Itifaki ya pili Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI**: Bado?

**MHE. PAULINE P. GEKUL - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI – OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MAZINGIRA**: Bado ya pili na ya mwisho.

**MWENYEKITI**: Haya malizia.

**MHE. PAULINE P. GEKUL - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI – OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Kuridhia Itifaki ya Nagoya ya Kusimamia Upatikanaji na Mgawanyo Sahihi wa Faida zitokanazo na Matumizi ya Rasilimali za Kijenetiki. Naomba yote yaingie kwenye *Hansard* lakini kwa kuokoa muda nisome maoni ya jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maoni ya jumla kuingia kwenye *Hansard* Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ilitilie mkazo haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Serikali ihakikishe Rasilimali za Kijenetiki za asili zinalindwa. Mfano, mbegu za nafaka na mazao mbalimbali, miti ya asili, mifugo yetu ya asili ambayo zimekuwa himilivu kwa magonjwa, ukame na mabadiliko ya hali ya hewa. Aidha, pendekezo hili la Kambi Rasmi ya Upinzani halina maana ya kupuuza tafiti mbalimbali katika maeneo haya bali ina lengo la kuikumbusha Serikali...

**KUHUSU UTARATIBU**

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi hatujapewa kitabu cha maoni ya Upinzani.

**MWENYEKITI:** Kitabu?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, cha maoni ya Upinzani na akimaliza kusoma hapo tunaanza kuchangia, sasa tunachangia huku ambapo hatujasoma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, nimekuambia vitabu vinakuja vyote, vilichelewa vya upande wa huku vinakuja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vinakuja lini?

**MWENYEKITI:** Vinakuja, vyote vinakuja na msifanye *interruptions* ambazo hazinia nini. Endelea Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL - NAIBU MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha pendekezo hili la Kambi Rasmi ya Upinzani halina maana ya kupuuza tafiti mbalimbali katika maeneo hayo bali yana lengo la kuikumbusha Serikali kulinda na kuendeleza rasilimali zetu za kijenetiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pili, Serikali iwe makini na watafiti wanaoingia nchini kufanya tafiti mbalimbali ili kuhakikisha kuwa rasilimali zetu za kijenetiki hazipotezwi kwa maksudi au kwa lengo baya kwa mwavuli wa utafiti. Mfano halisi ni vyura wa kihansi wanaopatikana katika maporomoko ya Udzungwa waliopelekwa nchini Marekani Chuo Kikuu cha Colorado kwa ajili ya utafiti lakini jambo la kushangaza baada ya vyura hao kurudishwa nchini wameendelea kutoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zinaonyesha pengine kutoweka kwa vyura hawa kunaweza kuwa kumesababishwa na aina fulani ya *fungus* waitwao *chytrid* hivyo ni muhimu sana Serikali ikawa makini na watafiti wa

kigeni pamoja na aina mbalimbali ya rasilimali za kijenetiki zinazopelekwa nje ya mipaka ya nchi yetu.

Tatu, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri pamoja na kazi zinazofanywa na watafiti wetu hapa nchini bado vyuo vya utafiti vina hali ngumu sana jambo ambalo linaathiri ufanisi wa utafiti au tafiti zetu za kufahamu thamani halisi ya rasilimali zetu za kijenetiki. Vyuo hivi vinakosa fedha na hata pale zinapotoka fedha hizo hazitoki kwa wakati, hivyo basi ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba Serikali kuwekeza vizuri katika vyuo vyetu vya tafiti ili kuweza kunufaika na rasilimali zetu za kijenetiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho Kambi Rasmi ya Upinzani inasema jambo la msingi ni kuhakikisha tunasimamia vema rasilimali zetu za kijenetiki ili zisije zikapotea kutokana na uingizwaji wa nguvu wa rasilimali kutoka kwa wenzetu wenye lengo la kuhakikisha vya kwetu vinapotea kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani haipingani na kuridhiwa kwa Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU KURIDHIA ITIFAKI YA KUSIMAMIA UPATIKANAJI NA MGAWANYO SAHIHI WA FAIDA ZITOKANAZO NA MATUMIZI YA RASILIMALI ZA KIJENETIKI**

***(Nagoya Protocol on Access to Genetic Resources and the Fair and Equitable Sharing of Benefits Arising from their Utilization to the Convention on Biological Diversity) –*** **KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

“ Yanatolewa kwa Mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016”

Mheshimiwa Spika, Rasilimali za Kijenetiki ni vinasaba

mbalimbali katika mimea, wanayama na viumbe hai wengine, vinasaba husika katika viumbe hai kwa ujumla wake ni muhimu katika utafiti wa mimea na wanyama na matumizi ya bioteknolojia ya kisasa.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni mwanachama wa Mkataba wa Bioanuai wa mwaka 1992, unaohusu hifadhi ya bioanuai; matumizi endelevu ya bioanuai; na mgawanyo wa faida zitokanazo na matumizi ya bioanuai. Tanzania ili saini mkataba huu tarehe 8 Machi,1996.

**Mheshimiwa Spika**, Mkataba huo wa Bioanuai una itifaki mbili, moja ni Itifaki ya Cartegana ya mwaka 2000 na Tanzania iliridhia Itifaki hii tarehe 16 Machi 2003. Itifaki ya pili ni hii tunayoridhia sasa ambayo ilianzia rasmi kwenye mkutano wa sita (6) wan chi wanachama uliofanyika Afrika ya Kusini mwaka 2002 na kuhitimishwa na rasmi katika mkutano wa wanachama uliofanyika Nagoya Japan mwaka 2010.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania na Afrika nchiza ilikuwa na rasilimali za kijenetiki nyingi sana, lakini kutokana na teknolojia inayoletwa rasilimali hizo zimeendelea kupotea na sasa baada ya wale waliozipoteza kuona hilo wanarudi tena na mikataba kama hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza ni nani au kabila gani lisilokuwa na aina yake ya mbegu au nina asiyefahamu kuwa ng'ombe aina ya Zebu asili yake ni Tanzania? Na je ni kwanini ng'ombe aina hiyo wanafanyiwa mkakati wa kuhakikisha wanapotea kabisa. Sababu kuu ni moja kwamba aina hiyo ya ng'ombe inavumilia sana magonjwa na kwa sababu hiyo wale wanaotengeneza madawa ya mifugo watauza wapi madawa hayo?

**Mheshimiwa Spika,** si hilo tu mbegu zetu za asili inajulikana kwamba ni mbegu zilizokuwa zinavumilia sana mazingira yetu japokuwa hazikuwa zinazalisha sana, lakini kwa wenzetu kuliona hilo wakaja na ujanja wa kutuaminisha kuwa zina matatizo, na mbegu nyingi za asili kwa makabila mbali mbali

zimepotea kabisa. Huo ulikuwa ni mkakati maalum wa kuhakikisha masoko ya madawa yao ya kilimo na mbegu zao zinapata soko kwetu.

**Mheshimiwa Spika,** huo ulikuwa ni mtazamo wetu kuhusiana na raslimali zetu za kijenetiki zinavyopotea na baadae tunaambiwa tuzilinde.

**Mheshimiwa Spika**,hiyo haiondoi ukweli kwamba kama nchi tukiridhia mkataba huu, watanzania na jamii mbalimbali za kitanzania zitanufaika kwa Nyanja mbalimbali kama zilivyooneshwa katika Ibara ya Tano ya Itifaki, sambamba na hilo ni kwenye utangulizi katika aya ya nne na tano. Faida zake zimeelezewa vizuri na zinaeleweka kwa wale wote wanaohitaji kuelewa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na manufaa ya itifaki hii kwa Tanzania na jamii nzima ya kitanzania, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini raslimali za kijenetiki ziko nchi nzima na kwa kila jamii, kwa msingi huo hatuna sababu yoyote ya kupingana na uridhiwa wa azimio hili.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Serikali mara nyingi imekuwa ikijivuta katika suala zima la kutunga sheria za ***"ku-domesticate"*** itifaki zinazoridhiwa na Bunge ili kuweka uratatibu mzuri zaidi wa kiutendaji.

**Mheshimiwa Spika**, katika kukazia hoja hiyo, Ibara ya 15 ya Itifaki inasema kuhusu ***"compliance with domestic legislation or regulatory requirements on access and benefit sharing",***

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli kwamba kwa kiasi kikubwa Tanzania imekuwa ikipoteza rasilimali zake za kijenetiki katika sekta ya madawa ya asilia pale ambapo wanaojiita watafiti wanachukua mimea yetu kwa ajili ya kufanyia utafiti zaidi kwa kigezo kwamba Tanzania haina maabara za kisasa kuweza kutoa matokea tarajiwa. Hivyo basi kwa kifungu hicho na kama usimamizi na jutekelezaji wa sheria zetu za ndani utakuwa imara ni dhahiri nchi yetu itanufaika zaidi na rasilimali za kijenentiki.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 17 inasema kuhusu ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za kijenetiki, hoja ya msingi ni matumizi hayo yanafuatiliwa wapi? Kwa kuwa rasilimali hizo zipo katika jamii yetu na kwa njia moja au nyingine jamii ndiyo mtumiaji mkuu na muangalizi wa rasilimali hizo. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kwamba; jambo la muhimu kwanza ni kuzitambua raslimali ambazo inahitaji na kuziwekea utaratibu ili matumizi yake yawe endelevu, kinyume cha hapo wananchi wanaweza kupata madhara kutoka kwenye vyombo vya dola bila ya wao kufahamu. Mfano mzuri ni matumizi ya mti wa Mpingo, watanzania wengi wana ufahamu ni kwanini mti huo unalindwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kwanza kutambua rasilimali hizi ziko wapi na hivyo kutoa elimu kwa jamii mbalimbali za kitanzania ambazo ndizo mmiliki wa rasilimali husika ili wazitunze na kuziendeleza kwa manufaa ya kizazi kilichopo na cha baadae. Hii imejitokeza katika Ibara ya 21, japokuwa ugumu unaweza kujitokeza kutokana na ukweli kwamba jambo hili linahitaji rasilimali fedha za kutosha ili itifaki hii iweze kutoa mrejesho uliohitajika kwa taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa ushauri huo kutokana na ukweli kwamba, mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaikumba Dunia yetu vile vile yanasababisha kupotea kwa rasilimali nyingi za kijenetiki katika mimea, wanyama na viumbe hai wengine. Hivyo ni jukumu la nchi kuhakikisha rasilimali zetu za kijenetiki zinaendelea kuhifadhiwa.

## MAONI YA JUMLA

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kueleza hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iltilie mkazo haya yafuatayo:

i. Serikali ihakikishe rasilimali za kijenetiki za asili zinalindwa, mfano. Mbegu za nafaka na mazao mbalimbali, miti ya asili, mifugo yetu ya asili ambayo zimekuwa himilivu kwa magonjwa, ukame na mabadiliko ya hali ya

hewa.Aidha, pendekezo hili la Kambi Rasmi ya Upinzani halina maana ya kupuuza tafiti mbalimbali katika maeneo hayo bali lina lengo la kuikumbusha Serikali kulinda na kuendeleza rasilimali zetu za kijenetiki.

ii. Serikali iwe makini na watafiti wanaoingia nchini kufanya tafiti mbalimbali ili kuhakikisha kuwa rasilimali zetu za kijenetiki hazipotezwi kwa makusudi au kwa lengo baya kwa mwavuli wa utafiti. Mfano halisi ni vyura wa kihansi wanaopatikana katika maporomoko ya Udzungwa waliopelekwa nchini Marekani (Chuo Kikuu cha Colorado) kwa ajili ya utafiti, lakini jambo la kushangaza baada ya vyura hao kurudishwa nchini wameendelea kutoweka. Tafiti zinaonesha pengine kutoweka kwa vyura hawa (***nectophrynoides asperginis***) kunaweza kuwa kumesababishwa na aina fulani ya fungus waitwao ***chytrid.*** Hivyo ni muhimu sana Serikali ikawa makini na watafiti wa kigeni pamoja na aina mbalimbali ya rasilimali za kijenetiki zinazopelekwa nje ya mipaka ya nchi yetu.

iii. Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi zinazofanywa na watafiti wetu hapa nchini bado vyuo vya utafiti vina hali ngumu sana, jambo ambalo linaathiri ufanisi wa tafiti zetu za kufahamu thamani halisi ya rasilimali zetu za kijenetiki. Vyuo hivi vinakosa fedha na hata pale zinapotoka hazitoki kwa wakati. Hivyo basi ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwekeza vizuri katika vyuo vyetu vya tafiti ili kuweza kunufaika na rasilimali zetu za kijenetiki.

iv. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema jambo la msingi ni kuhakikisha tunasimamia vyema rasilimali zetu za kijenetiki ili zisije zikapotea kutokana na uingizwaji wa nguvu wa rasilimali toka kwa wenzetu wenye lengo la kuhakikisha vya kwetu vinapotea kabisa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani haipingani na

uridhiwaji wa azimio hili, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha.

**......................**
**Pauline Philipo Gekul (Mb)**
**Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani –**
**Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira**
**29.06.2017**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru maeneo yote mawili hakuna upande ambao umepinga kuridhiwa kwa hiyo sasa tunaanza mjadala na tunaanza na Mheshimiwa Dau, ajiandae Mheshimiwa Kitandula, Mheshimiwa Kuchauka na Mheshimiwa Lema kwa dakika tano.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kuunga mkono itifaki ya Azimio hili na kwa namna ya kipekee kabisa niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuunge mkono hili jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natokea Mafia, kwa kiasi kikubwa sana maisha ya watu wa Mafia ambayo ni kisiwa maisha yetu ni bahari na bahari ndio watu wa Mafia. Chochote kile ambacho kinaelekea katika kulinda na kuhifadhi bahari kwa maana nyingine hicho ni chenye kutoa manufaa na nafuu kwa watu wa Mafia. Hali ya mazingira ya bahari kwa sasa ni mbaya sana, kwa maana ya kwamba kuna baadhi ya visiwa, Mafia ni kisiwa lakini ndani yake kuna visiwa vidogo vidogo. Vile visiwa vidogo vidogo vingine vimeshaanzwa kumezwa na bahari kutokana na uchafuzi wa mazingira na mabadiliko ya masuala ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa wadogo kule Mafia tulikuwa tunakwenda kuvua katika maji usawa wa magoti, lakini sasa hivi unaweza ukaenda maji ya kina

kikubwa kabisa na vyombo na ukarudi ukiwa na kikapu kimoja au pengine ukarudi mikono mitupu. Kwa hiyo, ipo haja ya makusudi kabisa sisi Wabunge tukubaliane na tuliunge mkono Azimio hili ambalo lina nia njema na nchi yetu na mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha ifikapo mwaka 2030 ndani ya bahari na hususan Bahari ya Hindi kutakuwa na takataka nyingi zaidi kwa maana ya mifuko hii ya "rambo" na mifuko mingine ya plastiki kuliko samaki wenyewe. Kwa hiyo, hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ilipotokea ile ndege ya Malaysia ikapotea na ikasemekana imeangukia baharini ndipo wataalam wakaenda kugundua mambo makubwa zaidi yaliyokuwepo chini ya bahari kutokana na uchafuzi wa mazingira, wakakuta kuna takataka nyingi mno. Tuna kila aina ya sababu kuhakikisha kwamba tunaunga mkono Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafia kuna taasisi maalum inayohusiana na masuala ya uhifadhi wa bahari maarufu kama *Marine Park.* Ningeomba sana na sina uhakika kama Waziri mwenye dhamana ya Kilimo, Uvuvi na Mifugo yupo hapa, lakini ningeomba sana watusaidie wenzetu wa Serikali kuhakikisha kwamba ile Taasisi ya Hifadhi ya Bahari inajikita na kujiingiza zaidi katika suala la uhifadhi. Kwa sasa hivi wamekuwa wana mambo mengi zaidi kuliko uhifadhi wenyewe. Wamejiingiza katika masuala ya ukusanyaji wa maduhuli, wamejiingiza katika masuala ya ujenzi, masuala ya uwekezaji na uuzaji wa visiwa, wanajikuta mpaka kwenye *the core business* yao wamekuwa *diverted* na sasa wanashughulika zaidi na mambo ambayo hayawahusu na hayahusiani zaidi na uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana kama Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi yupo hapa ahakikishe kwamba, anawaelekeza watu wa hifadhi ya bahari Mafia wajikite kwenye uhifadhi, hiyo ndiyo shughuli yao ya msingi waachane na habari ya kuuza visiwa, kuuza maeneo, mambo ya ujenzi,

uwekezaji, ukusanyaji wa maduhuri hilo ni suala la *TRA* na Halmashauri ya Mafia tunaweza tukayafanya sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kidogo suala la mbadala. Ndugu yangu Mheshimiwa Kitandula amekuwa akizungumza sana hapa, suala la ufugaji wa samaki. Baharini samaki wa bahari pia wanafugwa. Sasa kutokana na hali...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kitandula, ajiandae Mheshimiwa Kuchauka na Mheshimiwa Lema pia ajiandae.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie kwenye itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema naiunga mkono itifaki hii kwa sababu inazungumzia maisha ya sisi watu wa Pwani na sisi watu wa Pwani bila bahari maisha hayapo. Vilevile niseme kwamba itifaki hii itakuwa na maana tu kama itatuhakikishia watu wa Pwani maisha yetu yataboreka. Kama itifaki hii haitatusaidia maisha yetu kuboreka haina maana, kama itifaki hii haitatuhakikishia kuboreka kwa maisha ya watu wa Pwani basi itifaki hii haina maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu mwaka 1996 tulisaini mkataba ule uliokuwa unazungumzia udhibiti wa bahari ukanda wa Afrika Mashariki. Mwaka 2010 tukaiboresha itifaki ile tukasaini. Nataka tu nijiulize hivi tangu 1996 tuliposaini watu wa Pwani maisha yamekuwa bora? Nini kinatuhakikishia leo kwa kusaini itifaki hii kwamba maisha ya Pwani yataboreka? Utafiti umetuonyesha kwamba itifaki hii katika utekelezaji wake tangu mwaka 1996 umekuwa na changamoto kubwa ya kimfumo wa usimamizi wa taasisi

za usimamizi, vilevile changamoto kubwa ya kifedha. Tafiti hazifanyiki na zikifanyika zinafanyika kwa ufinyu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo watu wa Pwani zana tunazotumia kwenye uvuvi ni zana duni, tumekuwa tukitamani tuyaone yanayofanyika kwenye sekta ya kilimo kupewa pembejeo na vitu vya namna hii, yafanywe kwenye sekta ya uvuvi hayafanyiki. Tumekuwa tukitamani tuyaone yanayofanyika kwenye sekta ya mifugo kwa watu wa sekta ya uvuvi hayafanyiki. Ndiyo maana mnashuhudia watu wale wanaendelea kutumia zana duni za tangu enzi ya Nabii Nuhu. Ndiyo maana mnashuhudia uvuvi wa kutumia mabomu unaendelea, ndiyo maana mnaona mazalia ya samaki yanaendelea kuharibika kwa sababu tumeitupa mkono sekta ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifurahi kwenye Ilani yetu tuliposema kwamba katika kipindi hiki tutaleta meli tano za uvuvi. Nataka tu niikumbushe Serikali yangu, mwaka wa pili huu sasa wa utekelezaji, tumebakia na miaka mitatu tujitahidi ahadi ile itimie. Lakini hata ahadi hiyo ikitimia bado asilimia kubwa ya wavuvi watakuwa hawana zana za kisasa kwenda kuvua, ndiyo maana leo unaona hata kwenye uuzaji wetu wa samaki tunategemea sana samaki wa kutoka Ziwa Victoria, uvuvi kwenye eneo la baharini uko duni. Twendeni tukawekeze kwenye *blue economy,* twendeni tukahakikishe ufugaji wa samaki unafanyika kwenye ukanda wa Pwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jarida la Sofia la *FAO* linatuambia hivi takribani watu milioni 57 wana... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Kuchauka

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa nafasi nitoe mchango wangu katika kuridhia hii itifaki ambayo imewasilishwa leo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kama mwasilishaji alivyosema kwamba tunazo faida mbalimbali ameziainisha hapa, faida ambazo tungeweza kuzipata anasema kwamba ni kuimarisha uchumi, kuongeza mazao ya bahari pamoja na ushirikiano wa kikanda. Lakini wazo langu au maoni yangu ni kwamba kwanza kabisa niungane na Kambi Rasmi ya Upinzani yale maoni ambayo wameyatoa naishauri Serikali iendelee kuyazingatia kwa umakini kabisa, kwa sababu tatizo letu siyo tu kuridhia hii mikataba kwanza ni mipango dhabiti ya utekelezaji wa mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Tanzania imekuwa na kawaida ya kusuasua sana kutekeleza mikataba mbalimbali ambayo tunaingia ya Kimataifa. Kwa mfano, sasa hivi tunakwenda kuridhia hii itifaki ambayo tunaizungumzia leo, lakini je, Serikali iko tayari kuleta sheria, kutunga sheria za utekelezaji ambayo itasimamia kwa uhalisia kabisa kulingana na matakwa ya mikataba hii ambayo tunakwenda kuiridhia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukiangalia tunayo taasisi ambayo kama msemaji aliyepita alisema Taasisi ya Uhifadhi wa Mali/Bidhaa za Bahari. Lakini je, hii taasisi kama Serikali mmeiwezesha kwa kiwango gani ili hayo matakwa yaweze kutekelezeka kama ambavyo tumeridhia? Vilevile kwenye utafiti mara nyingi tumekuwa tukiibiwa rasilimali zetu nyingi za baharini na nchi kavu na hawa watu wanaojiita watafiti. Ni kweli kabisa mara nyingi watafiti wanapofanya utafiti wanaondoka na viumbe hai, wanaondoka na mali zetu, lakini sisi wenyewe tumejidhatiti kwa kiwango gani, hizi tafiti badala ya kufanyika na watu wa nje na wenyewe tuweze kufanya hizi tafiti ili taasisi yetu kwa mfano, *Maritime Institute* pale Dar es Salaam sijui kwamba na yenyewe imeimarishwa kwa kiwango gani ili tafiti nyingine ziweze kufanyika hapa nchini badala ya kwamba hawa watu wanakuja kutuibia, wakati wenyewe tuna uwezo nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukiangalia mara nyingi Watanzania tumekuwa na kigugumizi sana. Mimi sijaelewa Serikali inakuwaga na kigugumizi cha namna gani, kwa sababu ukiangalia mikataba mingi tuliyoridhia kwanza tunachukua muda mrefu sana kuiridhia na baada ya kuiridhia tunakuwa na kigugumizi sana katika utekelezaji. Naiomba Serikali izingatie ushauri ambao umetolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani na Wabunge mbalimbali ambao wanachangia hapa. Hili wote tunajua kwamba tunafanya hivi kwa kuhifadhi mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema ukweli kwa upande wa baharini, kwa kweli Serikali tumesahau sana bahari, kwa sababu ukiangalia uchumi Tanzania tumezungukwa na Pwani kutoka Tanga mpaka Mtwara, lakini ni kiwango gani tunanufaika? Serikali inanufaikaje na fukwe hizi? Tumewekeza kwa kiwango gani? Utakuta uwekezaji tuliouwekeza huku ni mdogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema hapa wakati tunachangia bajeti ya kilimo na uvuvi wakasema kwamba sekta binafsi ndiyo wameachiwa wao ndiyo wanunue meli kubwa za uvuvi ili tuweze kuvua na ndio jambo linalopelekea mpaka leo hii tunakula samaki kutoka China. Hivi kweli kwa utajiri huu tulionao Tanzania kuanzia Tanga mpaka Mtwara leo hii hatuna hata meli moja ya uvuvi wa kisasa, hivi tunategemea ulinzi huu wa hizi rasilimali zetu za baharini huyo mlinzi atatoka wapi? Hivi ni kweli hawa Watafiti ambao tunawategemea kutoka nje ndiyo waweze kulinda mali zetu? Kwa kweli jambo hili silioni kama lina tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwa dhati kabisa tutoke tuwekeze kwenye bahari ili nasi tuweze kunufaika nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa hayo machache naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Peter Msigwa, Mheshimiwa Lema ajiandae.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *in principle* sina tatizo na itifaki zilizoletwa, lakini nilitaka tu tujitafakari kama Bunge. Hili Bunge letu la Bajeti ni Bunge la muda mrefu na Bunge huwa linajua ratiba itakuwaje. Lakini kumekuwa na mazoea kila siku mnapoleta itifaki hizi mnatuletea siku hiyo ya kupitisha hizo itifaki. Hii inaonesha jinsi gani ambavyo Bunge linaonekana halitimizi wajibu wake na kwamba Serikali inatuchukulia poa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vifungu ukiwauliza Wabunge unavipitia saa ngapi, kila wakati itifaki zinapokuja zinaletwa siku hiyo hiyo, hivi vifungu unavipitia saa ngapi? Unasoma saa ngapi? Unapewa dakika tano kuchangia wakati ingegaiwa mapema kwenye Kamati watu wangepitia tunapojua ratiba inavyokwenda tuje tusome, lakini imekuwa *business as usual* tunapiga makofi na Bunge tunakubaliana mikono yetu na nguvu yetu ya Bunge inapungua nguvu kwa mambo kama haya ya kuridhia mambo ambayo hayawezekani, kwa sababu ni mambo ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watalaam wanasema *the past is where you have learn the lesson and the future is where you apply the lesson.* Asubuhi hapa tumejaribu hata kuomba miongozo, mambo ya Hati za Dharura tunarudia tena kana kwamba mambo ya nyuma hatujajifunza kwa sababu tunaenda haraka haya mambo! Wabunge hebu tujiulize, hivi wananchi huko wakituona tunaondoka tumebeba mavitabu haya, tunasoma saa ngapi? Tunasoma saa ngapi hivi vitabu! Tunaletewa muda mfupi! *(Makofi)*

Mheshikiwa Mwenyekiti, hii ni kulifanya Bunge liwe *crippled,* Bunge ambalo haliwezi kuisimamia Serikali, kwa hiyo hapa sisi tumekuja ku-*rubber stamp.* Tukubaliane kwamba, Bunge hili linaongozwa na Serikali, Bunge haliwezi kuisimamia Serikali kwa sababu tunakuja hapa tuna-*rubber stamp... (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa kwa mujibu wa taratibu za Kibunge baada ya Serikali kuwasilisha taarifa yake upande wa Kamati umetoa taarifa yake umeridhia. Fursa imetolewa upande wa Upinzani na amesoma Mheshimiwa Dkt. Sware amesoma na Mheshimiwa Gekul, wote na wao wameunga mkono Itifaki hii na Maazimio haya. Wote upande wa Upinzani na upande wa Kamati.

Ushauri uliotolewa ambao na wewe unayo nafasi ya kusema, tunakubaliana na hiki kitu, lakini mna-*reservations* zenu, ushauri uwe ni huu ili tuende na wenzetu wa kimataifa. Sasa unapoanza lugha zingine Mheshimiwa Msigwa *with due respect,* tumalizeni hii kazi ambayo iko mbele yetu. Soma maoni yako, ushauri unaotaka kutoa uutoe sasa hivi Serikali iufanyie kazi, ndio kazi ya Bunge, kwa sababu haya mengine sijui *rubber stamping,* wala si sehemu yake leo wala siku yoyote nyingine. Kwa hiyo, nakuomba tujielekeze kwenye Azimio.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na unachokisema, lakini kumbuka Waziri Kivuli analetewa *copy,* lakini kama Wabunge tunatakiwa tuwe na *copy* hizi tukae nazo tuzisome. Nimesema ratiba huwa inakuja kabla! Hili Bunge tunakaa miezi mitatu hapa! Sasa kila siku tunaletewa, hebu tuwe wa kweli, umesoma saa ngapi? Aniambie Mbunge tumesoma saa ngapi hivi vifungu ambavyo tunaridhia hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Wabunge hatuwezi kuhoji haya mambo hapa, tutahojia wapi? Ninachozungumza lazima tuwe na Bunge *strong,* Bunge linaloweza kui-*challenge* Serikali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Chief Whip* wa Serikali!

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE,**

**KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Msigwa, kwa utaratibu wa Kibunge tunaoendelea nao na ambao ndiyo utaratibu tunaoutumia ndani ya Bunge, ukiona Kambi ya Upinzani inasoma taarifa hapa ndani ya Bunge ina maana jambo hilo ambalo linaendelea ndani ya Bunge upande huo wa Upinzani walishalipata muda mrefu na ilikuwa ni wajibu wa kila kiongozi kwa upande husika anapopata hoja ya Bunge kuikabidhi kwenye kambi yake ili Wabunge wanaohusika waweze kuiangalia na kujiandaa. *(Makofi)*

Mheshikiwa Mwenyekiti, suala la pili, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge, ratiba ya Vikao vya Bunge toka siku ya kwanza ilionesha tutakuwa na kazi ya Maazimio ndani ya Bunge ambayo kila Mbunge alipaswa kujiandaa.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware kaa chini kwanza.

Mheshimiwa Msigwa, *with due respect,* Maazimio haya yameanza toka Bunge letu lianze miezi mitatu na nusu iliyopita. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nakuomba na Kambi yenu ya Upinzani imeeleza vizuri tu hapa, haipingani kabisa na Maazimio isipokuwa wanataka Serikali ipokee ushauri walioutoa. Sasa na wewe elekea kwenye ushauri, unaposema hujasoma inawezekana utaachwa peke yako humu. Wenzio wamesoma!

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kwa nini tunashindwa kue…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware taarifa.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ningependa kuiambia Serikali na wale wanao-*represent* Serikali, haya makabrasha mengine tumeyasoma asubuhi na kuyafanyia kazi asubuhi, yamechelewa kufika kwenye Kambi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mradi mmeweka Mezani taarifa zenu, ni Taarifa Rasmi za Serikali. Mheshimiwa Msigwa, tunakwenda na *procedure* za Kibunge.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui ni wapi tunashindana, mahali pako wazi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokizungumza hata Waziri akisoma hotuba hapo haimaanishi kwamba Wabunge wa CCM hawatakiwi kuchangia kwa sababu tu Waziri amesoma, ndiyo maana inaletwa humu ndani tutoe mawazo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema tunali-*cripple* Bunge kwa kuleta vitu hivi haraka! Tunatakiwa tupate muda wa kusoma, tuyapitie, tujue vifungu, tuishauri Serikali tunapotoa haya Maazimio, ugumu uko wapi? *(Makofi)*

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshikiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nyongo, taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira. Taarifa hii tulipewa mapema na ndani ya Kamati ya Viwanda na Biashara kuna Wabunge wa Upinzani akiwemo Mheshimiwa Komu ambaye tulipitia naye haya Maazimio. Tumepita tuka-*digest* kwa pamoja, wengine ni Mheshimia Lema ni Mjumbe

wa Kamati yangu, lakini kwa bahati mbaya hajawahi kuhudhuria hata siku moja. *(Makofi)*

Mheshikiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba niwapatie taarifa hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa endelea.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshikiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Nyongo labda kwa sababu hana uzoefu...

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kaa chini sasa, mnachukua muda mwingi. Mheshimiwa Msigwa endelea.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najaribu kumjibu Mheshimiwa Nyongo. Kwenye Kamati huwa zinapewa, mimi nazungumza Bunge. Kamati huwa zinapewa zote zinajadili, atapata uzoefu kidogo, nazungumzia Bunge hizi *document* tusome ili tuje tupitishe vifungu tunavyovijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunarudia makosa yale ambayo tunapewa sheria, tunapitisha, tena tunataka turudie tena. Ninachoomba, hizi itifaki sio mbaya, lakini...

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Komu hebu kaa kwanza. Mheshimiwa Msigwa endelea, wewe endelea Mheshimiwa Msigwa malizia. Mheshimiwa Mnyika mara nyingi hukai Bungeni humu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Sikai au mnanitoa?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba hili Bunge letu, Serikali iwe inafanya vitu kwa utaratibu, kwa sababu Serikali zote duniani huwa zinapenda

kulifanya Bunge liwe kibogoyo ili zifanye mambo yake vizuri. Na sisi kama Wabunge tuna wajibu wa kuhakikisha tunachukua *role* yetu kuisimamia Serikali. Hatuwezi kuchukua *role* kama tunauziwa mbuzi kwenye magunia. Huku ni kuletewa mbuzi kwenye magunia, halafu tunashangilia katika vitu ambavyo hatujasoma, na ni kukwepa wajibu wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshikiwa Mwenyekiti, tunaposema mikataba na sheria ziletwe Bungeni hatumaanishi iletwe kama hivi itupwe hapa! Tuna maana iletwe tupate muda wa kuisoma na kuitafakari ili tuone ni jinsi gani tunawawakilisha wananchi ambao wametutuma, lakini ikiletwa tu hapa inakaa mezani, inaletwa hapa, halafu wanasema tunaazimia, watu tunapiga makofi, tunasema ililetwa Bungeni, hiyo siyo maana halisi ya kuletwa Bungeni. Hakuna kati yetu hapa aliyesoma hapa tukisema lipi ambalo tunaazimia hapa, waliosoma ni wachache sana kwenye Kamati idadi kubwa ya Wabunge hatujasoma. *(Makofi)*

Mheshikiwa Mwenyekiti, hilo ndiyo naliomba tuliinue Bunge letu kiwango. *The more* tutakuwa na Bunge dhaifu, *the more* tutakuwa na Serikali dhaifu. Hawa Mawaziri lazima tuwashughulishe wafanye kazi. Hawa Mawaziri hawatafanya kazi kama Wabunge tutakuwa *weak.* Ni lazima tuwe *after them,* watakuwa na nguvu ili kuishauri Serikali na ndiyo wajibu wetu. *(Makofi)*

Mheshikiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Enhee, Mheshimiwa Komu ulikuwa unasemaje.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshikiwa Mwenyekiti, nakushukuu sana. Alichosema Mheshimiwa Nyongo ni kweli kwamba tulipewa hizo taarifa mapema na tukazifanyia kazi. Lakini jana tulivyo-*wind up* nikataka kuondoka na makabrasha nikaambiwa na Katibu wa Kamati kwamba...

**MWENYEKITI:** Sasa hiyo ni taarifa au unachangia?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaambiwa bado ni mali ya Kamati.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mimi nazungumza na mhusika, mbona wengine mnaanza kunyoosha mikono, mnaanza ku-nini! Eeh vipi tena! Bado mna *fever* ya sikukuu? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Komu haya malizia.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kweli kwamba, taarifa zimefika kwenye Kambi yetu asubuhi. Na sisi kama Wajumbe wa Kamati, hatukuwa na ruksa yoyote ya kwenda kuzisambaza kwa sababu kwanza kazi za Kamati ni siri kwa hiyo, mwenye kutoa ruhusa ni Katibu wa Kamati.

**MWENYEKITI:** Haya, umeeleweka ahsante. Mheshimiwa Rehani, ajiandae Mheshimiwa Mtulia.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi nashukuru kuweza kupata nafasi hii, ninakushukuru kwa kuweza kupewa haya makabrasha na maazimio haya yote matatu wakati mmoja kuweza kuyapitisha, tatizo moja tu lililokuwepo kwamba uelewa wa Wabunge wengi katika haya Maazimio ndiyo kitu kidogo kinachoonekana ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina-*declare interest* kwamba nimefanya kazi kwenye *Marine Conservation* kwenye Mradi wa *MACEP* chini ya *World Bank* miaka mitatu, naelewa haya maazimio yaliyokuwa yamepita huku nyuma. Lakini nilitaka kutoa ushauri tu sijui kama muda utatosha katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja katika maazimio

ambayo yalipendekezwa miaka mingi kwa nchi yetu hii imegeuka dampo la kutupwa takataka nyingi kutoka nchi za nje. Wenzetu Kenya waliridhia mapema, baadae baada ya kuridhia wakawa wanachukua bidhaa kutoka viwandani mwao, zile *by products* zilizomalizika wanakuja kutupa katika bahari yetu kwa sababu tumeshindwa kuridhia mkataba huu, kwa hiyo shamba hili limekuwa kila mmoja anaweza kutupa na kufanya anavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili katika bahari kuna mambo mengi, moja katika vitu vinavyokuwa *disturbed* ni bioanuai iliyopo katika bahari. Mazingira yetu ya bahari yanachafuliwa kwa vitu vingi, hali ya hewa inachangia, lakini mtiririsho wa bidhaa za kikemikali kutoka kwenye viwanda umekuwa ni mkubwa na hasa Watanzania wenyewe tunaufanya. *(Makofi)*

Mheshikiwa Mwenyekiti, tuna viwanda vingi katika *belt* hii ya bahari ambayo Wahindi na wengineo wanaomiliki viwanda vile wanatiririsha maji ambayo yana sumu na kemikali kutoka kwenye viwanda vyao, hawana mifumo ya kuhifadhi maji machafu na ya kemikali ambayo wanatengeneza bidhaa mbalimbali. Sasa sheria hii au Azimio hili liende likawabane hawa wote wenye viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua wazi kwamba wengi wao wanawahonga wale watu wa mazingira wanaokwenda kufanya *impact assessment* katika maeneo yao na kusababisha uchafuzi wa mazingira uongezeke. Bahari yetu, *beach* zetu, kila siku, kila mwaka inaongezeka zaidi ya mita moja, bahari inalika kutokana na *destruction* ambazo zinafanyika za uchafuzi wa mazingira katika maeneo haya, ninaiomba Serikali hili tuweze kulisimamia. *(Makofi)*

Mheshikiwa Mwenyekiti, jingine ambalo linachangia, tumeweka uwekezaji wa mahoteli, tumezuwia wenye mahoteli kujenga ndani ya bahari, lakini yapo mahoteli wamejenga migahawa ndani ya bahari kitu ambacho vilevile kinachangia kuharibu fukwe na kuharibu ule uoto wa asili wa bahari uliokuwemo katika maeneo yale. Ninaishauri

Serikali kwamba tatizo kubwa lililokuweko la nchi nyingi za nje...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa naongeza muda. Endelea Mheshimiwa Rehani.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi za nje zinatumia eneo lile la bahari kuu kupitisha na kumwaga bidhaa mbalimbali katika maeneo hayo. Mfano mdogo nilionao ni meli nyingi zilizokuwa zimezuiliwa kipindi kile na *Al-Shabab* zilikaa na bidhaa zile kwa muda mrefu zikiwa zimezuiliwa katika maeneo yao na bidhaa zile zilimwagwa katika ukanda huu wa bahari yetu sisi.

Kwa hiyo, athari iliyotokea samaki wengi waliokuweko katika maeneo yale waliathirika, lakini watu ambao walitumia wale samaki walipata matatizo ya ngozi na wengine walipata matatizo ya *cancer.* Haya matatizo imekuwa sasa kwetu bila kuridhia mikataba kama hii au maazimio kama haya hatutaweza kuweza kufanya usimamizi wa mazingira yetu. *(Makofi)*

Mheshikiwa Mwenyekiti, lingine lililokuweko katika nchi pamoja na rasilimali nyingi tulizokuwanazo katika eneo letu lakini hakuna doria ambazo zinakwenda kuangalia kitu gani kinafanyika katika ukanda wa bahari kuu, kitu ambacho kila mmoja ana uwezo wa kufanya anachokitaka, mpaka silaha mbalimbali...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtulia, ajiandae Mheshimiwa Lema.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia. Nashukuru kwa michango mizuri iliyotolewa na wenzangu, lakini na wawakilishi wetu wa Kambi Rasmi ya Upinzani na hasa

kuonesha tofauti kwa sababu mara nyingi watu wengi wanafikiri upinzani ni kupinga tu, lakini leo upinzani umeonesha kabisa siyo lengo letu kupinga tu, mambo mazuri tunayaunga mkono. Kwa hiyo, hili nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshikiwa Mwenyekiti, na mimi naunga mkono hizi itifaki, lakini nina maeneo ambayo nayaona lazima tuyaangalie na tuyarekebishe.

Mheshikiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza, Wajumbe wa Kamati na hata watu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wamelalamikia suala la muda, kwamba wakati mwingine Serikali inaingia itifaki muda mrefu takribani miaka sita, bado hawajaleta Bungeni kwa ajili ya kuridhia hilo Azimio. Hili siyo jambo zuri. Naiomba Serikali itambue kwamba, Wabunge kwa ujumla wao wapo kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Tutajitajhidi kufanya lolote lile kwa maslahi ya nchi yetu, kwa hiyo, hata jambo lolote wakiliona zuri wasihofie wala tusiviziane, walete Bungeni na Wabunge huku kama kawaida yetu tutalichangia vizuri.

Kwa hiyo, hili jambo liangaliwe isiwe kawaida ya Serikali kuwa na wasiwasi wa kuleta jambo, jambo lolote lenye maslahi mapana ya nchi yetu wasiwe na kigugumizi, walilete tutalichangia, penye kasoro tutawaeleza, penye kuunga mkono tutaunga mkono, tuwe na utamaduni huo. *(Makofi)*

Mheshikiwa Mwenyekiti, wewe unajua sisi tuko Dar es Salaam pale, tunapozungumzia itifaki ya mambo haya ya bahari mimi nakubaliana na itifaki, lakini nina mashaka na utekelezaji wetu wa kazi zetu wenyewe.

Mheshimiwa Mwneyekiti, wewe Jimbo lako la Ilala pamoja na Jimbo langu mimi la Kinondoni tunaungana pale *Salender Bridge,* tuna mikoko na Serikali tunayo pale Dar es Salaam. Wizara ya Mazingira iko pale Dar es Salaam, lakini mikoko yetu inakufa pale Jangwani na maeneo mengine yote! Sasa haya yataondoshwa kwa itifaki haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kwamba, tuna mto wetu pale Msimbazi, tuna Mto Ng'ombe na mito mingine, inaleta uharibifu mkubwa wa mafuriko ni kwa sababu tu ile mito hatuiangalii. Kwa taarifa tu mwaka huu Jangwani pale tumepita salama sana, nilitumia pesa zangu za Mfuko wa Jimbo kusafisha Mto na hatimaye mafuriko mwaka huu Jangwani pale hayakutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatuna utaratibu wa kulinda mito yetu hii, hizi itifaki sidhani kama zitatusaidia sana. Ni vizuri sasa kama Serikali yetu, kama Viongozi, tujikite katika kutatua matatizo yetu wenyewe, hizi itifaki ni jumla tu, itifaki haiwezi kuja kutuondolea matatizo yetu ya ndani ambayo sisi wenyewe hatufanyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka sheria ya mita 60, hivi hii sheria ya mita 60 kuiacha bahari, hii bahari anaisafisha nani? Tunapokaa umbali wa mita 60 anayetegemewa sasa Serikali ndio ikafanye kazi za kusafisha mito. Je, inafanya? Tunapokaa umbali wa mita 60 inategemewa sasa bahari yetu Serikali ndio ikasafishe, matokeo yake bahari yetu inanuka. *(Makofi)*

Mheshikiwa Mwenyekiti, lakini ukienda nchi zilizoendelea, Paris hata ukienda Dubai, watu sasa hivi wanajenga mpaka kwenye bahari. Hizi sheria sisi tunaangalia kulingana na hali ya sasa au sheria tunaleta tu ili mradi? Lazima tutoe sheria ambazo zitaendana na wakati. *(Makofi)*

Mheshikiwa Mwenyekiti, watu wetu waruhusiwe kujenga kwenye bahari kwa lengo la kutunza hiyo bahari yenyewe. Watu wetu waruhusiwe kukaa karibu na mito kwa lengo la kutunza hiyo mito yenyewe, kwa sababu hiyo Serikali inayotaka watu wakae mbali, wao hawawezi kwenda huko wala hawawezi kwenda kutunza, badala yake tunakuwa na fukwe chafu, tunakuwa na mito michafu ni kwa sababu ya kutengeneza sheria ambazo wakati mwingine hatuna uwezo wa kwenda kuzisimamia. *(Makofi)*

Mheshikiwa Mwenyekiti, mfano watu wangu wa

mabondeni pale wanatakiwa wahame, hivi pale Jangwani mtu anahama vipi wakati watu Dubai wanakaa baharini? Wewe unamhamishaje mtu Jangwani! Una mhamisha mtu Jangwani akakae Mabwepande wakati Jangwani anaenda Posta hata Kariakoo kwa mguu, Mabwepande anatumia nauli shilingi 2,000 na anatumia saa matatu! Mimi nafikiri hii siyo sawa, tutoke huko tuende katika ulimwengu wa kisasa. *(Makofi)*

Mheshikiwa Mwenyekiti, pale Dar es Salaam, Jangwani, watu wako wana uwezo wa kuendelea kukaa pale hakuna madhara yoyote. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshikiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nikazie pale alipoishia Mheshimiwa Msigwa na Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi niwaombe sana, hili Bunge ndiyo *think tank* ya nchi. *Demand* yetu ya kupata nyaraka muhimu kwa ajili ya kuishauri Serikali ni kwa sababu ya kutoa *opinion* ambazo zitawasaidia ninyi na Taifa letu na watoto wa watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshikiwa Mwenyekiti, *opinion* zetu kila mara zinaonekana ni uadui, na hii ndiyo inasababisha kuanza kususiana futari, hii ndiyo inasababisha uhasama unakuwa ni uhasama. Kwa sababu hakuna *opinion* yetu ya msingi ambayo ninyi mtaichukua kama ni jambo muhimu katika Taifa hili. Sisi sote ni Watanzania, mnapokuja na hizi nyaraka sasa hivi naongea hapa hakuna hata hiyo hotuba ya Kambi ya Upinzani haipo mezani. *(Makofi)*

Mheshikiwa Mwenyekiti, leo tu asubuhi hapa tumeambiwa tutajadili habari ya Mikataba na Sheria za Madini mpaka Jumatano mwisho. Sheria hizo mnaleta kwa Hati ya Dharura. Wabunge wamekaa hapa miezi mitatu, wamechoka. Binadamu anapochoka ana-*loose capacity* ya ku-*focus,* leo tunaenda *emotionally.* Kwa sababu makinikia na ripoti zimesomwa mbili kwa Rais, *television* mkapeleka

nchi nzima kwenye masoko waone, sasa leo mnataka ku-*implement* jambo hilo ndani ya siku nne, kinachotokea ni nini? Kitakachotokea mtafanya makosa yale mliyoyafanya kipindi cha mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi ndiyo Serikali, haya mambo kama yana umuhimu kwa kiwango hiki wapeni Wabunge hizi nyaraka wazisome, wapeni Wabunge hizi nyaraka wazipitie. Sasa kazi ya Mheshimiwa Jenista Mhagama hapa yeye, iko siku atatokea mtu huku aseme amegundua dawa ya UKIMWI, Mheshimiwa Jenista utasimama uombe utaratibu na ukatae kabisa, kama hiyo itakuwa inatibu kwa sababu haiwezekani kila *opinion* yetu mnaikataa, tunasema hakuna nyaraka mnakataa, tunawaambia hivi mnakataa, sasa tuishauri, futeni basi upinzani tubaki chama kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi kile CCM mko peke yenu kulikuwa kuna *G7* tukiwa wadogo, mlikuwa mnashindana lakini mlikuwa hambaguani, sasa hivi tunaanza kupishana na tunaanza kubaguana. Narudia tena hiki mnachoendelea kupanda kitatoka hapo nje ya Bunge, kitakwenda mitaani. Haya yanayotokea Kibiti msishangae siku moja yakasambaa nchi nzima kwa sababu ya chuki zinazojengwa ndani ya Bunge hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema jielekeze kwenye mjadala.

**MHE. GODBLESS J. LEMA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakwenda kwenye mjadala nilikuwa najenga hoja.

**MWENYEKITI:** Nenda kwenye mjadala achana na mambo ambayo hayapo mbele yako.

**MHE. GODBLESS J. LEMA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Mbunge ni kutoa ushauri sasa nitoe ushauri gani zaidi ya huu? Huu ndiyo ushauri, nasema hizi chuki mnazojenga ndani ya Bunge ndiyo zitatoka hapo nje, zikitoka hapo nje zitakwenda mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena itafika mahali nchi hii itakuwa ni sehemu mbaya ya kuishi kwa sababu ninyi mlio wengi mmekataa kuchukua *opinion* zetu za msingi kwa sababu tu tumeitwa Wapinzani, utafikiri tumetoka Sudan sasa leo tunajadili mambo ya itifaki. *(Makofi)*

Haya mambo ya mazingira, *DC* wa Hai alikwenda akavunja vunja shamba la Mheshimiwa Mbowe, *Sea Cliff Hotel* na *Golden Tulip* ziko baharini sasa kwa sababu *issue* hapa ni itifaki ya kuridhia mazingira bora ya bahari na hizi hoteli basi zilizopo kando kando ya bahari zipigwe marufuku kabisa, ziwe mita 120 kutoka ufukwe wa bahari, kwa sababu *issue* kama leo ni itifaki ya mazingira ya bahari ambayo leo mmeilete hapa, ipi ilikuwa ni muhimu? Kwenda kuvunja shamba la mboga ama kuondoa *Sea Cliff* iliyoko pale kando kando ya bahari ambapo vichungi vya sigara vinatumbukizwa mle ndani? *(Makofi)*

Kwa hiyo haya mambo ya itifaki nilikuwa nataka tu niwaambie tu hichi ninachowaambia hivi mnavyoishi endeleeni, ila nawaaambia iko siku kama ambavyo sasa hivi hata *issue* za Kibiti mnaogopa kuzijadili utafikiri hamna kitu kinachiendelea. Kila mtu anaogopa kujadili humu ndani, Waziri wa Mambo ya Ndani naye anaogopa, nani anaogopa, Usalama wanaogopa kwa sababu mkianza kujadili tu ni kwamba jamaa wanaweza wakaja na hii inasababishwa na hasira ya wananchi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana hasira hizi ambazo mnawapandikizia wananchi, mambo haya mnayotufanyia humu ndani ya Bunge, mnatuzuia tusiseme, mnatuzuia tusitoe *opinion* zetu, ninawashauri vunjeni siasa za vyama vingi katika Taifa hili mbaki wenyewe na familia zenu na wajukuu zenu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Stephen Masele.

**MHE. STEPHEN J. MASELE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii ya kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja hii na nizungumze mambo mawili. Kwanza ni kwenye eneo la utafiti, lakini la pili ni kwenye usimamizi na utekelezaji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itifaki hii ni muhimu sana kwa Taifa letu na itaweka ulinzi wa rasilimali zetu hasa za baharini na tafiti zinazoendelea kufanyika zinaonesha kwamba kwenye bahari zetu tuna rasilimali zenye thamani kubwa sana inawezekana kuzidi rasilimali zilizopo nchi kavu. Kwa hiyo, ushauri wangu kwa Serikali ni kuongeza uwezo wa vyombo vyetu vya utafiti hasa kupitia vyuo vikuu vyetu ili tuwe na uwezo mkubwa wa kibajeti na kitaalam na sisi tuweze kufanya tafiti hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kushirikiana na vyombo vya utafiti va Kimataifa ili kujua kinachoendelea kwenye tafiti ambazo zinafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo tafiti nyingi zinaendelea hapa nchini wakati mwingine unaweza kukuta hata kwenye Wizara Serikali haitambui kama tafiti hizi zinafanyika. Kwa mfano, kuna taifiti moja inafanyika na Chuo Kikuu cha Florida cha Marekani wa kutafiti maji ya mito yetu kwa mfano Mto Wami, Mto Mara, Mto Morogoro na Mito mingine miwili hapa Tanzania lakini unakuta wale wanaotafiti hawana *coordination* kabisa na Serikali, kwa hiyo mimi ombi langu kwa Serikali kwamba baada ya kupitisha ikawa sheria basi tusimamie na tuhakikishe tunasimamia na tunashiriki katika tafiti zinazofanywa ndani na Mashirika ama makampuni ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutimize wajibu wetu kama Wabunge wa kutunga Sheria na Serikali itimize wajibu wake wa kutekeleza haya ambayo tunayapitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mkataba mmoja pamoja na Itifaki mbili na nimepata wasaa wa kuzisoma soma hapa, lakini kwa kuwa kuna dakika tano nitajielekeza kwenye mambo machache tu.

Mheshimiwa Msigwa aliposema Bunge dhaifu husababisha Serikali dhaifu amenikumbusha kauli ambayo niliisema Bungeni hapa tarehe 19 mwaka 2012. Na kinyume chake, Serikali dhaifu vilevile husababisha Bunge kuwa dhaifu na ndiyo hali ambayo tunayo hivi sasa. Bunge letu limefanywa dhaifu sana na limefanywa dhaifu na Serikali na Serikali hii ingekuwa na nguvu ingejiamini sana, isingefanya Bunge kuwa dhaifu, lakini kwa sababu Serikali ni dhaifu ni lazima na Bunge nalo liwe dhaifu. *(Makofi)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Subiri Mheshimiwa Mnyika, kuna taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mnyika kwa sababu yeye katika Bunge hili hakuwepo kwa kipindi kirefu sana na hajui nini kinachoendelea Bungeni, naomba nimpe taarifa tu kuwa Bunge lako siyo dhaifu kama anavyofikiria na Bunge letu liko *strong.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika endelea.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwombea Mwenyenzi Mungu Mheshimiwa Mlinga aweze kubadilika hiyo tabia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili limekuwa dhaifu kwa kiwango ambacho miswada, mkataba mmoja na Itifaki

mbili zinaletwa zote kwa siku moja wakati ambapo Bunge lenye nguvu lingesema kwamba siku hii tunajadili mkataba huu, tunaujadili vizuri vinatafakari hoja umetolewa. Siku hii tunajadili mkataba huu, siku hii tunajadili mkataba huu. Kwa udhaifu huu wa Bunge unaoendelea anasema sikuwepo siku nyingi. Hii siku nyingine sikuwepo si Mwenyekiti unajua mlinitoa ndiyo maana sikuwepo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya udhaifu huu Wabunge Mheshimiwa Halima Mdee hatakuwepo kwa muda wote ambao hatakuwepo, akija kurudi mtamwambia maneno haya haya. Mheshimiwa Ester Bulaya hatakuwepo hakirudi mtamwambia maneno haya haya. Sasa hii hoja ya uchafunzi wa mazingira upande wa bahari nizungumzie kwa niaba ya Mheshimiwa Mdee wa Jimbo la Kawe ambaye bahari inazunguka eneo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba hii Serikali iliisaini muda mrefu, lakini hakuna kinachofanyika kuzuia uchafuzi, hakuna kinachofanyika cha kutosha kunufaisha wavuvi. Nataka kusema nini hapa, kuridhia mikataba hii peke yake na Kambi ya Upinzani hapa inairidhia inaunga mkono kuridhiwa kwa hii mikataba haitoshi kama mwisho wa siku masharti ya msingi yaliyoko kwenye Itifaki, masharti ya msingi yaliyoko kwenye mikataba hayatekelezwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutaruhusu Serikali kuendelea kuwa dhaifu na Bunge kuendelea kuwa dhaifu ni wazi siku zote tutapitisha mikataba na sheria lakini utekelezaji hakuna. Tuna Mkataba muhimu sana hapa, huu mkataba unahusu rasilimali za kijenetiki ambao nchi iliuingia mwaka 2010 tumeletewa leo kuridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matajiri unaowakuta duniani iwe ni akina Bill Gates, iwe ni tajiri wa *Apple* aliyefariki matajiri mnawakuta duniani walipata utajiri kwa sababu ya ubunifu. Wenzetu wana ubunifu wa kiteknolojia sisi tunawabunifu wengi sana ambao wangeweza kunufaika na rasilimali za kijenetiki kwenye ugunduzi wa dawa, tiba, vitu

na mbalimbali lakini kwa sababu mambo haya hatuyafanyi vile inavyostahili ndiyo maana hatufiki pale ambazo tunafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumeingia katika sekta ambayo wengine ndiyo tunadhani ina manufaa zaidi ya madini. Kumbe huku kuna madini kwenye jenetiki, lakini hatufanyi ipasavyo. Hata kwenye madini tumewaambia muda mrefu leteni mikataba hapa Bungeni tumewaambia muda mrefu leteni mikataba leteni mikataba, tumeimba kwa miaka mingi leteni mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mnatuletea hoja mnasema kwamba tunaleta sheria ya kulipa Bunge mamlaka juu ya mikataba halafu mnataka *propaganda* kama vile sisi ambao ndiyo tulikuwa tunasema mikataba iletwe tunakataa, sisi tunachokataa ni kwamba ninyi wa kuzileta sheria kwa Hati ya Dharura mnatunga sheria mbovu ambazo mwisho wa siku hazileti tija ambayo inasukudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli ninyi mnataka kuisaidia nchi kwenye masuala ya madini, hata kama tukianzia na hapo ambapo nilisema Rais angekuwa makini asingeanzia na makinikia angeanzia na madini. Hata kama tukiamua kuanzia na makinikia cha kwanza ambacho Bunge ingetaka kwenye Bunge hili kabla hata kuletewa miswada kusoma kwa mara ya kwanza zile ripoti mbili zile, zile ripoti alizokabidhiwa Mheshimiwa Rais, ipaswa ziwasilishwe hapa Bungeni Mawaziri wazisome tuzijadili Wabunge halafu tuseme sasa Serikali kaandae mapendekezo ya muswada ya kuhusu hiki, kuhusu hiki, kuhusu hiki, iletwe hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nachotaka kusema hapa ni kuwa, badala ya kuanza kujadili Miswada ya Sheria kwa Hati ya Dharura, Bunge hili liletewe kwa udharura huo huo ripoti mbili za Rais kuhusu makinikia, zisomwe hapa Bungeni, zijadiliwe hapa Bunge msipofanya hivyo ile kauli niliyosema kwamba Rais makini alipaswa kuanza na madini kabla ya makinikia kuna siku itakuja kuwatafuna.

Mheshimiwa Lema amesema kwamba kama hamtasikia maoni yetu basi ni afadhali mfike hatua mfute Kambi ya Upinzani. Mheshimiwa Lema kabla hawajafuta Kambi ya Upinzani kama wataendelea kutosikiliza maoni yetu imefikia hatua Watanzania waiondoe hii Serikali madarakani. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mmechelewa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnadhani tumechelewa, kama mnashindwa tu kuwadhibiti wale watu wa Kibiti, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, kama mnashindwa kuwadhibiti watu wa Kibiti wanaotumia silaha, ndugu zangu hamuwezi kuwadhibiti Watanzania hawa wakiamua kutumia silaha yao, kadi yao kupigia kura kwenye sanduku la kura. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika jielekeze kwenye hoja, mambo ya Kibiti hayahusiani na utafiti. Jielekeze kwenye hoja ambayo iko mbele yako. *(Kicheko)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema haya kwa sababu kule Kibiti...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante muda wako umekwisha kengele ilishapigwa. Mheshimiwa Musukuma mchangiaji wetu wa mwisho mjiandae watoa hoja kwa majibu. Waziri, Naibu Waziri na wengine nitawapa muda wenu.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme maneno machache sana kwa leo, hii safari tuliyonayo ya kuibadilisha Tanzania hawa wenzetu hawako na sisi. Kwa hiyo, ni kama tunampigia mbuzi gitaa. Hakuna mtu aliye tayari kusafiri na hii kasi tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza rafiki yangu hapa amechangia anasema tunaletewa Hati za Dharura, toka nimekuwa Bungeni taarifa zote za Kamati huwa tunapewa hapa, zinasomwa tunaanza kuchangia, sijaona jipya wakisoma taarifa tunagawiwa na sisi hapa tunasoma baadaye tunaanza kuchangia. Sasa kama ninavyowaona hawa, mtu mwenye akili hata kama ungepewa siku kumi huwezi kuelewa ambaye huna akili. Lakini mwenye akili haya masuala tumeshapewa leo na Kamati ya Uongozi imeshakaa imeshauriana sioni sababu ya kushindwa kuendelea na kujadili. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuruku sana. Ndugu yangu, shemeji yangu Musukuma alisha-*declare* kwamba shule hajaenda sana, kwa hiyo hata akipewa dakika mbili akapitia tu kichwa cha habari akaanza kuchangia ataogelea tu! Lakini watu wenye akili zao wanahitaji muda wa *concentration*, wanahitaji muda wa kufanya *reference point,* duniani kote wenzetu walifanyaje hiyo ndiyo taarifa muhimu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara kaa chini. Mheshimiwa Musukuma endelea.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wamemsikia Mheshimiwa anayejiita shemeji yangu kwa kusema nilisha-*declare* mimi sijasoma. Ni bora ukasema mimi ni darasa la saba kuliko kuwa na hivyo vyeti ulivyo navyo wakati akili huna. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumza haya maneno yanayozunguzwa humu ndani, yote haya ni *propaganda* kinacholengwa humu ni makinikia. Hawa watu

wanachokitaka ni safari ya kurefusha mjadala kwamba tusijadili hizi sheria ili tukabanane na wazungu tulipwe pesa, lengo lao ni kurefusha masafara ili wakatafute *cross-cross* kule Morena walikokuwa wanakaa. Hatukubaliani nayo ngoma imeletwa tupige leo hii hii tumalize.

Nafahamu hawa wenzetu hawana uchungu na hii miswada mara nyingi hawana uchungu, sisi wenzenu tulioumia tunatamani hata ingepigwa siku moja hii sheria ambayo inataka kwenda kumbana mzungu atulipe pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tuende na ile *slogan* ya juzi kwamba hela zikitoka hawa tusiwape, zije kwenye majimbo yetu sisi wenye shida. Haiwezekani mtu anasimama hapa anazungumza anasema Wabunge tumekaa miezi mitatu tumechoka kutafuta nini wakati tunalipwa pesa, tuongezwe hata wiki mbili. Watu wenyewe njaa humu zimetuua humu watu mkifukuzwa mnatoa macho, halafu unakuja kuanza kuzungumza vitu vya ajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiria masuala haya yaende kama yalivyopangwa na hakuna mambo ya kutishana mambo ya Kibiti kuna nini. *(Kicheko)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge anayezungumza amekuwa na tabia ya kuongea lugha ambazo siyo za Kibunge. Kama sasa hivi anasema tumetoa macho, tunalia na kwamba kuna watu wamehongwa Morena, na yeye ndiye anayekaa Morena sasa tungeomba ili Bunge liwe na hadhi kama kuna watu wamechukua hela ana ushahidi awataje. Maana asikae ana tisha tisha watu hapa watu. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Musukuma endelea.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, unajua Waheshimiwa Wabunge Spika anatuelekeza vizuri uwe na tabia ya kuwasiliza na wenzio huwa tunavumilia, wewe umesema hapa tumekuwa Bunge la vibogoyo, kutoa macho unaumia? Na kweli umeyatoa macho! Tunawaona hapa mkifukuzwa mnavyotoa macho kule mtaani. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo suala la kuzungumza kukodoa macho au watu wamehongwa ni maneno yako tu na vitendo vyako vinadhihirisha kwenye Umma. Hivi kweli unategemea hiyo Serikali ya kuitoa CCM ya ninyi mnaowatetea wezi kwa *style* hii! Serikali ya ninyi mnaokataa kujadili Miswada ya kwenda kudai pesa zetu. Mimi nilikuwa nashauri tu kwamba hawa wenzetu hawapo pamoja na sisi katika safari ya kuibadilisha Tanzania, hapo wamekaa tu kizungumkuti lakini muda wowote walikuwa wanaondoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana......

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mweyekiti, ahsante kwa mjadala wako.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Wewe bwana kaa chini. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri mjadala umeuona kambi zote wameridhika pokea ushauri, dakika tano.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunawashukuru sana Wabunge wote waliopata

nafasi ya kuchangia ambao wamechangia vizuri sana kuhusu hoja hii na bahati nzuri wote Mkataba pamoja Itifaki zote mbili zimeungwa mkono na Bunge hili na kwamba hakuna upande wowote ambao umepinga, tunaahidi kwamba yale mapendekezo waliyoyatoa Waheshimiwa Wabunge tutayazingatia katika kuhakikisha kwamba tuna usimamizi bora wa mkataba pamoja na itifaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme moja la nyongeza katika hayo kwamba Serikali hapa imelaumiwa katika kuleta nyaraka. Serikali inaonewa kwa vipi katika jambo hilo? Siyo kazi ya Serikali kugawa nyaraka Bungeni. Kazi ya Serikali tulipoingiza kazi za Serikali katika Mkutano huu wa Saba tuliainisha kazi zote na nyaraka zote tuliwasilisha.

Kwa hiyo, siyo kazi ya Serikali tena kulaumiwa kuhusu nyaraka na kwa Wabunge wanaojua kufuatilia nyaraka kama rafiki yangu hapa amekuwa akilalamika na ni mkongwe kabisa anajua, Serikali ikishaorodhesha kazi zake *document* zipo kwa Katibu wa Bunge. Hivyo, Serikali haihusiki tena katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoleta mikataba hii na itifaki hizi, haimaanishi kwamba Serikali haijafanya lolote katika utekelezaji wa majukumu yake. Serikali tumefanya mambo mengi katika usimamizi wa Bahari Kuu pamoja na Ukanda wa Pwani, hilo lazima lifahamike. Sheria na kanuni nyingi zimetungwa na usimamizi wa usiku na mchana kuhakikisha kwamba Ukanda wa Pwani unalindwa katika uchafuzi, unalindwa katika uharibifu wa mazingira ambayo yanaweza yakafanyika Ukanda wa Pwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi pia iongelee kuhusu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Tumeshauriwa kwamba mali zetu zimekuwa zikiibiwa kwa utaratibu huu, wizi wa rasilimali za kijenetiki kwa mfumo wa watu wanajifanya ni watafiti na wafanyabiashara na tukaombwa kwamba tuweke mwongozo mahsusi ambao utalinda rasilimali zetu zisiweze kuporwa tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwaambia kwamba Kambi zote bahati nzuri imezungumzwa na Kamati yenyewe ya Viwanda, Biashara na Mazingira na imezungumzwa na Kambi ya Upinzani na Serikali haina tatizo katika hili. Tutaandaa mkakati mahsusi ambao unadhibiti wizi wa aina yoyote katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maisha ya Pwani yamekuwa bora vipi toka mwaka tulivyoridhia. Amezungumza Makamu Mwenyekiti wangu enzi hizo wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara kwamba wamenufaika vipi Pwani pamoja kuridhia mwaka 1996. Wamenufaika kwa mengi, moja ni kwamba miradi mingi sana inayojengwa sasa hivi tuna ujenzi wa kuta katika Pwani kwa maana ya Pangani, Rufiji, Zanzibar, Pemba na Kilimani zinajengwa. Tunapanda mikoko katika maeneo yaliyoharibiwa ya pwani, tunaanda mikoko Rufiji, Zanzibar na maeneo mengine ili kuhakikisha kwamba tunanusuru. Pia tunajenga mifereji maene ambayo yanaathiriwa na kuongezeka kwa kina cha bahari ili kuweza kuhimili pia maji ya mvua ambayo yanaleta mafuriko makubwa kwa wananchi, kama kwa rafiki yangu hapa Mheshimiwa Mtolea kule miradi mbalimbali inaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hatujakaa, tunacho chuo kikubwa sana ambacho wamekisifu sana Kamati hapa, hiki chuo chetu cha Taasisi ya Sayansi ya Bahari ambacho kinafanya kazi kubwa na kimejengwa Zanzibar kwa maana hiyo hiyo ya kuhakikisha kwamba ukanda wa pwani unalindwa kwa nguvu zote na tafiti zinapatikana kwa wakati na kutumika kwa wakati. Sio hivyo tu, tumeanzisha sheria mbalimbali nyingi za kulinda mazingira yetu katika ukanda wa bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi za tafiti zinafanya vizuri tu, *COSTECH* na *IMS* katika kuhakikisha kwamba Ukanda wa Pwani unanufaika hasa katika maeneo ya ufugaji wa samaki, mwani pamoja na mazao mengine ya bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji mmoja alisema

kwamba Tanzania imegeuzwa kuwa dampo na sisi hatusimamii. Ni kweli tuna haja tu ya kuongeza usimamizi, lakini ni kweli kabisa mipaka yetu yote tunailinda, ndani ya eneo la bahari yetu tunalilinda kwa nguvu zote na taasisi za Serikali zipo kazini. *NEMC, SUMATRA* na *TPA* wapo kazini kuhakikisha kwamba kwa namna yoyote meli zinapongia ndani katika eneo letu hili udhibiti wa uchafuzi wa mazingira hauruhusiwi kwa aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata upande wa kemikali tupo vizuri, sawa zinaweza zikatokea kesi mbalimbali ambazo zipo hapa nchini za umwagaji wa sumu katika bahari yetu na katika kingo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, mambo mengine uwajibu kwa maandishi. Mheshimiwa Mtoa Hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa na niwashukuru Wabunge wote kwa umoja wao kwa kuridhia mapendekezo haya ya maazimio pamoja na itifaki tuliyoweka mezani. Kwa kuwa wameridhia kama ulivyosema sitakuwa na mengi ya kusema, niseme mawali tu ambayo yameleta sura za tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Serikali *strong,* yenye nguvu ni Serikali inayochukua hatua, inatenda na siyo Serikali inayosema na hiki ndicho kinachoendelea. Mheshimiwa Mnyika anaposema tumeongea sana kwenye mikataba na anajua ukubwa wa mambo yale, lakini Serikali jasiri na yenye nguvu imeenda kwenye kutenda, hicho ndicho ambacho Wabunge na Watanzania wote wametamani muda mwingi sana kukiona na ndicho ambacho Mheshimiwa Rais anakwenda kukitenda na analiomba Bunge lione umuhimu huo kwa ukubwa wa rasilimali za nchi yetu na ukubwa wa jambo lenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ukigeugeu ndiyo ambao huwa unaweka mashaka kwamba mtu ambaye ameliongea kwa muda mrefu sana jambo, linapoletwa anageuka inaleta maswali kwamba huyu mtu amegeukaje. Nimemshukuru sana ndugu zangu hapa walipokuja kuongelea kwamba siyo kila kitu kupinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili jambo ambalo lina maslahi ya Taifa, niwaambie Waheshimiwa Wabunge hata kama ataunga mkono mtu mmoja tu, Serikali hatuwezi tukarudi nyuma maadam tumepewa dhamana ya rasilimali za nchi yetu. Wabunge na kama Serikali na Wasaidizi wa Rais tunawahakikishia kwamba nia na dira aliyonayo Rais ni njema sana kwenye rasilimali za nchi yetu. Nawaombeni twende tuunge mkono wala tusipepesuke kwa kuzingatia vitu vingine ambavyo haviko kwenye dira yetu visije vikatutoa kwenye dira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi sana ambayo yamo kwenye itifaki hizi yalishaletwa mbele ya Wabunge na Wabunge wameshafuatilia na yamefanyiwa kazi na watalaam ambao wana dhamana na wenyewe kwenye Taifa letu, hatuna haja ya kuwa na mashaka, niwaombe tuende turidhie ili yaweze kwenda kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine Waheshimiwa Wabunge tunapoongelea ameongea Mheshimiwa Lema na Mheshimiwa Mnyika, ni vema sana tukawa makini sana tunapoongea. Nimemsikia akiongelea suala la Kibiti, lakini ningekuwa nakuuliza maswali mengi, najua usingepata majibu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kama una uhusiano na wale wahalifu hata ukadhani wameshinda, hebu waulize walianza wangapi na sasa wapo wangapi. Mwenzio Lema kwa sababu alikuwa kule gerezani anaweza akawaona wengine kule, wewe Mheshimiwa Mnyika ambaye hujaenda unaweza ukatusaidia, wewe unayedhani wameshinda wapo wangapi na wapo wapi? Lakini nikuhakikishie kwamba sisi kama Serikali hatutaacha eneo hata moja la nchi yetu hii

likatawaliwa na uhalifu. Tutashughulika na mmoja mmoja na lazima haki ya watu wetu itasimama katika eneo lote la nchi yetu watasimama wakiwa wanafanya kazi kwa mazingira yaliyo salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaongea kimzaha mzaha, lakini taswira iliyopo ndani kabisa na niliisema mahali pengine, ina taswira hiyo ya siasa siasa. Leo hii ukituambia kwamba yale yanayoendelea Kibiti yataenda na maeneo mengine, tunaendelea tu kutafuta *connection* unajuaje kwamba yanaendelea na maeneo mengine. Kwa sababu kama anauawa Mwenyekiti wa CCM, anauawa wa CCM, wanaruka nyumba ya yule asiye wa CCM na wewe unasema yataendelea na maeneo mengine, una haja ya kutusaidia kujua kwa nini yataendelea na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini unadhani kwamba wanashinda,kwa sababu sisi kwenye mpango kazi wetu tuliopanga, tunaenda hatua kwa hatua kuhakikisha kwamba wananchi wa maeneo yote ya nchi yetu wanakuwa katika mazingira salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sentensi kama hizi pamoja na kwamba zimesemewa Bungeni nadhani kuna umuhimu sana ndugu zetu hawa watasaidia kujua kwamba kumbe sisi tunavyotafuta sana kumbe kiini ama kinatoka Bungeni au Serikalini, lakini sasa wanaenda kuhangaika na wananchi ambao ni *very innocent,* ndiyo maana sisi tunakuwa *very responsible.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu kwenye mambo ya siasa tunatakiwa tupambane sisi wanasiasa na siyo wananchi wengine ambao wanashughulika na shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda umeisha, ninaomba tu kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa katika Mkutano wake wa Saba liridhie Maazimio tuliyoyaleta pamoja na marekebisho na Itifaki tuliyoleta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja hiyo imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kwa mujibu wa kanuni zetu za kibunge. Kwamba Bunge sasa liridhie marekebisho ya Mkataba wa Nairobi wa Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi *(Amended Convention for the Protection Management and Development of Marine and Coastal Environment of the Western Indian Ocean).*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja liiamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji Azimio lingine kuwa Bunge sasa liridhie Itifaki ya Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi kutokana na Vyanzo na Shughuli zinazofanyika Nchi Kavu *(Protocol For The Protection of the Marine and Coastal Environment of the Western Indian Ocean from Land base Sources and Activities). (Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Azimio la mwisho, kuwa Bunge liridhie Itifaki ya Nagoya ya Kusimamia Upatikanaji na Mgawanyo Sahihi wa Faida Zitokanazo na Matumizi ya Rasilimali za Kijenetiki *(Nagoya Protocol on Access to Genetic Resources and The Fair and Equitable Sharing of Benefits Arising from their Utilization to the Convention on Biological Diversity). (Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Azimio hili nalo limepita. Nichukue nafasi hii kuwapongeza sehemu zote mbili za Bunge kwa kupitisha Maazimio haya muhimu. Wengine hamjui, tuna mabaharia wetu ambao wangeweza kupoteza kazi kesho kama Maazimio haya yasingepita, wale Mabaharia ambao wanafanya kazi Kimataifa. Hivyo, nawapongeza wote. *(Makofi)*

Lakini Serikali chukueni ushauri mliopewa, kuna *reservations* ambazo mkiingia kwenye itifaki, muhusika anayo haki ya kuingiza *reservations* zake ili zikubaliwe, bahari zetu zilindwe na bahari zetu zisimwagiwe sumu, kwa sababu sumu hizi zinaharibu mazingira na viumbe hai ndani ya bahari. Kwa hiyo, nawapongeza wote, naipongeza Serikali na upande wa Vyama vyote kwa kupitisha Maazimio haya matatu, kazi haikuwa ndogo lakini tumevuka. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna semina ya *Red Cross* sasa hivi, kwa hiyo nawaomba Waheshimiwa Wabunge msiondoke mhudhurie semina ya *Red Cross* ambayo ni muhimu sana na itaratibiwa na *Tanzania Red Cross* na itafanyika ukumbi huu wa Bunge kuanzia sasa.

Waheshimiwa Wabunge, ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.30 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 30 Juni, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*